Ufafanuzi Wa Agano Jipya

1 Petro - Yuda

Na Dorothy Almond

mwisho na Askofu Francis Ntiruka

www.africanpastors.org

Ufafanuzi Wa
Agano Jipya

1 Petro - Yuda

Dorothy Almond

© African Pastors Fellowship 2010

Kimetolewa na:
AFRICAN PASTORS FELLOWSHIP
Station House, Station Approach, Adisham
Canterbury, Kent CT3 3JE
United Kingdom

www.africanpastors.org

WARAKA WA KWANZA WA PETRO MTUME

YALIYOMO

UTANGULIZI

a) Mwandishi wa Waraka
b) Mahali pa kuandikwa kwa Waraka
c) Walioandikiwa Waraka
d) Tarehe ya kuandikwa kwa Waraka
e) Sababu za kuandikwa kwa Waraka

UFAFANUZI

1: 1-2 Salaam
3-12 Wokovu, hali yake na ufunuo wake
13-25 Mwito wa kuishi maisha ya tofauti
2: 1-3 Hamu ya kukua kiroho
4-10 Heshima ya kuwa katika jamii ya Watu wa Mungu
11-25 Ushuhuda katika ulimwengu
3: 1-7 Maisha ya nyumbani
8-12 Warithi wa baraka na jinsi iwapasavyo kuishi
13-17 Kuvumilia mateso
18-22 Kielelezo cha Kristo
4: 1-6 Kujitoa kabisa kwa mapenzi ya Mungu
7-11 Wajibu mbalimbali
12-19 Kukubali mateso kwa furaha
5: 1-5 Maagizo kwa wazee
6-11 Maagizo juu ya mambo kadha wa kadha
12-14 Salaam za kuagana

UTANGULIZI

a) Mwandishi wa Waraka

Ni Mtume Petro kama isemavyo mwanzoni mwa Waraka (1:1). Ndani ya Waraka ushuhuda umo wa kulithibitisha neno hilo. Kwa mfano katika 5:1 ni maneno ya mtu aliyeyaona mateso ya Kristo („shahidi wa mateso ya Kristo") vilevile na maneno ya 2:20-25. Pamoja na hayo Waraka umetaja sana tabia za Bwana Yesu Mwenyewe (1:13; 2:20-25; 3:14; 4:14) wala si ajabu kama umeandikwa na mmoja aliyeandama na Yesu kwa miaka mitatu ya huduma yake.

Wataalamu wachache hawakubali kwamba Petro alikuwa mwandishi. Hasa sababu yao yahusu hali ya Kiyunani cha Waraka. Ni Kiyunani safi ambacho wao wadhani kwamba mtu aliyekuwa mvuvi kama Petro asingaliweza kukiandika. Pamoja na sababu hiyo wengine wafikiri kwamba hali ya mateso iliyotajwa ni ile ya baadaye, wakati Wakristo walipoteswa kwa sababu ya kuwa Wakristo tu.

Lakini watu hueleza mambo hayo kwa kusema kwamba iwapo Petro mvuvi hakuelimishwa katika shule za marabi (ndiyo maana ya Mdo.4:13) siyo kusema Petro hakujua Kiyunani. Katika safari za kuieneza Injili na kukutana na watu mbalimbali alipata nafasi ya kujiendeleza katika lugha hiyo. Pia kutokana na maneno ya 5:12 „kwa mkono wa Silwano.....nimewaandikia kwa maneno machache...." Petro alisaidiwa na mkalimani, Silwano. Kama Silwano aliichukua barua tu ingalitosha kusema „natuma barua kwa mkono wa Silwano". Pengine Petro alimjulisha alivyotaka kuandika na Silwano aliandika aliyoambiwa na Petro kwa kutumia maneno yake mwenyewe.

Kuhusu hali ya mateso Petro alisema iliwezekana wateswe kwa Imani, ila hasa wajihadharini wasije wakateswa kwa ajili ya makosa yao si kwa imani yao. Katika 2:13-15 Petro hakutazamia watateswa wakifanya vizuri. Hata hivyo, katika 4:12 picha ni tofauti, alisema juu ya „msiba ulio kati yenu". Huenda shida imetokea mahali fulani iliyomfanya atumie lugha hiyo ila haikuwa kawaida ya kila mahali na ya kila wakati. Katika karne ya pili hali ilibadilika na mtu aliteswa akiwa Mkristo tu.

b) Mahali pa kuandikwa Kwa Waraka

Mwisho wa Waraka Petro alitaja „Babeli" na kutuma salaam za „Marko, mwanangu" aliyekuwa pamoja naye. Katika Ufunuo 16:19; 17:15 Jiji kuu la Dola ya Kirumi liliitwa „Babeli" kwa kuficha mahali. Ila Petro hakuwa na sababu ya kupaficha mahali alipo. Watalaamu wengi hufikiri kwamba Petro alikuwa Rumi. Hasa kwa sababu ya kumtaja Marko. Huyo Marko (Yohana Marko) amefikiriwa kuwa yule kijana aliyekwenda na Paulo katika Safari kubwa ya kwanza ya Injili halafu akaachana naye pale Perge (Mdo.13:13). Baadaye alikuwa huko Rumi pamoja na Paulo aliyetazamia kumtuma Asia Ndogo (Kol.4:10) halafu katika 2 Tim.4:11 alikuwako Asia Ndogo na Paulo alituma habari kwamba alitaka arudi kwake Rumi. Huenda Paulo na Petro walikuwa pamoja huko Rumi wakati fulani.

c) Walioandikiwa Waraka

Tumeambiwa ni watu walioishi kaskazini ya Asia Ndogo mbele ya Milima ya Taurus. Ni vigumu kujua kwa usahihi mahali pao maana Petro ametumia majina ya nchi na ya falme za zamani pamoja na majina ya Majimbo ya Kirumi kwa maeneo yaliyoingizwa katika Dola baada ya Warumi kuyashinda. Petro alitumia sana Agano la Kale katika Waraka. Je! alikuwa akiwaandikia

Wayahudi hasa? Si lazima tufikiri hivyo maana yeye mwenyewe alikuwa Myahudi na alijua Kanisa la Kikristo limerithi mahali pa Israeli ya zamani na ahadi zilizotolewa kwa Watu wa Mungu wa zamani. Ni dhahiri kwamba Wakristo wa KiMataifa waliandikiwa pia, tazama 1:14,18; 2:9,18ku; 4:3-5.

d) Tarehe ya kuandikwa kwa Waraka

Waraka uliandikwa kama B.K.63/64 wakati wa Utawala wa Kaisari Nero. Petro hakusema lolote juu ya Paulo kuuawa. Mapokeo yasema Petro na Paulo waliuawa Rumi kama B.K.64.

e) Sababu za kuandikwa kwa Waraka

Barua ilitumwa kwa shirika zilizokuwa hapo na pale katika sehemu zilizotajwa. Huenda baadhi yao zilikuwa za Wakristo wapya, vikundi vya waumini wachachechache. Shabaha ya Petro ilikuwa kuwatia moyo wa kushikilia sana imani yao, hasa wakati wa mateso na magumu, ili wafahamu kabisa kwamba hii ndiyo njia kwa kuwa hata Bwana wao, Yesu Kristo, alikanyaga njia iyohiyo, budi na wao waikanyage. Petro alisisitiza sana jambo la maisha safi na jinsi ya kuishi katika mambo ya kila siku, nyumbani, kazini, na kati ya jamii. Alisema kwa wazi kuhusu hali na tabia zilizotakikana na matendo yaliyowapasa.

UFAFANUZI

1: 1-2 Salaam

Petro alijiita “Mtume wa Yesu Kristo” mtu aliyeitwa na Yesu Mwenyewe na kupewa Utume pia Uongozi kati ya Mitume wenzake. Aliandama na Bwana Yesu na kuyasikia aliyoyasema na kuyaona aliyoyafanya. Kwa hiyo aliwaandikia kwa mamlaka ya KiMitume.

1b Aliwaandikia “wateule wa Utawanyiko wakaao hali ya ugeni katika Ponto, na Galatia, na Kapadokia, na Asia, na Bithinia”. Maneno “wateule wa Utawanyiko” yatuelekeza kufikiri ni Wakristo wa Kiyahudi walioandikiwa, ila katika sehemu za Waraka ni wazi kwamba maneno yake yaliwahusu Wakristo wa KiMataifa (1.14,18; 2.9,18ku, 4.3-5). Hivyo Waraka uliwahusu Wakristo wote, wa Kiyahudi na wa KiMataifa, waliotawanyika huko na huko katika sehemu zilizotajwa. Pia ni ukumbusho kwamba Wakristo ni “wageni” hapa duniani, „nyumbani“ si hapa, wao ni raia wa mbinguni. Petro alikuwa akiwafikirisha wawaze kwamba wao ni wageni na wasafiri (2.11). Neno “wateule” laonyesha uhusiano wao na Mungu. Kwa ulimwengu ni wageni, ila kwa Mungu ni “wenyeji” ambao Mungu amewateua kuwa Wake.

Sehemu zilizotajwa zilikuwa kaskazini ya eneo la Asia Ndogo. Inaonekana Petro alitumia majina ya majimbo ya Kirumi pamoja na majina ya asili ya nchi. Katika Safari kubwa ya pili ya Injili Paulo hakuruhusiwa kuhubiri katika nchi za

Asia wala Bithinia (Mdo.16:6-7) Hatuna habari juu ya Petro kufanya kazi katika sehemu hizo wala hatujui uhusiano wake nao ulitokeaje.

k.2 Petro (kama Paulo katika Nyaraka zake) aliwatakia baraka kubwa za Injili, neema na amani. Pia alitaka wazijue zaidi na zaidi. Neema ni msingi wa uhusiano wote kati ya Mungu na watu wake na amani ni tunda lake. Kutokana na upatanisho uliofanywa na Kristo Msalabani, Mungu huwapokea na kuwatendea watu kufuatana na ustahili wake Kristo si kwa ustahili wao.

1: 3-12 Wokovu, hali yake na ufunuo wake

Alipokumbuka baraka nyingi kubwa za wokovu, Petro alimshukuru Mungu sana sana. “Ahimidiwe Mungu, Baba wa Bwana Yesu Kristo” ndipo aliendelea kwa kuzitaja hizo baraka kubwa za wokovu.

Asili ya wokovu huo wa ajabu ni rehemu nyingi za Mungu. Katika Agano Jipya rehema ya Mungu imeeleza kuwa fadhili zake hasa katika kuwaleta Kwake wenye dhambi, na wasiostahili, na walio mbali, na walio nje, mfano wa WaMataifa ili waushiriki wokovu na utukufu na utajiri wa Kristo (Rum.11:30-32; 15:9; Efe.2:4; Tito.3:5). Ni Bwana Yesu Kristo aliyeutengeneza wokovu. Yeye ni Yule Masihi aliyeahidiwa na Mungu, pamoja na kuwa Bwana aliyewekwa na Mungu kuwa Mkuu (Mdo.2:36). Huyo ni „wetu" kwa sababu amefanya hayo yote kwa ajili yetu, Yeye yuko kwa shabaha ya kutuletea baraka za Kufa na Kufufuka Kwake.

Wokovu ni nini? Petro alieleza wokovu ni kuzaliwa kwa mara ya pili akisema Mungu „alituzaa" kwa hiyo ni kazi ya Mungu ambaye Anafanya uumbaji mpya, jamii mpya wa binadamu, na wasomaji wake wameingizwa katika jamii hiyo na kushirikishwa uzima wake (1.23; Yn.3:3). Kutokana na hayo mabadiliko makubwa mazuri yametokea, hali yao na tumaini lao vimebadilika (2.24; 3.18).

Tokeo la wokovu ni waumini kupewa tumaini lililo hai kwa sababu ya Kristo kufufuka kutoka wafu. Tumaini ni hai kwa sababu Kristo ni hai, na kwa kuwa wamezaliwa mara ya pili wameushiriki uzima wa Kristo asiyepatikana tena na mauti (Rum.6:8-9). Wala tumaini lao haliwi katika jambo la mbele tu, hata limegusa na kukolea hali ya kuishi kwao sasa. Mtu wa tumaini anaishi tofauti sana na yeye asiye na tumaini.

k.4 Pamoja na hayo wamefanywa kuwa warithi wa Ufalme wa Mungu na wa uzima wa milele. Zamani za Agano la Kale Waisraeli walitoka nchi ya utumwa wakaingia nchi ya ahadi, nchi ya Kanaani. Kila kabila lilipewa fungu lake, ndipo walipoingia Kanaani kila kabila lilirithi sehemu yake kufuatana na ahadi waliyopewa. Vivyo hivyo, kila muumini, na waumini wote kwa pamoja, wamepewa fungu katika Ufalme wa Mungu, wamefanywa kuwa warithi, nao watauingia urithi wao mbeleni (Kol.3:24).

Urithi ni wa namna gani? Ni mzuri sana, na maneno aliyoyatumia Petro yaonyesha uzuri wake; „usioharibika, usio na uchafu, usionyauka". Ni urithi usiofanana na urithi wowote wa hapa duniani. Haupatikani na uharibifu wa aina yoyote, haupatikani na uchafu wa aina yoyote, wala hauguswi na ubaya wa aina yoyote, maana yake, hakuna kitu cha nje kiwezacho kuugusa na kuuharibu, wala hamna kitu cha ndani kiwezacho kuunyausha na kusababisha maozo. Ni urithi usiochakaa wala uzuri wake hautapungua.

Zaidi ni urithi unaotunzwa vizuri sana. Kwanza unatunzwa mahali pazuri, pale mbinguni, mahali pa usalama kabisa. Pia, unatunzwa kwa ajili yao. Hilo ni jambo la ajabu. Ni urithi unaowangojea na katika umilele wataufurahia.

Tukiuliza, urithi huo ni nini hasa? Iwapo mengine yapo, hasa twaweza kusema ni Bwana Mwenyewe, Yeye ndiye fungu la watu wake (Zab.16:5). Yeye ameitwa „hazina" (Kol.3:1-3; Mwa.15:1; 1 The.4:17; 5:9-10; 1 Yoh.3:2). Bila shaka mazuri mengi yamefungana na Bwana Yesu na waumini watayashiriki hayo yote.

k.5 Urithi unalindwa mbinguni huku waumini wanalindwa duniani. Neno la Kigriki lililotumika kwa „kulindwa" ni neno la kijeshi. Waumini wanalindwa na nguvu za Mungu wakati wote wa kusafiri kwao hapa duniani mpaka watakapofika salama salamini huko mbinguni mwisho wa safari ndipo wataingia urithi waliowekewa. Wahubiri wa zamani zile waliamini kabisa kwamba wale walioitika wito wa Injili na kumwamini Kristo, hakika Mungu huwashika na kuwapitisha katika majaribu na mateso yao yote (Flp.1:6; 1 Kor.1:8).

„kwa njia ya imani" Kwa upande wao walitakiwa kuwa na imani na kuzitimiza wajibu zao na kuendelea kuishi kwa imani. Hakika Mungu kwa upande wake atawalinda.

k.5b Wokovu unaosemwa hapo ni wokovu utakaopata matimizo yake mbeleni. Ni wokovu ulioandaliwa tayari, nao utatimizwa kwa wakati wake, imebaki ufunuliwe kwa ukamilifu baadaye. Iwapo wameokolewa na kuzionja baraka zake katika maisha ya kila siku, hata hivyo, uzuri wake wa ajabu utadhihirika katika Sikukuu ya baadaye, Kristo atakapotokea tena. Ndipo wataufurahia kabisa wokovu timamu (Rum.13:11; Ebr.1:14; 9:28).

1.6 Baraka ya kuwa na urithi mzuri sana na baraka ya kulindwa na nguvu za Mungu zilitosha kuwatia moyo wa kuishi kwa furaha iwapo walikuwa wakijaribiwa kwa njia mbalimbali. Wala si ajabu wafurahi wakiyalinganisha majaribu yao ambayo ni ya muda tu na matazamio ya mambo mazuri sana ya kudumu yaliyo mbele yao.

k.7 Mungu aliruhusu wapatwe na majaribu kwa sababu kwa njia hiyo imani yao ilipimwa na ukweli wake ulithibitishwa. Pia imani yao ilisafishwa. Kwa nini iwe hivyo? ni kwa sababu imani ni kitu cha thamani sana, budi ipitishwe katika „moto" wa kuijaribu, moto ni mateso, dhiki, na magumu, ambayo waliyapata kwa ajili ya kumwamini Kristo. Hivyo walijulikana kuwa wafuasi wa kweli. Pamoja na hayo yote Kristo naye alisifiwa kwa jinsi walivyomthamini kiasi cha kumfuata kwa uaminifu haidhuru walipatwa na shida gani.

Imani ni kitu cha thamani mno ipitayo thamani ya dhahabu ambayo ni ya muda na baadaye hupotea. Wakati mgumu Wakristo walihitaji kutiwa moyo wa kuendelea kumwamini Kristo. Iliwapasa wayapokee majaribu yao kwa furaha, hali wakijua ukweli wa imani yao utadhihirika. Wakumbuke kwamba hata Kristo naye aliikanyaga njia hiyo naye amewaita wote watakaomfuata waubebe msalaba.

Pia twaona kwamba majaribu yote ni ya muda mfupi na urithi ni uzima wa milele (2 Kor.4:17). Majaribu yaliyozungumzwa ni shida zilizotoka nje yao. Majaribu huleta huzuni, lakini huzuni ya namna ile isiyoizima furaha ya kweli. Ajabu ni kwamba Mkristo hufurahi wakati uleule wa kuhuzunishwa (Rum.5:2-4; 8:18; Yak.1:2-4).

k.8-9 Waraka wa Paulo kwa Wafilipi wasema sana juu ya furaha. Iwapo wakati ule Paulo alifungwa alisikia furaha sana moyoni mwake na aliwasihi Wafilipi pia wafurahi. Hapo twaona Petro alikaza neno la furaha, alitaja „furaha isiyoneneka" kwa hiyo ni dhahiri kwamba imani ya Kikristo ni ya kipekee, kwa sababu waumini waweza kuwa katika dhiki na majaribu na kusikia huzuni, huku pia wasikia furaha kubwa. Kwa nini? Kwa sababu wanampenda Bwana Yesu bila kumwona. Kwa kumwamini kabisa na kwa kushirikiana naye kiroho wanao uhakika wa kuishi naye katika uzima wa milele. Hivyo waishi kana kwamba wamekwisha kufika mbinguni, kwa macho ya kiroho wamwona Kristo kwa sababu wamekataa kuziangalia shida zao kiasi cha kulemewa nazo (Flp.4:4). Petro aliyewaandikia alikuwa amemwona Yesu kwa macho ya kimwili, tofauti na wao, hata hivyo alikumbuka maneno ya Bwana Yesu „wa heri wale wasioona, wakasadiki" (Yn.20:29; Ebr.11:6; Mt.5:12).

Kristo aliyasababisha na kuyatokeza mambo makuu katika maisha ya wale waliojikabidhi Kwake: tumaini k.3; imani k.7,9; upendo na furaha k.8 (1 The.1:3; 5:8).

k.10-12 Petro aliendelea kwa kusema juu ya wokovu na jinsi ambavyo manabii wa zamani walizitafuta na kuzichunguza habari zake. Walitabiri mambo mawili ambayo watu hawakutazamia. Walitabiri kwamba WaMataifa watafunuliwa na kushirikishwa neema ya Kristo. Walishuhudia kwamba Masihi atakayekuja atateswa na baada ya mateso atatukuzwa kwa kufufuliwa kutoka kwa wafu na kupandishwa juu na kupewa Jina lipitalo kila jina.

Manabii walitafiti ni wakati gani wa Kristo kutokea na namna ya Kutokea Kwake. Walipata kufahamu kwamba wao wenyewe hawatayaona mambo hayo. Unabii wao uliwahusu watu wa baadaye ambao wataufaidi ukombozi wa Kristo, yaani wale walioandikiwa katika Nyaraka za Petro na Paulo. Hao walihubiriwa Injili na Mitume na wenzao ambao kwa uwezo wa Roho walimtangaza Kristo.

„neema itakayowafikia ninyi" Hasa neema hiyo iliwahusu WaMataifa kuingizwa katika mpango wa Mungu wa kuwajalia wokovu (Rum.9:25-26; 10:11,13,20; 15:9-12, 21).

Zamani zile WaMataifa waliwazwa kuwa nje ya fadhili za Mungu. Ilitokea kama jambo la kuwashtusha Mitume walipopata kuyafahamu mapenzi ya Mungu juu ya WaMataifa. Kweli, katika huduma ya Bwana Yesu alikuwa ameyaelekeza mawazo yao kwa habari hiyo (Mk.13:10; Mt.28:19) ndipo hatua kwa hatua walithibitishwa neno hilo kwa njia ya matukio mbalimbali. Hasa hatua moja kubwa ilifanyika Petro alipotumwa kwa Kornelio (Mdo.10) pia katika mafanikio ya Injili kupokelewa na WaMataifa katika mji mkuu wa Antiokia wa Shamu (Mdo.11). Hatua nyingine ya maana ilitokea wakati wa Kanisa kukata shauri la kuwapokea waumini wa KiMataifa kwa ubatizo bila kuwatahiri (Mdo.15). Tena, baraka za Mungu zilionekana sana katika huduma ya Mtume Paulo kati ya WaMataifa. Wengi walimwamini Kristo na kuuonyesha ukweli wa imani yao katika mabadiliko makubwa kimaisha, wakitoka katika giza la imani zao za jadi na kuingia katika nuru ya Kristo. Hivyo ilikuwa kweli kusema kwamba „neema imewafikia".

Kwa hiyo, waumini wa KiMataifa watiwe moyo kwa ajili ya neema ya Mungu iliyowashirikisha mambo ambayo hata manabii hawakujaliwa kuyaonja ila waliyaona kwa mbali. Petro aliongeza kwa kusema kuwa hata malaika wanatamani kujua yale Mungu anayofanya (Rum.8:19).

Twaona ilikuwa Roho Mtakatifu aliyewaongoza manabii kuyaandika matokeo ya baadaye kabla hayajatokea, mambo makuu ambayo yaliubadili mwenendo wa historia. Hawakufanya kwa ujuzi wao bali kwa uwezo wa Roho (Yn.11:49- 52; 2 Pet.1:19-21).

Kwa uongozi wa Roho waliyatabiri mambo mawili yaliyo mageni katika mawazo ya Kiyahudi. Kwanza, Masihi atakayekuja atateswa, jambo ambalo hawakuliwaza hata kidogo. Pili, WaMataifa wataokolewa na kupokelewa sawa na wao. Iwapo wazo hilo lilikuwapo, ni wazo ambalo hawakulipenda wala hawakulikaribisha. Kumbe mambo hayo mawili yalisemwa katika Maandiko yao waliyoyasoma kila siku. Paulo aliandika kwamba Agano la Kale yaliandikwa kwa shabaha ya kuwafundisha Wakristo (Rum.15:4; 1 Kor.10;11; 2 Tim.3:15) Roho ameitwa Roho wa Kristo (Yn.15:26; 16:14).

1: 13-25 Mwito wa kuishi maisha ya tofauti

Kwanza ni mwito wa kuishi maisha matakatifu. Baada ya kuuonyesha uzuri wa wokovu na baraka zake za ajabu, na kuwafikirisha kwamba kumwamini Kristo ni jambo la thamani sana lipitalo kabisa shida na majaribu yote watakayoyapata, ndipo Petro aliendelea kwa kusema juu ya wajibu wa kuishi maisha yastahiliyo mwito wao.

k.13 Alianza na maneno „kwa hiyo" maneno yanayoonyesha uhusiano na yaliyotangulia. Wokovu ni kipawa cha kupokelewa tu kwa kumtegemea Mungu na neema yake. Baada ya kuupokea wokovu kama kipawa wameitwa kuishi maisha mapya katika Kristo, kwa neema yake, na kwa kuukaza mwendo wazidi kufanya yampendezayo. (Rum.12:2; Efe.4:17,18,23).

Petro alisema kwamba ni wajibu wao kuikaza nia zao, yaani wayatawale mawazo yao ili wapate kuamua na kufanya iwapasayo. „kuwa na kiasi" maana yake wasiishi kwa mradi tu, wala kwa bahati nasibu, wala kwa kuchukuliwa tu, bali wauangalie sana mwenendo wao, wawe macho, pia wawe na bidii, kusudi imani yao itekelezwe katika maisha ya kila siku. Mtu mwenye kujazwa Roho ni mtu wa „kiasi" si mtu wa kuchukuliwa huko na huko (Gal.5:22-23; 2 Tim.1:7).

Wakati wote Kristo huwajalia wafuasi wake neema. Wanao uhakika wa baraka zake kwa sasa na hata kwa baadaye. Kwa kuzionja sasa wanajua watazionja zaidi sana katika uzima wa milele.

k.14-15 Halafu Petro alitaja jambo la utii ambalo aliutaja mwanzoni mwa Waraka (1.2). Wawe wazoefu katika kumtii Baba aliyewazaa, ili wawe „watoto wa utii" kwa njia mbili. Kwanza kwa kutokuishi kama hapo nyuma, wasitawaliwe na tamaa mbaya za ujinga jinsi walivyoishi na kuongozwa nazo, tamaa zilizokosa msingi wa ujuzi wa kweli wa Mungu. Pili, wauonyesha utii wao kwa Baba kwa kuishi maisha matakatifu ambayo msingi wake ni katika tabia za Mungu Mwenyewe. Kwa hiyo, mfano wao ni Mungu (Efe.5:1; Mt.5:48; Kol. 3:10). Ni utakatifu unaogusa na kukolea maisha yao yote, katika kila eneo la maisha waishi kulingana na Alivyo Mungu.

Walipookolewa waliletwa kwenye uhusiano mwema na Mungu aliye Mtakatifu, kwa hiyo uhusiano wao mwema utaendelezwa kadiri watakavyofanya mapenzi yake. Mungu alipowaokoa Waisraeli na kuwatoa katika nchi ya Misri na kuwaleta katika nchi ya ahadi alifanya Agano nao na kuwaleta katika uhusiano mwema naye na mwito wake ulikuwa wawe watakatifu kama Yeye. Vivyo hivyo Wakristo wamepewa wito uohuo na Mungu yuleyule. Kwa njia ya damu ya Kristo iliyomwagika Msalabani Mungu amefanya Agano Jipya nao. Ni wito uliojengwa katika Maandiko „kwa maana imeandikwa" (k.16). Mungu aliyewaokoa Waisraeli watoke utumwa wa Misri ni yuleyule aliyewaokoa wao watoke utumwa wa dhambi.

k.17 Wakristo humwita Mungu „Baba" na kumwomba kama „Baba" kwa sababu Yesu aliwafundisha wanafunzi wake kufanya hivyo. Lakini ajabu ni kwamba huyo wanayemwita „Baba" pia ni Mhukumu wa kila mwanadamu, hakimu asiye na upendeleo. Atampima kila mtu kufuatana na kazi yake, kwa kuyaangalia aliyoyafanya, si aliyoyasema tu. Waisraeli walifundishwa kuwacha wazazi wao kwanza, hata kabla ya mahakimu yao (Law.19:2-3). Kwa hiyo, wamche Mungu kwa sababu ni „Baba". Wameingizwa katika familia ya Mungu Mtakatifu, na kwa sababu hiyo, wapaswa wafanane na Baba yao. Waishi hapa duniani kama watu wasio na makao ya kudumu hapa; bali waishi kama watu wanaotazamia kuishi mahali pengine baadaye. Wahesabu kwamba wapo hapa kwa muda tu, na waishi hivyo. Mtu anayehama anaishughulikia nyumba anayoihamia si ile anayohama, bidii zake ni kwa nyumba anayoihamia. Vema Mkristo awaze kuhama kwake duniani na kuhamia kwake mbinguni.

k.18-19 Alitaka waumini wautambue ukubwa wa gharama wa wokovu wao. Wamekombolewa na kuwekwa huru mbali na maisha yasiyofaa, maisha ya bure waliyoyarithi kwa baba zao. Gharama ilikuwa damu ya Kristo, damu ya thamani sana. Kristo alitoa maisha yake mpaka kufa na katika kufa ili awatoe katika utumwa wa dhambi na mapokeo na kawaida za imani zao za jadi. Petro aliandika kwa kulinganisha na jinsi Waisraeli walivyotolewa utumwani mwa Misri. Wanakondoo wengi walichinjwa na damu yake iliwekwa kwenye vizingiti vya milango. Sharti wanakondoo wasiwe na mawaa wala madoa (Kut.12:5; Law.22:19,20; Kum.15:21) Vivyo hivyo, Petro alimwita Kristo „Mwana Kondoo asiye na ila, wala mawaa" maana yake Kristo alikuwa na maisha makamilifu, Kristo hakuwa na dhambi wala hakufanya dhambi, hivyo alistahili kuwakomboa wenye dhambi (Mk.10:45). Hali akitaka kuikuza thamani ya gharama iliyotolewa na Kristo, Petro aliipambanisha na „vitu viharibikavyo kama fedha na dhahabu". Wakifahamu hayo na kuithamini gharama iliyotolewa na Kristo kwa wokovu wao hakika watautambua na kuutimiza wajibu wao wa kuishi maisha matakatifu.

k.20 Ukombozi wa Kristo ulikusudiwa na kupangwa na Mungu hata kabla hajauumba ulimwengu. Alipanga kumtuma Kristo hata kabla ya wanadamu kuumbwa na kuanguka. Hivyo anguko la wanadamu na kuingia kwa dhambi havikumshtusha Mungu. Alijua kwamba uwezekano upo wa matukio hayo maana alikuwa amewapa wanadamu hiari ya mapenzi. Hivyo, aliwahi na kuuandaa uponyaji wake.

Pamoja na hayo alifahamu atamtuma Mwana wake mpendwa afanye ukombozi kama ukitakiwa. Yeye ni „Kristo, Mtumishi ateswaye" ambaye Isaya alitoa habari zake (Isa.53). Huyo atajazwa na kuwezeshwa na Roho kwa kazi hiyo (Efe.1:4-10).

Mpango uliopangwa katika umilele, ulitekelezwa hatua kwa hatua mpaka ulipowadia „utimilifu wa wakati" (Gal.4:4) ndipo Kristo akaja (Ebr.1:1; 9:26; 1

Yoh.3:5). Petro alisema kwamba hayo yalikuwa „kwa ajili yenu" (k.20b) yaani kwa wale waliomwamini Mungu na kumwekea Kristo tumaini lao (k.21).

Kwa njia mbili Mungu alitenda mambo makubwa ya kuwasaidia watu kumwamini Kristo na kujitoa Kwake (si kumwamini kwa kichwa tu). Kwanza, Mungu alimtuma Kristo, na Kristo aliwakomboa kwa gharama kubwa ili awalete kwa Mungu (3:18). Pili, Mungu Mwenyewe aliwathibitishia kwamba amemkubali Kristo na kazi yake kwa kumfufua kutoka kwa wafu na kumtukuza. Kwa hiyo wawe na ujasiri wa kumjia Mungu hali wakijua hakika kwamba atawapokea. Pamoja na hayo amewapa tumaini la kuushiriki utukufu uleule ambao kwa sasa Kristo anaufurahia (Rum.5:2; 8:16-25). Wokovu ni tendo la Mungu peke yake. Ulianzia Kwake, ulitekelezwa naye, na Yeye ataendelea kufanya kazi mpaka ameifaulu kuleta watu Kwake, na kuwaokoa, na kuwatakasa na kuwakamilisha ili wawe watakatifu na wakamilifu kama Yeye.

k.22-23 „kuitii kweli" ni itikio lao kwa Injili. Kiutendaji wameitika kwa kuyatii mapenzi ya Mungu. Ni mara ya tatu neno la utii limetajwa katika sura hiyo (k.2,14). Walipoamini Injili walitakaswa dhambi zao na kuzaliwa mara ya pili kwa Roho Mtakatifu. Ni kwa Neno la Mungu (kweli) watu huzaliwa kwa mara ya pili na kutakaswa (Yn.15:3;17:17;6:63b; Lk.8:11).

Neno la Mungu, „mbegu" ni mfano wa Mungu asili yake, haliharibiki, wala haliwezi kuharibika, tena ni hai, linao uzima ndani yake, pia ladumu hata milele. Ni neno lifaalo wakati wote, halizeeki, wala halikosi kufaulu kazi yake. Linaendelea kusema na watu kizazi kwa kizazi (Isa.55:10-11).

Tokeo la kutakaswa na kuzaliwa kwa upya ni utu mpya wa upendo. Mungu ni upendo, kwa hiyo, ni mamoja kusema Mungu ametuzaa na Upendo ametuzaa. Upendo utazaa nini? Si utazaa upendo? Hivyo dalili ya kuzaliwa kwa mara ya pili ni upendano wa ndugu, yaani kuwapenda kwa kweli, kwa moyo, na kwa bidii (4:8).

Petro alitilia mkazo aliyoyasema kwa kuyatumia maneno ya nabii Isaya. Isaya alisema kwamba uumbaji wote unapita, ni wa muda tu, hata utukufu wa wanadamu ni sawa na maua, ni wa muda tu. Ila Neno la Mungu ni tofauti, hilo ladumu (Isa.40:6-8). Kwa hiyo wanadamu kwa kulipokea hilo Neno la Mungu, yaani Injili (k.25) waushirikishwa uzima na uhai wake na kuletwa kwenye uhusiano mwema ulio hai na Mungu aliye hai.

MASWALI

1: 1-12: Petro aliwatia moyo wa kudumu waaminifu kwa kusema nini juu ya:
(a) urithi?
(b) imani?
(c) furaha?

1: 13-25: Petro alisema nini juu ya mwito wao wa:
(a) kuishi matakatifu?
(b) kwa nini waishi maisha matakatifu?
(c) Petro alisema nini juu ya ukombozi wa Kristo?

2: 1-3 Hamu ya kukua kiroho
Kwa kuwa wamezaliwa upya na kuingizwa katika familia ya Mungu, budi wawe na hali tofauti. Katika maisha mapya hamna nafasi kwa maovu, unafiki, hila, husuda na masingizio. Petro alikaza habari hiyo akitumia neno „ote" mara tatu, „uovu wote" „hila yote" „masingizio yote". Aliwaambia waumini kuyawekea mbali mambo hayo, mfano wa kutupilia mbali nguo zilizochakaa. Ni juu yao kunia halafu kuchukua hatua za kuwekea mbali, kwa sababu neema ya Mungu hufanya kazi pamoja nao. Bila neema ya Mungu hawataweza, na bila wao wenyewe kuamua, neema ya Mungu itakuwa bure, maana Mungu hamsukumu mtu kufanya kinyume cha nia yake.

Tunapofikiri juu ya maovu yaliyotajwa, masingizio, unafiki, hila, ni wazi kwamba ni hali zinazowazuia watu wasishirikiane vizuri. Ni kinyume cha upendo wa ndugu uliotajwa (1:22).

Ili wakue kiroho lazima uhusiano wao wote na maisha ya nyuma uvunjwe, hasa hali zile zote zilizowadhuru wengine. Wamepewa njia thabiti ya kukua kiroho, ila wameonywa kwamba wasipoifuata hamna njia nyingine badala yake itakayofaulu.

2:2 Badala ya kuishi maisha mabovu na bila upendo wawe na hamu ya kukua kiroho. Wafanane na watoto wachanga wanaotamani maziwa ya mama zao, kiasi cha kulia ili wayapate. Dalili nzuri ya afya yao kuwa nzuri ni kutamani maziwa. Vivyo hivyo, Wakristo ni watu waliozaliwa upya, ni watoto wachanga kiimani, nao wahitaji kukua kiroho. Watakuaje? Petro ametaja „maziwa ya akili yasiyoghoshiwa". Maana yake nini? „maziwa" ni Neno la kweli, neno safi, neno lisilo na hila, neno lisilochanganywa na kitu kingine. Bila shaka Petro alikuwa akiwaza Neno la Injili, Neno la Mungu. Wasipoachana na maisha ya nyuma hawataisikia hamu ya chakula kipya cha kiroho. Walenge kuufikia utimilifu wa wokovu wao katika uzima wa milele. Kwa kujilisha Neno la Mungu na kwa kushirikiana na Kristo Aliye Hai, hakika watakua.

k.3 Kwa kuzaliwa kwa mara ya pili wameletwa kwenye ushirikiano mwema na Mwokozi na Bwana wao. Wameuonja uzuri wake, kwa hiyo, haikosi watakuwa na hamu ya kumjua zaidi na zaidi kama ilivyo kati ya mtu na rafiki yake. Wakiwa na hamu hiyo ni dhahiri kwamba wameuonja uzuri wa Bwana (Zab.34:8). Wasipokua watapoa na kurudi nyuma. Kama mtu fulani amesema „dhambi hufanya mtu asisome Neno la Mungu, na Neno la Mungu lamfanya mtu asifanye dhambi".

2: 4-10 Heshima ya kuwa katika Jamii ya Watu wa Mungu

Mtu hupata kuwa Mkristo kwa kumwendea Kristo. Petro ameutumia mfano wa jiwe na jengo. Amewashauri „wamwendee Yeye Jiwe lililo hai". Waende Kwake na wakae Kwake na waungane naye kwa kushirikiana naye. Kristo alikataliwa na wanadamu bali kwa Mungu alikuwa Mteule na mwenye heshima ya juu sana. Alipokaribia Kufa Kwake, Bwana Yesu alijisemea kuwa Jiwe la kukataliwa ambalo Mungu ataliweka kuwa Jiwe Kuu la Pembeni. Neno hilo lilitabiriwa katika Zaburi 118:22 (Mt.21:42; Mk.12:10; Lk.20:17). Petro mwenyewe aliyatumia maneno yayohayo alipomshuhudia Kristo wakati aliposhtakiwa mahakamani kwa sababu ya kumhubiri Kristo na Kufufuka Kwake (Mdo.4:11) Paulo pia alitumia mfano wa jengo (1 Kor.3:11; Efe.2:20).

Jiwe ni kitu kisicho hai, ila Yesu ameitwa Jiwe hai kutokana na Kufa na Kufufuka Kwake. Wayahudi waliamua kwamba Yesu hakufaa kuwa Masihi wao wala hakustahili hata kuishi kwa sababu ya madai yake ya kuwa Masihi, basi walimwua. Ila walivyoona na kuamua hayakupatana na jinsi Mungu alivyoona na kuamua juu yake. Ndiyo sababu Mungu aliupindua uamuzi wao kwa kumfufua kutoka kwa wafu na kumpandisha juu sana, naye amekuwa sababu ya Uzima kwa wote wamwaminio (Mdo.3:15; 1 Yoh.5:11-12). Yawapasa wawe thabiti katika imani yao, hali wakijua kwamba Mungu hutawala yote kama alivyotawala yote wakati Yesu alipokuwapo duniani. Wamo katika ulimwengu ulio kinyume chao kama ulivyokuwa kinyume cha Kristo, basi wamwendee, maana Yeye ni Jiwe Hai, Teule, ili wajaliwe neema na uzima wake.

k.5 Kutokana na uhusiano wao na Jiwe hai wao ni mawe hai nao wameingizwa katika familia ya Mungu, budi wafanane na Baba yao. Mawe yana kazi, Mungu amekusudia kuwajenga pamoja ili wawe nyumba ya kiroho, kwa hiyo, Mungu anao mpango unaowahusu. Kila muumini hujengwa katika imani yake pamoja na kujengwa pamoja na wenzake, jinsi ilivyo katika jengo, jiwe moja lawekwa pamoja na mawe mengine. Kila jiwe lina mahali pake na kazi yake katika jengo, na kila mmoja hupata maana yake na thamani yake kutokana na uhusiano wake na wengine na uhusiano wake na Kristo aliye Msingi na Jiwe Kuu la pembeni. Jiwe peke yake halina kazi, litafanya nini peke yake? ni jengo gani ambalo ni la jiwe moja tu? Mafundisho ya Petro hufanana na mafundisho ya Paulo juu ya mwili na viungo vyake (1 Kor.12).

Neno la Jiwe lililoteuliwa na Mungu na kukataliwa na wanadamu liliongoza mahubiri ya Petro katika siku za kwanza za Kanisa. Kila wakati alipambanisha waliyofanya Wayahudi na aliyofanya Mungu (Mdo.2:23-24, 32-33; 4:11-12; 5:30-31; 10:30-40). Yesu alimpa Petro jina la Kefa, maana yake „jiwe"(Yn.2:42).

Nyumba inayojengwa ni nyumba ya Roho, ni kwa ibada ya Mungu, ndani yake ni watu waitwao „ukuhani utakatifu". Wamo kwa ajili ya kumtolea Mungu

„dhabihu za Roho" si dhabihu za wanyama kama Wayahudi walivyotoa. Dhabihu za Roho ni dhabihu gani? Ni sifa na shukrani kwa Mungu na kutangaza fadhili za Bwana. Hizo zampendeza Mungu na kukubalika naye. Hasa kwa sababu zatolewa kwa njia ya Yesu Kristo na katika Jina lake.

Hekalu la pale Yerusalemu lilijengwa na mawe yasiyo hai, na waabudu walimjia Mungu kwa njia ya kumtolea dhabihu za wanyama na walihudumiwa na makuhani waliotoka kabila la Lawi. Ila sasa tofauti kubwa ni kwamba kila Mkristo na Wakristo kwa pamoja wamwendee Mungu na kumwabudu moja kwa moja bila kupitia kwa wanadamu na bila kuleta wanyama wa sadaka. Ila imewapasa kuwa wamemkubali Kristo kuwa dhabihu itoshayo kwa dhambi zao (1.3 „kunyunyziwa damu"). Katika Agano Jipya dhabihu mbalimbali zimetajwa; sifa (Ebr.13:15) maombi (Ufu.5:8) kujitoa (Rum.12:1; Flp.2:17) ukarimu (Rum.15:27; Ebr.13:15-16) utoaji (2 Kor.9:12; Flp.4:18). Kwa nini dhabihu hizo zina maana kubwa na kuthaminiwa na Mungu? Ni kwa sababu watu huzitoa kwa hiari, na kwa kupenda, na kwa nia safi, na kwa hali ya kuelewa wafanyalo, tofauti na wanyama ambao hawakuelewa kwamba wamekuwa dhabihu, waliletwa tu bila wao kufahamu na kukubali.

k.6 Kristo ameitwa Jiwe kuu la pembeni, na ni sawa na jinsi Paulo alivyomwita „Kichwa juu ya yote kwa ajili ya Kanisa" (Efe.1:22). Mahali pengine Kristo ameitwa „Mwamba" na „Msingi". Sayuni ni Yerusalemu wa juu na Petro ametumia maneno ya Isaya 8:16 kusudi awatie moyo wa kuendelea kumwamini Kristo, maana ahadi ilitolewa „hawatatahayarika".

k.7-8 Kristo ameitwa Jiwe la Msingi (1 Kor.3:11) na Mitume na Manabii wameitwa vivyo hivyo (Efe.2:20) ila ni Kristo peke yake ambaye ameitwa Jiwe kuu la Pembeni, teule, na mwenye heshima. Katika k.7 Petro aliandika kwamba Kristo amekuwa hivyo „kwa ajili ya ninyi mnaoamini". Ndipo aliendelea kwa kuwabagua na wasioamini. Kwa waumini Kristo ni wa thamani sana na sababu ya heshima yao, maana waishiriki heshima yake. Lakini kwa wale waliomkataa, Jiwe limekuwa jiwe la kujikwaa na mwamba wa kuangusha.

Wengine wakiendelea kumkataa Kristo kwa kutokuiamini Habari Njema ya wokovu, hawataushiriki uzima wake wala baraka za msamaha wa dhambi n.k. Wa kwanza kumkataa walikuwa Wayahudi waliotoa hukumu kwamba afe. Kwa sababu hiyo Mungu aliwakataa, na wote wafuatao nyayo zao hupatwa na hukumu iyohiyo.

k.8b Maneno „nao waliwekwa kusudi wapate hayo" hayana maana kwamba Mungu amewachagua na kuwafanya wamkatae Kristo bila kujali watakavyoamua wenyewe. La! ila maana hasa ni kwamba kwa vyovyote wote wamkataao Kristo watakataliwa na Mungu, na wote wanaompokea watapokelewa na Mungu. Katika kumkataa Kristo wameukataa msamaha wa

dhambi zao na kipawa cha uzima wa milele, kwa hiyo, mwisho wao ni mauti. Badala ya Kristo kuwa kwa ajili yao amekuwa kinyume chao.

k.9-10 Watu wa Mungu: Katika vifungu hivi viwili Petro ameeleza waumini kuwa „mzao mteule" „ukuhani wa kifalme" n.k. akiyatumia lugha ya Agano la Kale (Kut.19:5-6; Isa.43:20-21). Alisema waumini ni „mzao mteule". Taifa la Israeli liliteuliwa na Mungu na sasa Mungu ameliteua Kanisa, wote wanaomwamini Kristo kuingia urithi wao. Wamezaliwa upya na Roho na kuingizwa katika familia ya Mungu na kuhesabiwa „watoto na wateule". Hawatoki kwa kabila au taifa moja tu bali watoka kwa makabila na mataifa mbalimbali na kwa watu aina zote.

„ukuhani wa kifalme" neno ukuhani ambalo limetumika hapo ni lile lililotumika kwa makuhani wa Agano la Kale. Neno hilo halikutumika kwa wahudumu wa Agano Jipya. Ukuhani wa Agano Jipya ni wa Wakristo wote (k.5; Ufu.1:16). Makuhani wa Agano Jipya hutoa dhabihu za kiroho. Ni ukuhani wa kifalme kwa sababu wanamtumikia Mfalme ambaye pia ni Kuhani. Pengine ina maana kwamba Wakristo hushirikiana na Kristo katika utawala wake. Tumekwisha kuona mafundisho ya Agano Jipya kuhusu waumini kushirikishwa Kufa na Kufufuka Kwake Kristo (Ufu.1:6; 5.10). Katika Agano la Kale Ufalme haukuunganika na Ukuhani isipokuwa katika habari za Melkizedeki (Mwa.14:18). Ilitazamiwa kwamba Masihi atakuwa Mfalme na Kuhani. Mfalme Sauli aliyethubutu kufanya mambo yote mawili alihukumiwa (1 Sam.13:5-13). Wakristo wameshirikishwa hali zote mbili, wameitwa kutawala pamoja na kutumika.

„taifa takatifu" Wakristo wameitwa kuwa watakatifu kama Mungu alivyo Mtakatifu. Wametengwa ili wawe mali yake, watu wa kumtukuza kwa kuishi maisha bora na tofauti na wengine. „watu wa milki ya Mungu" maana yake Wakristo wamejitoa kufanya mapenzi ya Mungu, wamekubali awatawale.

Kwa maelezo hayo Petro ametoboa wazi jinsi Wakristo walivyo hasa, watu wenye wajibu wa kuzitangaza sifa za Yule aliyewaita watoke gizani na kuingia katika nuru yake ya ajabu. Maneno „giza" na „nuru" huonyesha mabadiliko makubwa yaliyotokea maishani mwao. Wamepata kuwa watu wazuri, wakimpatia sifa Yule aliyewasaidia kuwa wazuri kutokana na fadhili na huruma zake katika kuwakomboa na kuwahuisha kiroho (Mdo.26:18; Efe.5:8; Kol.1:13). Hapo nyuma hawakuwa watu wake, walikuwa nje, hawakuzijua rehema zake, ila sasa, sivyo ilivyo. Mungu amewahurumia na kuwaingiza katika familia yake, wamezaliwa upya na kujaliwa baraka zote za kiroho (Hos.2:23; Rum.9:23-26)
Katika sehemu hiyo yote kuanzia k.4-10 Petro ameonyesha kwamba ni Kanisa, Jamii ya Watu wa Mungu, ambayo ni Israeli ya Kweli, wenye mwito maalumu kutoka Kwake na wenye urithi uliowekwa na kutunzwa na Mungu kwa ajili yao. Hayo yote yamepatikana kwa Kristo na ndani yake.

Ni watu gani waliohurumiwa? Ni wale wasiokuwa na cheo wala heshima, wenye dhambi waliostahili hukumu tu, hao ndio wamehurumiwa na Mungu kwa sababu wamemjia Kristo aliye Jiwe hai. Mungu amewakubali na kuwahesabu ni wateule wake, ukuhani wa kifalme, taifa takatifu. Wameunganika pamoja na kuletwa kwenye uhusiano mwema na Mungu na kujengwa pamoja ili wawe hekalu la Roho kwa shabaha ya kumtolea Mungu dhabihu za sifa na shukrani na kuutangaza uzuri wake wa ajabu.

2: 11-25 Ushuhuda katika ulimwengu

k.11: Ndipo Petro aliwasihi, akianzia na neno la kuwavuta „wapenzi" neno la kuwakumbusha kwamba wamependwa na Mungu na wameitwa kuishi ndani ya ushirika wa ndugu wanaopendana. Aliwaita „wapitaji" na „wasafiri". Neno „wapitaji" ni ukumbusho kwamba wapo hapo duniani kwa muda tu, wanapita, hawatadumu hapa. „wasafiri" ni neno la kuonyesha kwamba hawawi wenyeji wenye haki za uraia, maana uraia wao ni huko mbinguni, wamo njiani tu, wakiuendea uzima wa milele ili waishi pamoja na Kristo milele (Ebr.11:8-14; Zab.39:12; Flp.3:20).

Ni rahisi kwa Wakristo kusahau neno hilo na Kanisa na watu wake kutulia na kuishi kama wengine waishivyo wakisikia hapa ndipo „nyumbani". Bwana Yesu aliutaja jambo hilo alipowaombea wanafunzi wake kabla ya kuuawa (Yn.17:11-16).

Petro aliwasihi waepuke na tamaa za mwili ili wasifanane na wenyeji ambao „nyumbani kwao" ni hapa duniani, watu wasio na nyumba nyingine wala matazamio ya kuishi katika uzima wa milele. Pamoja na faida ya usalama wa kiroho, Petro aliwaza sana ushuhuda wao, usiwe wa midomo tu, bali zaidi uwe ushuhuda wa maisha mema. Iwapo adui zao wenye chuki huwasingizia, watashindwa watakapoyaona matendo yao mazuri. Na matendo hayo mazuri yatakumbukwa na Mungu siku atakaporudi Kristo.

Halafu Petro aliendelea kuwafundisha Wakristo wajibu zao mbalimbali. Wajibu kwa wenye madaraka katika serikali na jumuiya (k.13-17) ndipo wajibu wao kazini (k.18-20) na wajibu wao kwa Kristo Mwenyewe (k.21-25) kisha wajibu wao katika ndoa na kwa familia (3:1-7). Viongozi wa zamani kama akina Petro na Paulo walijitahidi kuwasaidia Wakristo kwa kuwafundisha kinaganaga juu ya mambo ya kufanya na mambo ya kuepa, na tabia zilizofaa na tabia zisizofaa. Kwa njia hiyo Wakristo walifahamu jinsi ya kuishi katika mazingara ya siku zao.

2: 13-17 Wajibu wa Kikristo kwa wenye amri hasa katika serikali na jumuiya. Uhusiano kati ya Kanisa na serikali ulizidi kuwa mbaya na kuyasababisha matatizo mengi hata mahali pengine waumini waliteswa. Wakati ule serikali zote ziliongozwa na wapagani, na ibada na desturi za kipagani zilisimamishwa nao. Kila upande wa maisha uliguswa, maisha ya jamii, ya uchumi, na ya siasa.

Hivyo shida nyingi zilitokea kwa sababu Wakristo walimpa Kristo utiifu wao wa kwanza, si serikali. Mwanzoni shida ilitokea kwa sababu viongozi wa Kiyahudi walijaa wivu sana walipoona maendeleo ya Kanisa. Tena waliamsha fitini katika nchi za WaMataifa walipoona WaMataifa wamekuwa tayari kumwamini Kristo na Kanisa liliwapokea.

k.13 Petro alisisitiza neno la utii kwa ajili ya Bwana. Maana yake kwa hiari yao wachague kuwa watiifu wakitambua asili ya utawala mzuri na amri zao ni Mungu. Katika mpango wake kuhusu utawala wa kuangalia na kuhifadhi jamii za watu, Mungu ameona vema ziwepo tawala na uongozi mbalimbali.

k.14 Alionyesha shabaha ya utawala ni:

a. kuwalipiza kisasi watenda mabaya (Rum.13:3). Si kazi ya Mkristo aliyedhulumiwa kulipiza kisasa (k.19-23) ni kazi ya Mungu (Rum.12:19) pia ni kazi ya mahakimu waliowekwa kwa kazi hiyo (Rum.12:19; Yn.19:11). Hivyo viongozi na watawala wapaswa kuipenda haki na kuuchukia udhalimu sawa na Mungu (Ebr.1:8,9. Rum.13:33,34).
b. kazi ya pili ya viongozi wa serikali ni kuwasifu watenda mema, ili raia wema watiwe moyo ndipo watatoa kielelezo chema kwa raia wengine wakizitii amri za serikali kwa moyo.

Wakristo walipenda iwepo hali ya amani kwa ajili ya uenezi wa Injili, hivyo walijitahidi kuishi kwa amani bila kuchokoza mambo. Wao waliona neno kubwa ni Injili kuhubiriwa na waumini kuwa na nafasi ya kufuata kanuni za Imani yao. Waliwatii viongozi kwa ajili ya cheo chao zaidi ya uzuri wao.

k.15-16 Mungu alitaka hali yao njema izibe vinywa wale waliowapinga bila sababu za haki na bila kufahamu Ukristo ni nini na bila kutambua mambo ya kiroho, watu ambao hawakumwekea Mungu nafasi katika fikara zao (Zab.14:1; Lk.12:20).

Iwapo wana jukumu la utii, hata hivyo, budi waishi kama watu walio huru, maana Kristo aliwaweka huru mbali na dhambi zao ili wamtumikie Mungu. Ni katika kumtii Kristo, Bwana wao, watasikia uhuru wa kweli, uhuru wa kufanya mema, kwa sababu Injili imewapa uwezo wa kufanya yale mema waliyoshindwa kufanya hapo nyuma walipokuwa watumwa wa dhambi. Uhuru wa Kikristo si uhuru wa kufanya wapendayo, bali ni uhuru wa kufanya wapasayo. Uhuru wa kweli ni katika kuvitumia vipawa vyao katika utumishi wa Mungu (1 Kor.7:22).

k.17 Kisha Petro aliwashauri mambo manne kwa ufupi: kwanza „waheshimuni watu wote" kwa kuwa kila mtu ameumbwa na Mungu katika sura yake na kila mtu amekombolewa na Kristo. Hii ni kweli kuhusu kila mwanadamu, kwa hiyo kila mtu aheshimiwe, na Mkristo asijione wala asijifikirie kuwa bora kuliko mtu yeyote mwingine maana hali yake njema imetokana na neema ya Mungu tu.

Pili „wapendeni ndugu". Waumini walifundishwa tangu mwanzo kuishi kwa kupendana, na katika kupendana wawasaidiane kwa shida za kimwili (Mdo.2:41ku; 4:32ku).

Tatu „mcheni Mungu". Ndani ya shauri hilo liko wazo la ibada, wamwabudu Mungu kwa kweli, wawe na hofu ya kumjali kwa kutafuta kujua na kufanya yampendezayo.

Nne „mpeni heshima mfalme". Waumini wamekwisha kuambiwa waheshimuni watu wote. Kwa nini Mfalme ametajwa peke yake? Wote wapaswa waheshimiwe kwa sababu ni wanadamu, ila Mfalme aheshimiwe kwa sababu ya cheo chake cha kuwa Mfalme. Wakati wa Petro kuandika maneno hayo Kaisari Nero alikuwa Mkuu wa Dola naye alikuwa mkatili sana kwa upande wa Wakristo.

k.18-20 Wajibu wao kazini: Hapo tena twakuta neno la utii. Waumini waliambiwa wazi kwamba wapaswa wawatii mabwana wao hata ikiwa walikuwa wabaya wenye kuwadhulumu na kuwatesa. Waliitwa kuvumilia mambo yote katika hali ya kumkumbuka Mungu na kujua hakika kwamba Muungu huuhesabu wema wa namna hiyo kuwa wema hasa.

k.21-25 Wajibu wao kwa Kristo: Mara Petro alifuata wajibu wao kwa mabwana wao kazini kwa kusema juu ya wajibu wao kwa Kristo. Yawezekana alikumbushwa kielelezo cha Bwana Yesu alipoteswa isivyo haki na jinsi alivyoyapokea mateso yake. Wameitwa kumfuata Kristo kwa ukaribu na kukanyaga nyayo zake.

k.22 Katika kifungu hiki Petro amesisitiza hali ya Yesu jinsi ilivyokuwa tofauti sana na wanadamu wote. Yeye hakutenda dhambi, wala hakuwa na hila. Katika kusema na kutenda hakuwa na makosa, tena zaidi ya kutokuwa na hatia ya yale aliyoshtakiwa na wanadamu, hata machoni mwa Mungu hakuwa na dhambi. Kwa vyovyote hakustahili kuteswa wala kuuawa ila alikubali kusudi awe fidia ya dhambi za wote. Petro alikuwa shahidi wa maisha yake kwa kuwa alifuatana naye kwa miaka mitatu bila kuona kasoro wala kosa katika maisha yake.

k.23 Halafu Petro aliendelea kusema juu ya hali ya Yesu wakati alipoletwa mahakamani, wakati uliokuwa mgumu kabisa Kwake. Hakufanya kama washtaki wake walivyofanya. Walipomtusi hakuwarudishia matusi, wala hakuwatukana wala kuwapiga, bali alitulia kabisa, tayari kupokea lolote watakalomfanyia (Mt.26:63; 27:12-14). Badala yake alijikabidhi kwa Baba yake hali akijua hakika kwamba Baba atampatia haki, si katika kuachiliwa bali katika kumfufua kutoka kwa wafu na kumpokea Kwake juu. Hapo nyuma Petro alikuwa amekwisha kuwafundisha kwamba wakiishi kwa Kristo wataushiriki utukufu wake baadaye.

k.24 Kifungu hicho ni kizuri sana na cha maana sana hasa katika kuifahamu maana halisi ya Kufa Kwake Bwana Yesu. Petro alitoboa wazi ni nini hasa Yesu aliyofanya alipotundikwa Msalabani. Hakufa tu, bali wakati uleule wa kufa, alizibeba dhambi za wanadamu wote, pamoja na hatia yake, na adhabu yake. Kutokana na Yeye kuwa dhabihu ya dhambi, wao pamoja na sisi, sote hatutahukumiwa kwa dhambi zetu „kwa Kupigwa Kwake mliponywa". Shabaha ya hayo yote ni waumini kuishi kama ni „wafu kwa dhambi" yaani dhambi ipigwe marufuku katika maisha yao wakihesabu kuwa haina haki ya kuwepo. Halafu, kwa upande wa pili „wawe hai kwa haki" watafute kufanya yaliyo haki na wema. Siyo kusema dhambi itatoweka kabisa, la! itazuka mara kwa mara, kwa kuwa ni vigumu kuishi bila kufanya dhambi, ila isiwe mazoea yao, ikitokea, budi waitubu na kuiacha. Kwa hiyo wasiwe na mazoea ya kufanya dhambi, bali wawe na mazoea ya kufanya mema na haki (1 Yoh.1:5-2:22; 3:4-10; taz. Isa.53).

MASWALI

2: 1-3: Watakuaje kiroho?
4-10: Yesu ameitwa nini?
Waumini wameitwa nini?
Shabaha ya Mungu ni nini?
11-25: Petro alisemaje juu ya kukaa kwao hapa duniani?
Petro aliwafundisha nini juu ya wajibu wao kwa jumuiya na serikali?
Alisema nini juu ya wajibu wao kazini?
21-25: Alisema nini juu ya Kristo na kifo chake?

3: 1-7 Maisha ya Nyumbani

Kama ambavyo tumeona mara nyingi katika Nyaraka za Paulo, Petro pia alitoa mafundisho makuu kumhusu Mungu Baba na Kristo, halafu akayafuata na mafundisho juu ya maadili, jinsi iwapasavyo Wakristo kuishi kulingana na Imani yao. Mkazo ni juu ya wajibu zao si juu ya haki zao, maana Mitume na wenzao hawakutaka Wakristo wawe na Imani ya kichwa tu bali waitekeleze katika maisha ya kila siku. Kwa njia hiyo waumini walisaidiwa kuwa na ufahamu mzuri kimafundisho na kiutendaji.

Katika sehemu hiyo Petro alizungumzia uhusiano wa mume na mke katika ndoa, hakusema juu ya uhusiano kati ya wanaume na wanawake kwa jumla. Mara kwa mara ilitokea kwamba mmoja wa ndoa aliokolewa huko mwenzake hakuamini. Ilikuwaje kama mke aliamini na mumewe bado hajaamini? Mke atawezaje kumvuta amwamini Kristo? Asemeseme naye kila wakati? si atamchosha? Petro alishauri kwamba njia bora ni kumshuhudia kwa kielelezo cha maisha mema. „watiini waume zao" kwa sababu Imani yao mpya haiwaruhusu kuwakaidi waume zao. Waishi kwa upendo na utulivu, wakiwastahi mume zao, wasiwadharau kwa kutokuamini kwao.

k.3-5 Ndipo Petro alitaja habari za kujipamba kwa nje na kujipamba kwa ndani, moyoni. Wasipite kiasi katika hali ya umalidadi kuhusu kuvaa, kusuka nywele, kujitia bangali, kipuli, n.k. Kwa jinsi alivyoandika inaonekana Petro aliwaza gharama pamoja na muda wa kutumiwa katika kujipamba kama kusuka nywele n.k. Kwa wanawake wa Kikristo jambo bora ni kujipamba kwa ndani, maana yake, wawe na tabia za upole, utulivu, na usafi, maana tabia hizo zampendeza Mungu sana, maana Yeye huangalia ndani kuliko nje (1 Sam.16:7). Mwanamke anayejipamba sana anajiwaza na huenda anajipenda sana. Pia ni njia ya kujionyesha na kuuvuta usikivu wa watu hasa wanaume. Petro alisema kwamba wake walio na mzigo juu ya hali za ndani wamo katika mfuatano mzuri wa wale waliohesabiwa kuwa „mama" katika Israeli, akina Sara, Rebeka, Lea, na Raheli. Hao walimtumaini Mungu na kuishi maisha safi, hali wakiwatii waume zao, wakijitia chini yao katika uongozi wa nyumba zao. Petro alitaja habari za Sara kumwita Ibrahimu „bwana" wakati aliposikia habari ya kumzalia mwana.

Iwapo Petro alisema juu ya kujipamba tusifikiri kwamba ni kosa kuangalia nguo n.k. Si ushuhuda mzuri ikiwa watu hawajali jinsi waonekanavyo. Ni vema wawe safi katika miili na nguo. Si sifa kwa Wakristo kuishi kama wangali wanaishi katika karne iliyopita kwa mitindo ya nguo n.k. Mambo mawili ya maana ni kuwa na kiasi na kutokuleta vikwazo.

Katika k.2 alisema wawe na hofu, maana yake, wamche Mungu, na katika k.6 alisema „hamkutishwa kwa hofu yoyote" maana yake hawana haja ya kuwaogopa wanadamu, wala waume zao, hasa neno hilo lilihusu wale walioteswa na mume zao kwa sababu ya kumwamini Kristo.

Ni wazi Petro alifikiri kwamba kwa njia hiyo wake humtumikia Kristo, hasa wakiishi hivyo kwa furaha na kwa moyo wa kutaka, si kwa mradi au kulazimishwa tu. Petro alikuwa na mzigo juu ya ushuhuda wa waumini mbele za walio nje, hakutaka Injili wala Kanisa kuwazwa vibaya (2:12,15) maana alijua kwamba watu huwachunguza sana Wakristo na maisha yao („wakiutazama" k.2) Kwa jumla twaweza kusema kwamba mke awe na uvutiko lakini sio ule wa nje bali ule wa ndani wa tabia njema.

Petro aliandika vifungu sita juu ya wake, huenda kwa sababu aliona ni hao waliohitaji ushauri, maana katika nyumba mume alikuwa na mamlaka na uongozi, hivyo, mume aliyeokolewa aliweza kuibadili mipango ya nyumba bila shida, ila mke aliyeokolewa hakuwa na sauti wala uamuzi, kwa hiyo, ilimwia vigumu kubadili mambo bila kibali cha mumewe.

k.7 Hapo Petro aliwageukia waume wa Kikristo na kuwashauri jinsi ya kuishi na wake zao. „kaeni na wake zenu kwa akili". Neno la kuachana halikutajwa. „kwa akili" maana yake nini? akae na mke hali ya kumwelewa na kufahamu kwamba hana nguvu za kimwili sawa na yeye, pia kusikia kwake huwa tofauti,

avutwa na mambo tofauti. Kwa mfano, kwa kawaida, mwanamke hulia kwa upesi kuliko mwanaume. Tena wanaume wapenda michezo kuliko wanawake. Wanawake huvutwa na mambo ya nguo na nyumba. Jambo hilo laonekana katika watoto. Kwa mfano, ukimpa mvulana acheze na gari au mtoto wa kubandia, atachagua kipi? na msichana atachagua kipi? Kwa hiyo, ni vema mume aelewe tofauti hizo ili aishi na mkewe kwa akili, yaani kwa ufahamu. Pia, amheshimu kwa kuwa ni binadamu sawa na yeye, tena katika mambo ya kiroho, wote wawili ni warithi pamoja wa uzima wa milele. Wote huhitaji neema ileile ili waishi maisha yao ya Kikristo. Petro aliposema „chombo kisicho na nguvu" hakuwa na maana kwamba mke amepungua katika akili au uwezo, la! ila kwa upande wa nguvu za kimwili tu. Jambo kubwa kwa upande wao ni kuelewa kwamba maombi yao yatafanikiwa au hayatafanikiwa kufuatana na hali ya kuishi kwao kwa pamoja katika ndoa. Neno hilo ni ajabu na ni juu ya Wakristo waliooana kulijali.

Kwa jumla Petro aliwashauri mambo ambayo yalimsaidia kila mmoja kuishi kwa ajili ya mwenzake na kwa kufikiri manufaa ya mwenzake, isiwepo hali ya kujipenda. Kushirikiana kwao ni sehemu katika ushirikiano wao na Mungu, ila tofauti moja kubwa ni kwamba ushirikiano wao na Mungu utadumu hadi uzima wa milele, na wa kwao utakoma hapo duniani wakati wa kufa.

Petro alizikaza wajibu za mke kwa mumewe, si haki zake. Vilevile alizikaza wajibu za mume kwa mkewe, si haki zake. Kila moja awaze atoe nini kwa mwenzake kuliko apate nini.

3: 8-12 Warithi wa baraka na jinsi iwapasavyo kuishi

k.8 „neno la mwisho ni hili" Petro alielekea kufunga sehemu ambayo ilianza katika k.2:11 juu ya wajibu zao mbalimbali katika ndoa, na kazi, na maisha ya jamii n.k.

Alitaja mambo sita yaliyowahusu Wakristo wote wa hali zote na tabaka zote. Kwanza, wawe na nia moja. Neno hilo latokea mara nyingi katika Nyaraka (Rum.15:5ku; 1 Kor.1:10ku. 3:3). Paulo alilikaza sana alipowaandikia Wafilipi (Flp.2:1-11). Bila shaka Petro alikumbuka jinsi Yesu Mwenyewe alivyoomba kabla ya Kufa Kwake „wawe na umoja kama..."(Yn.17:11). Vema wawe na shabaha moja ya kumfuata Kristo na kielelezo chake na kuishi kwa tabia zake.

Ndivyo Wakristo walivyojitahidi kufanya katika siku za kwanza za Ukristo (Mdo.4:32). Ilikuwa busara wafanye hivi, maana walikuwa katika ulimwengu uliokuwa kinyume chao na kinyume cha Bwana wao na adui zao walikuwa wengi. Mipango yote ya maisha ya jamii ilikuwa tofauti na mwenendo wa Kikristo.

Neno lingine lilikuwa wahurumiane, wakifurahi pamoja na wale waliofurahi, na kulia pamoja na wale waliolia (Rum.12:15). Wasijipende na kuyaangalia mambo yao wenyewe tu.

Katika Agano Jipya neno la umoja ni muhimu sana, mafarakano na matengano yamehesabiwa kuwa kinyume kabisa cha Injili.

Tena wapendane kama ndugu, waishi kama familia moja, familia ya Mungu, walioletwa pamoja kwa njia ya Kristo. Katika Imani ya Kikristo tofauti za jinsia, kabila, tabaka, hali, na cheo, si kitu. Wote ni viungo katika mwili mmoja (1 Kor.12:26-27).

Ndipo Petro alisema wawe wasikitivu na wanyenyekevu, yaani wawe na moyo ulio mwepesi wa kuwajali wengine na hali na shida zao, tayari kujiunga nao kimawazo na kiutendaji kwa kutoa msaada n.k. Katika siku zetu si rahisi kuwa wasikitivu. Redio na televishoni zatuletea habari nyingi kwa njia ya kusikia na kwa picha za kuona. Mbele ya macho yetu twaona taabu kubwa za wanadamu wenzetu, maelfuelfu ya watu wanaoonewa vibaya, wakimbizi waliokimbizwa makwao, wengi kujeruhiwa na kuuawa katika vita vya nje na vya ndani ya nchi.

Pia twasikia habari za wengi kuishi kwa taabu za kukosa chakula na nguo na mahitaji ya lazima, watu wanaoishi kama takataka. Kuona kwingi na kusikia mengi kumetufanya kufa ganzi moyoni, ni vigumu kuamsha huruma na kuamua na kuchukua hatua za kufanya mambo ya kuwasaidia. Kwa hiyo ni juu yetu sisi Wakristo kuwa wasikitivu wa kweli, watu wa kuwawaza hao watu, kuwahurumia, kuwaombea, na kuchukua jukumu la kuwatafutia msaada, hata ikiwa kwa kuchokoza siasa ya kukabili mambo hayo. Twaitwa kusimama bega kwa bega na maskini, na walioonewa, na kuwa sauti kwa wasio na sauti.

Ndipo Petro alitaja unyenyekevu ambao umetajwa mara nyingi katika Agano Jipya. Maisha yote ya Yesu yalikuwa kielelezo chema cha unyenyekevu wa kweli (Mt.11:29; Gal.5:23; Efe.4:2; Flp.2:3). Katika ulimwengu wa zamani Wayunani na WaMataifa waliwaza unyenyekevu kuwa dalili ya udhaifu na unyonge, kwa hiyo waliwadharau wanyenyekevu. Ila ni vigumu kwa Mkristo kufikiri hivyo kwa sababu zifuatazo. Kwanza, ni tabia ya Bwana Yesu; pili ni hali itupasayo tunapowaza yote tuliyotendewa katika Kristo na Msalaba wake; tatu, ni hali itupasayo tunapokumbuka udhaifu wetu kwa kulingana na mwito wa Mungu kwetu kuwa watakatifu na wakamilifu. Nne, kiburi ni kinyume kabisa na Mungu anakichukia kabisa (Yak.4:6; 1 Pet.5:5; Mt.23:12). Budi tujidhili na tuwe na mzigo juu ya wengine.

k.9 Hapo inaonekana Petro aliwaza watu wa nje na jinsi iwapasavyo Wakristo kuwafanyia wakitendewa vibaya na kulaumiwa nao. Badala ya kuwarudishia sawa na walivyofanyiwa, vema wawabariki, maana yake wawafanyie mema, kwa sababu wao wenyewe wametendewa mema na Mungu, maana

wamezionja baraka zake. Mungu hakuwarudishia sawa na dhambi zao, bali aliwasamehe makosa yao na kuwapokea kwa mikono miwili na kuwakirimia neema na uzima, hata uzima wa milele. Jinsi walivyotendewa na Mungu, wawatendee watu vivyo hivyo. Kwa njia hiyo watazidi kuzirithi baraka za Mungu na kuzikanyaga nyayo za Bwana Yesu (2:23). Ndipo wasioamini watajaliwa kuuona uzuri wa Kristo. Wema moja wa kuwafanyia ni kuwaombea (Lk.6:28; Mt.5:44).

Petro alitilia mkazo mambo hayo kwa kutumia Zaburi 34:12-16. Mtunga Zaburi aliuliza swali kwa wale waliotaka kuishi maisha mazuri na marefu. Petro alilibadili swali kidogo, maana alijua kwamba Wakristo hawakosi kupatwa na shida na magumu, kwa hiyo aliuliza „atakaye kupenda maisha na kuona siku njema?" yaani aliwaza uzuri wa maisha si urefu wake, hali akielewa thamani ya maisha ya Kikristo ni mwisho wake mzuri katika uzima wa milele. Waishije? Budi wajihadhari na usemi mbaya na uongo wa kuwadanganya watu (2:1, 22).

Yakobo katika Waraka wake aliandika kwa kirefu juu ya nguvu ya ulimi kwa upande wa mema na kwa upande wa mabaya na hasa kwa upande wa mabaya. Iwapo ni kiungo kidogo, kina nguvu na uwezo mkubwa (Yak.3:1ku) Maneno huweza kuyaleta madhara makubwa yadumuyo muda mrefu.

Halafu Mtunga Zaburi alisema juu ya kuacha mabaya na kutenda mema. Yaani licha ya kutenda mabaya mtu asiyawaze mabaya hata kidogo. Badala yake ayawaze mema na kuyatenda.

Tena, waitafute amani na kuifuata sana (Rum.12:19; 2 Tim.2:22; Ebr.12:14; Mt.5:19). Amani ilikuwa kiini cha kazi ya Yesu, kwa kuwa alikuja duniani kwa kusudi la kuufanya upatanisho na kuleta amani. Ni juu ya kila Mkristo kuishi kwa amani, na inapokosekana afanye juu chini kuwapatanisha watu, na kwa vyovyote yeye mwenyewe asiwe sababu ya watu kukosa amani.

3:12 Mtunga Zaburi aliwahakikishia walio waaminifu kwa Mungu kwamba daima Bwana wao huwaangalia na kuwatunza, ndiyo maana ya maneno „macho ya Bwana huwaelekea wenye haki". Hayana maana kwamba Mungu anachunguza kuona wanafanya nini. Tena Mungu ni mwepesi wa kuyasikia maombi yao „masikio yake husikiliza maombi yao" ni lugha ya kipicha inayoonyesha uhusiano wa ukaribu kati ya Mungu na watu wake.

Watenda mabaya ni tofauti sana na „wenye haki" wanazozifuata njia za Mungu wao. Mungu ni kinyume cha watenda mabaya „uso wa Bwana ni juu ya watenda mabaya". Maneno hayo huonyesha uhusiano mbaya kati yao na Mungu maana wao wamempa Mungu kisogo na Mungu amewapa wao kisogo kwa kutokuwashirikisha neema yake na kwa kutokusikiliza maombi yao (Zab.1:1-6). Petro hakuweka sehemu ya mwisho wa Zab.34:16b „aliondoe

kumbukumbu lao duniani". Pengine kwa kuwa aliamini kwamba maadamu wangali hai nafasi ipo ya toba (Lk.23:43).

3: 13-17 <u>Kuvumilia mateso</u>

Wakristo waitwa kufanya mema hata wakiteswa kwa ajili yake. Katika k.13-14 Petro aliuliza swali ambalo jibu lake lilitazamiwa kuwa „hamna mtu" maana haikutazamiwa kwamba mwenye juhudi katika mema atadhuriwa. Hata hivyo, Petro alitambua ya kuwa sivyo ilivyo. Inawezekana Wakristo wateswe iwapo wanaishi maisha mema na ya haki.

Petro aliwakumbusha ni baraka „wanayo heri" wakiteswa bila sababu (Mt.5:3-11 hasa k.10-11). Alikuwa amedokezea hayo katika 1.6. Mungu yu upande wao, naye atawahifadhi wala hakuna awezaye kuwazuia wasiingie urithi wao uliotunzwa na Mungu (1.4; 2:20-21). Madhara ni ya muda tu, wala hayawezi kuugusa uhusiano wao na Mungu. Kwa hiyo, wawe tayari kwa mema yao kuwazwa vibaya na itikio la watu kuwa tofauti na jinsi ilivyo haki, maana katika 2:14 Petro aliandika kwamba wakubwa wamewajibika kuwalipa kisasi watenda mabaya na kuwasifu watenda mema. Mara nyingi watu hawapendi watenda mema kwa sababu maisha yao mazuri ni hukumu juu ya maisha yao mabovu, tena wameachiwa hawana udhuru. Hata ikiwa wema wa mtu ni dhahiri na wote huuona hata hivyo wengine watatafuta sababu zisizo kweli za kumshtaki Mkristo.

Iliyopo, kwa upande wao, ni wajue kwa hakika kwamba Mungu atawajalia neema ya kutosha itakayowasaidia kuyakabili magumu ya aina yoyote, na kwa kupitia katika magumu watakua katika kumjua Bwana (2 Pet.3:18) hivyo wasifadhaike.

k.15-17 Jambo litakalowasaidia ni uhusiano wao kibinafsi na Bwana Yesu. Wamtukuze Kristo mioyoni mwao, maana yake wamruhusu Bwana Yesu awemo ndani yao ili awalinde na amani yake (Flp.4:7). Mkristo aliye peke yake, ambaye hana nafasi ya kushirikiana na wenzake na kuabudu pamoja na wengine, hata hivyo, anao ushirikiano wa ndani na Yesu Mwenyewe, kwa hiyo, afanye juu chini kuutunza huo uhusiano kwa kuyatii mapenzi yake. Akisongwa na majaribu ya kumwasi Bwana, kwa mfano, wakuu wakimleta kwenye sanamu ya Kaisari na kumshurutisha atoe dhabihu na kusema „Kaisari ni Bwana" awe mwaminifu kwa Kristo.

Wakiitwa kuyajibu mashtaka au wakiulizwa juu ya Imani yao wasinyamaze iwapo watajaribiwa kukaa kimya. Wakati huo wajibu kwa kuwaelezea tumaini walilo nalo katika Kristo. Bila shaka wengine watashangaa watakapouona uthabiti wao nao watataka kujua hiyo imani waliyo nayo ni ya namna gami. Ila wasifanye kwa kiburi, wala majivuno, wala kwa hali yoyote ya uchokozi, bali wawe wapole. Wasiwahofu wanadamu bali wamche Mungu.

k.15 Maisha yao na maneno yao yalingane ili wasikie nguvu katika dhamiri zao ndipo itakuwa vigumu kwa masingizio na mashtaka ya watu kufaulu, kisha wapinzani wao watatahayarika.

k.17 Kama adui zao badala ya kutahayarika wakizidi kuwapinga na kuwatesa, basi wajue kwa hakika kwamba ni vema kuteswa kwa ajili ya kutenda mema kuliko kuteswa kwa kutenda mabaya. Watesi wao watakuwa wamepewa ushuhuda mkali juu ya uwezo wa Injili kumbadili mtu na kumwezesha aishi maisha mema potelea mbali apingwe kiasi gani. Yawezekana ndiyo sababu Mungu huruhusu watu wake kuteswa isivyo halali. Katika kutumia neno „afadhali" (k.17) Petro alikuwa akiwaza mambo ya baadaye si mambo ya sasa tu. Mbeleni Mungu atafanya hukumu ya mwisho, na katika siku ile utu wema utakuwa na ushindi juu ya utu uovu. Wakristo wasisahau neno hilo wanapopita katika dhiki.

MASWALI

3: 1-7: Petro aliserna nini kuhusu wajibu zao mume na mke?
13-17: Alisemaje juu ya kuyavumilia mateso?

3:18-22 Kielelezo cha Kristo

Petro alipowaza juu ya watu kupata mateso bila sababu na bila kuyastahili alimkumbuka Bwana Yesu. Zaidi ya wanadamu wote Yesu hakustahili kuteswa hata kidogo. Alipokuwa duniani alitumia nafasi yake yote katika kutenda mema. Alitembea huko na huko akiwaponya watu, akiwatoa pepo, akiwafundisha, akiwatumainisha juu ya maisha, akiwashughulikia maskini, waliolemewa, wale wasiopendwa na watu, na aliwakaribisha watu waliowekwa kando ya maisha ya jamii (Mdo.2:22; 10:38). Wapinzani wake walishindwa kuonyesha kosa ndani yake (Yn.8:46). Kisha akauawa kwa mashtaka ya uongo (Mdo.2:23).

Hoja ya Petro ilikuwa kwamba wafuasi wa Kristo wapaswa wakifuate kielelezo chake chema. Hapo nyuma aliwashauri wake kuwastahi waume zao wasioamini, wawe watulivu na wapole, wasiwachokoze na kuwasemasema, ili maisha yao mazuri yaseme nao. Na katika sura hiyo amewashauri wale walioteswa vibaya wasiwarudishie watesi wao mabaya bali wawe wapole na wenye adabu kwao (3:15). Tena katika 2:21-23 alisema juu ya Kristo kutuachia kielelezo chema alipoletwa mahakamani na kuhukumiwa isiyo halali.

Kwa hiyo Petro aliwaza Kufa Kwake Kristo ni mfano bora, lakini pamoja na kuwa mfano bora aliendelea kuonyesha kwamba Kifo chake hasa kilikuwa fidia ya dhambi. Mungu alimruhusu Kristo afe kwa ajili ya dhambi, mwenye haki kwa wasio haki, ili Kristo awaokoe wenye dhambi. Kwa Kifo chake Kristo alitengeneza njia ya watu kumrudia Mungu „ili atulete kwa Mungu". Kristo aliteswa mara moja kwa ajili ya dhambi, Yeye ambaye hakuwa na dhambi (1:19; 2:22; 1 Yoh.3:5; 1 Kor.15:3; Gal.1:4; Ebr.10:12). Alitoa dhabihu ya nafsi

yake mara moja tu, nayo ilitosha kuzifidia dhambi zote za watu wote wa wakati wote (Ebr.7:27; 9:12,26,28; 10:10).

Sehemu inayofuata ni vigumu kujua maana yake kwa uhakika. Katika k.18b Petro aliandika „mwili wake akauawa bali roho yake akahuishwa; ambayo kwa hiyo aliwaendea roho waliokaa kifungoni, akawahubiri..." Siku ile aliposulibiwa ni kweli mwili wake uliuawa, hata hivyo, mara baada ya Kufa na kabla ya Kufufuka aliwekwa uhuru na mipaka ya mwili na alifanya kazi katika ulimwengu wa roho kama mwanadamu aliyeshinda dhambi na mauti. Katika hali hiyo aliwaendea roho waliokaa kifungoni, watu wasiotii hapo zamani. Hao walikuwa akina nani? Katika Mwanzo 6.1-4 tuna habari za „wana wa Mungu" (Je! hao ni malaika?) waliofanya dhambi na wanadamu. Katika 2 Petro 2:4-5 na Yuda 6 tuna habari za malaika waliofungwa gizani kwa sababu ya uasi wao. Au pengine ni watu wa kizazi cha Nuhu ambao hawakuujali wito wa Nuhu wa kutubu, kisha gharika ikawameza; hao walidhaniwa kuwa wafanya dhambi wabaya sana. Kweli ni vigumu kusema kwa uhakika.

Je! aliwahubiri wokovu? au aliwatangazia ushindi wake juu ya maovu na mauti? kama aliwatangazia ushindi wake walipata kujua kwamba hukumu yao imetiwa muhuri, kwa hiyo ilikuwa habari mbaya kwao. Jambo la Yesu kwenda kuzimuni lilidokezwa katika Mdo.2:27,31; Rum.10:6-8; Efe.4:8-10; Yn.5:25-29; twajua wafu walifufuka siku ile alipofufuka Yesu (Mt:27:52). Kwa maneno hayo inaonekana Yesu alikuwa akifanya kazi kati ya Siku ya Kufa Kwake hadi Siku ya Kufufuka Kwake. Kama ilikuwa kuhubiri Injili na kuwapa watu nafasi ya kuokolewa, au ilikuwa kuwatangazia ushindi wake, ni vigumu kujua kwa hakika. Ni fumbo kwetu, ila twajifunze tusimwekee Yesu mipaka katika kazi zake.

Katika k.20 Petro alitaja uvumilivu wa Mungu, jambo la maana sana katika wokovu wa wanadamu. Ni unyenyekevu wa ajabu kwa Mungu kuwangojea wanadamu, hali Yeye, kwa upande wake, amefanya yote yaliyotakiwa, tena kwa gharama kubwa sana ipitayo kuwaza kwetu.

Yawezekana Kanisa lilitumia sana habari za Nuhu katika kuwaandaa watu kwa ubatizo. Habari za Gharika ziliwahusu watu wanane kuokolewa huku watu wengi walipotea chini ya hukumu ya Mungu. Hao waliookolewa walisalimika kwa njia ya ajabu. Safina ni mfano wa Kristo, safina ilipigwa na maji pamoja na kubebwa na maji huku wanane walisitiri ndani wasipigwe na hukumu hiyo ya maji.

k.21 Petro aliona ubatizo ni mfano mzuri wa watu kuokolewa kwa maji. Ila Petro alitoboa wazi kwamba watu waokolewa kwa Kufa na Kufufuka Kwake Kristo. Katika Warumi sura ya sita Paulo alieleza juu ya kufa na kufufuka pamoja na Kristo. Nguvu ya ubatizo si katika maji yanayotumiwa bali katika nguvu ya Yesu Aliyefufuka. Maji ni ishara yake tu. Katika ubatizo „jibu la dhamiri safi lilitakiwa" yaani watu kukiri utiifu wao kwa Kristo kwa kujitoa Kwake.

k.22 Petro akaifunga sehemu hiyo kwa kurudia neno la ushindi wa Kristo. Zaidi ya Kufufuka, Yesu akapaa na kutawazwa juu ya enzi, malaika, na nguvu zote. Neno hilo liliwatia moyo wote walioteswa au waliotazamia kuteswa karibuni hivi.

4: 1-6 Kujitoa kabisa kwa mapenzi ya Mungu

Petro aliendelea kwa kuonyesha matokeo kiutendaji yawapasayo wafuasi wa Kristo katika kumfuata Yule aliyejitoa kiasi cha kukubali kuuawa ili ayatimize mapenzi ya Mungu.

Alianza kwa kusema juu ya Kristo na mateso yake. Kifo chake kilikuwa zaidi ya kielelezo, hasa kilihusu dhambi (2:24; 3:18). Alipofufuka, Kristo alikwisha kabisa kuhusika na dhambi, kwa kuwa alikuwa ameitoa dhabihu iliyotosha kwa dhambi za ulimwengu wote, hivyo „ameachana na dhambi". Vivyo hivyo, wafuasi wake pia waamue kuachana kabisa na dhambi, isipate nafasi tena katika maisha yao, kwa hiyo wajivike „silaha ya nia ileile" ya Kristo. Hapo Petro amefanana na Paulo katika mafundisho yake na bila shaka hayo mafundisho yalikuwa kiini cha matayarisho kwa wale waliotaka kubatizwa. Katika sura ya sita ya Waraka kwa Warumi Paulo alieleza kwa wazi neno hilo, taz. Rumi 6:1- 12 hasa k.10-12. Wakristo walijua kwa hakika kwamba iwapo Kifo cha Kristo kilikuwa kielelezo cha kufuatwa, zaidi kilikuwa dhabihu ya dhambi. Wao kwa njia ya kuamini na kubatizwa wameungana na Kristo na kushirikishwa baraka za Kufa na Kufufuka Kwake. Maana yake walihesabiwa kuwa katika Kristo alipokufa, kwa hiyo, wameifia dhambi, pia Alipofufuka wao nao walifufuliwa ili wamwishie Mungu.

Nguvu ya Kristo Aliyefufuka yatosha kuwawezesha waikatae dhambi, kwa sababu Kristo ameivunja nguvu ya dhambi na ahadi ipo „dhambi haitatawala ninyi" (Rum.6:14). Budi wajivike nia ya kuikataa dhambi hasa wakikumbuka vita aliyokuwa nayo Kristo aliposhindana na dhambi, hata kuteswa na kuuawa kwa ajili ya kuishinda (Ebr.12:3-4). Twaona umuhimu wa nia zetu katika maisha ya Kikristo (Rum.12:2; Efe.4:17,23).

4: 2-3 Walipaswa waubadili mwenendo wao na kuachana kabisa na maisha ya nyuma na kuishi maisha mapya ya kufanya mapenzi ya Mungu. Wasitawaliwe na tamaa za kibinadamu zilizowashika na kuwaongoza kujiunga na wengine katika kufanya mabaya. Petro alisema kwamba walikuwa wameupoteza muda wa kutosha katika mambo yasiyofaa na yasiyo na faida, basi wautumie muda uliowabakia kwa mambo yenye faida kwa maisha ya sasa hata ya baadaye. Waukomboe wakati (Efe.5:15-17).

Petro aliorodhesha dhambi mbalimbali ambazo hao walioandikiwa walikuwa wamezoea kufanya kabla ya kumpokea Kristo, Petro aliziita „mapenzi ya Mataifa". Iwapo wengi wao walikuwa WaMataifa, tusifikiri kwamba Wayahudi

hawakuwemo miongoni mwao. Petro alilitumia Agano la Kale mara kwa mara na ni vigumu kufikiri kwamba alifanya hivi ikiwa baadhi yao hawakuwa Wayahudi. Orodha ina dhambi za kila aina na inatupa picha ya maisha ya kawaida ya watu walioishi wakati ule katika sehemu zile. Kama Petro alivyosema katika k.4 watu walishangaa walipowaona wenzao waliacha kufuatana nao na kuishi tofauti nao. Bila shaka walijiuliza „imekuwaje?" „wamepata wapi uwezo huu?". Hata hivyo, badala ya kuwasifu na kuwapongeza, waliwatukana (2:12; 3:9; 4:4,14). Mara nyingi watu hawapendi kuona maisha mema ya mtu kwa sababu ni hukumu kwa maisha yao, tena inawanyima nafasi ya kutoa udhuru kwa maisha yao mabovu.

k.5 Hata hivyo wataitwa kutoa hesabu kwa mambo hayo. Kwanza kwa ajili ya maisha yao mabaya ya kutokumcha Mungu, na pili kwa itikio lao baya walipoyaona maisha mazuri ya wenzao.

Mungu atawahukumu wanadamu wote (Mdo.10:42; 2 Tim.4:1; Ebr.9:27). Kristo atakaporudi atawakuta wengine walio hai na wengine watakuwa wamefariki dunia. Haidhuru mtu yu hai au siyo wote watahukumiwa. Hukumu itakuwa „pasipo upendeleo" (4:17) itakuwa „kwa haki" (2:23) „yu tayari" maana yake haibaki nafasi ya ushawishi wa kuibadili (4:5) ni „mtimilifu" (4:6).

k.6 Ni vigumu kuelewa maana halisi ya kifungu hiki. Huenda chahusu Wakristo waliokufa na tofauti kwa upande wao haiwi katika kufa, maana watakufa sawa na wengine wote, ila baada ya kufa watakuwa hai na kuishi kiroho. Yawezekana watu waliuliza „iko tofauti gani kati ya Wakristo na sisi kwa kuwa sote tunakufa?". Tofauti kubwa ni katika Wakristo kuondolewa umo na uchungu wa mauti (1 Kor.15:55-56), mauti ni mlango wa kupitia ili waingie katika maisha mapya ya kushirikiana na Kristo kwa ukaribu sana. Hivyo rafiki na jamaa zao hawakuwa na haja ya kusikia hofu na wasiwasi juu yao (1 The.4:13-17; Yn.5:24).

4: 7-11 Wajibu mbalimbali

Katika k.5 Petro aliwakumbusha Wakristo juu ya hukumu ya Mungu, na katika sehemu hiyo aliendelea na neno hilo akiwashauri mambo kadha kuhusu maisha yao ya kila siku akisema „mwisho wa mambo yote umekaribia". Yaani hukumu ya Mungu haiwi mbali sana, kwa sababu inahusu jinsi waishivyo sasa, vilevile Kurudi kwa Kristo hakuwi mbali sana. Ila kwa kusema ni karibu siyo sawa na kusema Kristo atarudi kesho au mwaka ujao la! Hasa mkazo ni juu ya mambo yote kuwa na hali ya kupita, yakielekea kufikia matimizo yaliyowekwa na Mungu. Daima Mungu hufanya kazi kwa kufuata malengo yake. Mwisho ni kufika kwa „mambo yale" yatakayokuwa badala ya mambo ya sasa. Kwa Wakristo, maisha waliyo nayo katika Kristo yataendelea na kuzidi kuwa bora Kristo atakaporudi, na kwa sababu hiyo, Petro aliwashauri juu ya maisha yao ya sasa. Tangu Kuja kwa Kristo wamekuwa katika „siku za mwisho" (1:20;

Ebr.1:2; 9:26; Rum.13: 11) kwa sababu Kristo ameushinda ulimwengu (Mk.13:33).

Hivyo ni jambo muhimu sana Wakristo wakazane katika maisha yao. Wawe na akili, wawe macho, wajitawale, waishi hali wakiutafakaria sana mwenendo wao. Waamue mambo kwa kuyatanguliza mambo ya maana na ya faida kiroho, wasimezwe katika shughuli za dunia na kuchukuliwa tu na kawaida za ulimwengu huu. Tena, wakeshe katika maombi, wautunze sana ushirikiano wao na Mungu, ili wapate kuelewa mapenzi yake na kuufuata uongozi wake.

k.8 Ni neno la maana sana wawe na juhudi katika kupendana, si upendo wa juujuu wa kutegemea kusikia kwao, bali upendo unaowagharimia bidii na nguvu na mawazo. Kwa upendo wawe tayari kuwasamehe watu makosa yao tena na tena bila kufanya hesabu (Mit.10:12; Mt.6:14).

k.9 Wawe tayari kuwahudumia watu na kukaribisha watu nyumbani. Baadhi wa waumini walitengwa na familia na rafiki zao walipokata shauri la kumfuata Kristo na wengine walikosa nafasi ya kazi, kwa hiyo walihitaji msaada wa Wakristo wenzao. Katika siku zile Wakristo walikutana katika nyumba zao kwa ibada na mikutano (Rum.16:5; 1 Kor. 16:10,19; Kol.4:15). Wahudumu na wainjilisti waliokwenda huko na huko walihitaji mahali pa kukaa kwa sababu nyumba za wageni hazikuwa salaam, zilitumiwa na makahaba na wevi. Hivyo iliwapasa Wakristo wawe wakirimu wa kuwapokea watumishi waliosafiri huko na huko kwa ajili ya Injili (3 Yoh.5-8; 1 Tim.3:2). Petro aliongeza maneno „pasipo kunung'unika". Mahali pengine Wakristo walifikiwa na watu kila wakati, hata wakasikia kulemewa, hata hivyo, kwa sababu huduma ya ukaribishaji ilihitajika sana budi waendelee bila kuchoka. Kwa njia hiyo walilisaidia Kanisa sana katika uenezi wa Injili na utunzaji wa wahudumu.

k.10 Kila Mkristo amejaliwa kipawa kwa shabaha ya kumtumikia Mungu. Hakuna aliye na udhuru wa kutokufanya jambo fulani. Hakuna aliye dhaifu au aliyekosa uwezo wa kufanya kitu. Shabaha ni kwa kila Mkristo kuitumia karama yake kwa ajili ya wengine. Karama zimetolewa ili wajengane na kusaidiana (Lk.12:42). Wafute wazo la kufikiri ni wachache tu walioitwa kufanya kazi. Katika mwili kila kiungo kina kazi, vilevile katika shirika la Kikristo kila Mkristo anao wajibu wake. Karama zatofautiana, nyingine zahusu huduma ya kiroho kama kuhubiri Neno la Mungu na nyingine zahusu „huduma ya mezani" (Mdo.6:1ku). Wanaofanyia kazi za kimwili huhitaji nguvu za mwili na hekima katika kuifanya, tukikumbuka wanaowahudumia wagonjwa, wenye njaa, na wahitaji mbalimbali. Wengine huwa na kipawa cha kuwatembelea watu n.k. ziko aina nyingi za kuhudumiana. Aina zote zimetoka kwa Mungu, Yeye ameziwekea nafasi. Yeye Mungu hufanya kazi kwa njia ya watu kuvitumia vipawa vyao, na matokeo mema yasababishwa na Mungu kujiunga nao si kwa sababu ya uwezo wao wenyewe tu. „neema mbalimbali" maneno hayo huonyesha karamu zatolewa kwa neema ya Mungu, zimetolewa bure na

Mungu Mkarimu. Mungu humfanyia kila mtu kama yeye ni wa pekee, na kumgawia kila mtu kitu cha kumfaa yeye na kilicho tofauti na wenzake.
k.11 „Mhubiri aseme kama mausia ya Mungu" Maneno yake ni ya kibinadamu ambayo hayana uwezo wala hayatoshi, ila Roho afanya ajabu kwa kuyachukua hayo maneno yake na kuyavuvia ili yawe ujumbe hai wa Mungu. Hivyo yampasa mhubiri amtegemee Mungu kabisa. Kwa upande wa mhubiri yeye apaswa afanye maandalio mazuri, asiwe mvivu katika matayarisho ya mahubiri yake, ila mwishowe ajue ni Mungu atakayeyahuisha hayo mahubiri (1 The.2:13). Shabaha ya kutumia vipawa ni Mungu atukuzwe na usikivu wa watu uende kwa Mungu si kwa watu (1 Kor. 4:7).

4: 12-19 Kukubali mateso kwa furaha

Petro alianza sehemu hiyo na neno „wapenzi" kwa kuwa alitaka kuwatia moyo juu ya mateso ya „moto" yaliyowakabili. Katika 3:14 Petro aliandika kwa kukubali kwamba upo uwezekano wa wao kupatwa na mateso ila kwa jinsi alivyosema ilionekana hayajaanza bado. Ila hapo inaonekana mateso yamekwisha kutokea „ulio kati yenu, unaowapata..." Imekuwaje tofauti imetokea katika barua moja fupi? Pengine jambo fulani lilitokea ambalo limewahakikishia kwamba ile dhoruba ambayo mawingu yake meusi wameyaona kwa muda, sasa iko karibu sana kuwapata.

Neno la kwanza wasishtuke, wala wasilihesabu kuwa jambo geni, kwa sababu mateso ni jambo la kawaida kwa Kanisa na watu wake katika ulimwengu huo, kama Bwana Yesu alivyofundisha na kuyapata katika maisha yake (Mt.5:11ku. Mk.13:13; Yn.15:18-20;16:33; 1 Yoh.3:13ku. 1 The.3:3). Ingalihesabiwa kuwa ajabu kama Wakristo wasingaliteswa, maana hao huwa kinyume cha tabia za watu wa dunia ambao kwa jumla ni watu wa kujipenda. Wakristo wameitwa kuwapenda jirani kama nafsi zao hata kuwapenda adui zao. Kwa kawaida watu wa dunia hii hawapendi kuona watu wanamtanguliza Mungu katika maisha yao kwa sababu wanakumbushwa Kuwepo kwa Mungu na madai yake juu ya maisha yao, madai wanayojitahidi kuyasahau na kuyasukumia mbali.

Petro aliyataja mateso kuwa „moto ili kuwajaribu". Neno „moto" laleta maana ya mateso kuwa njia ya kuipima na kuisafisha imani yao ili ukweli wake udhihirike. Wasio Wakristo wa kweli hutoweka wakati wa shida na hatari.

Pia mateso ni njia ya kuyashiriki mateso ya Kristo. Katika mateso Kristo hushiriki pamoja na wale wateswao na wateswao hushiriki na Kristo. Twakumbuka habari za Danieli na rafiki zake wakati walipotupwa katika tanuru ya moto, na „mwingine" alionekana pamoja nao kati ya moto (Dan.3:25). Yesu alisema Roho atakuwa pamoja nao katika mateso (Mt.10:20; Mdo.7:55). Kwa sababu Kristo yu pamoja nao watasikia furaha kubwa, furaha ambayo itaendelea na kuufikia upeo wakati wa Kristo Kurudi.

Kuishiriki aibu ya Kristo katika ulimwengu huo ni ishara thabiti ya kuushiriki utukufu wake katika ulimwengu ujao. Hawatakuwa watazamaji tu bali washiriki wakati wa Kristo kuadhimishwa mbele za watu wote.

k.14 Wanayo heri, ni baraka kulaumiwa kwa ajili ya Kristo, ni heshima kubwa kwa sababu Roho wa Mungu ambaye ni Roho wa Utukufu hukaa juu yao na juu ya Kanisa linapoteswa. Neno „huwakalia" laonyesha kwamba wateswao watakuwa na amani wakati wa dhorubu kuvuma. Wateswao ni watu wa kupongezwa (Mdo.5:41). Petro aliyeandika hayo, mwenyewe alikuwa ameteswa kwa ajili ya Kristo kama ilivyoandikwa katika Matendo ya Mitume.

k.15 Ila Petro alitaka wajue kwamba hayo aliyosema yalihusu mateso kwa ajili ya Kristo, si mateso kwa makosa yao. Ni wazi kwamba mwuaji, mwizi, na mtenda mabaya wastahili kuadhibiwa kwa mabaya yao. Alitaja jambo lingine „mtu ajishughulishaye na mambo ya watu wengine". Si vema Mkristo ajiingize katika mambo ya wengine isipokuwa kwa lazima. Ikimlazimu ajiingize asifanye kwa kiburi au uchokozi. Ni haki atengeneze maisha yake lakini si haki ajaribu kuwasaidia wasioamini kuyatengeneza maisha yao kwa kujiingiza kwa nguvu katika mambo yao pasipo wao kutaka.

k.16 Baadaye wakati ulifika ambapo ilitosha mtu akiri kuwa Mkristo akahukumiwa kosa, yaani kumwamini Kristo tu kulihesabiwa ni kosa.

k.17-19 Si rahisi kuona uhusiano wa vifungu hivi na sehemu iliyotangulia isipokuwa kwa neno la mateso. Kuwa miongoni mwa kwanza kuhukumiwa na Mungu ni afadhali (1 Kor.11:32) kwa sababu hukumu itazidi kuwa mbaya zaidi itakapowafikia wasioamini na wale ambao hawakuitikia wito wa Injili. Neno la hukumu kuanza kwa watu wa Mungu laonekana katika Agano la Kale (Yer.25:29; Eze.9:6; Mal.3:1-5). Shabaha ya Petro ilikuwa kuwatia moyo waumini ili wayastahimili mateso yao kwa sababu iwapo watasikia shida sana haitakuwa sawa na shida itakayapata wale wasiomfuata Kristo. Hivyo wasitafute kuyaepa mateso kwa kumwasi Kristo, maana wakifanya hivi watafanana na mtu anayeruka sufuria ya moto inayopika mboga na kuingia moto mwenyewe (Mit.11:31). Iliyopo wajikabidhi kwa Mungu na waendelee kutenda mema, wasikate tamaa, maana Mungu wao ni Muumba mwaminifu (2 Kor.1:18,20). Yeye huipima na kuisafisha imani kwa yale yanayowapata. Imani yao ni ya thamani sana, vema ipate kibali machoni mwake.

Katika sehemu hiyo liko fundisho kwamba hata waumini wapaswa kupitia chini ya hukumu ya Mungu ili watayarishwe kuingia katika urithi wao. Na kama ni hivyo, itakuwaje kwa wenye dhambi wasioamini? (Mal.3:1-6,17,18; 4:1; 2 The.1:4-10). Wakristo watatoa hesabu kuhusu itikio lao kwa fadhili kubwa ya kumjua Mungu na neema yake (Lk.12:48). Kazi yoyote ya utakasaji huwa na maumivu ila mwisho ni mzuri (Rum.8:18). Ila wasisahau kwamba wamekwisha kukubalika na Mungu na kuhesabiwa haki kwa kumwamini Kristo.

5: 1-5 Maagizo kwa Wazee

Hapo Petro aliwaelekea viongozi wa shirika za palepale, yaani mapasta katika mitaa, na kusema nao kama mmoja wao, bila kuitumia mamlaka yake ya KiMitume. Wazee walikuwa wenye ujuzi wa maisha ya Kikristo nao walipewa wajibu wa kuwaongoza Wakristo wenzao mahali walipo.

Alianza kwa kujiunga nao katika kazi akionyesha jinsi alivyostahili kusema nao kama mtu aliyeyaona kwa macho yake mwenyewe mateso ya Kristo. Hakujiinua kwa kuwa alitambua kwamba yeye bado angali ni mchungaji mwenye wajibu wa kuwachunga Watu wa Mungu, kazi aliyopewa na Yesu wakati Yesu alipokutana na Mitume baada ya Kufufuka Kwake (Yn.21:15-17). Wakati ule aliwekwa na Yesu kuchunga kundi lake pamoja na kuwa shahidi wa Kufa na Kufufuka Kwake. Halafu alijitaja kuwa „mshirika wa utukufu utakaofunuliwa baadaye". Kama Kristo alivyotukuzwa baada ya mateso yake, vivyo hivyo na waumini watakavyoushiriki utukufu wake. Pengine hapo Petro aliwaza wakati Yesu alipogeuka sura na yeye alikuwa mmoja wa wale watatu waliojaliwa kuuona utukufu wake kwa muda mfupi (Mt.17:1ku. 2 Pet.1:15-17).

Viongozi katika shirika walipaswa kuwachunga watu wao. Petro alitumia mfano wa mchungaji na kondoo katika 2:25 aliposema juu ya Kristo na wafuasi wake. Paulo alitumia mfano huo alipoagana na wazee wa Efeso (Mdo.20:28). Ni vema waitwe wachungaji kwa sababu wazee hufanya kazi chini ya Mchungaji Mkuu, Bwana Yesu, nao wapaswa wakifuate kielelezo chake.

Mchungaji huwajibika kuwatunza kondoo, hasa kuwapatia malisho mema, chakula na maji, pia kuuangalia usalama wao, ili wasije wakararuliwa na wanyama au kujikwaa mwambani au kuanguka gengeni. Mchungaji mzuri huwa tayari kuhatarisha maisha yake kwa ajili ya kondoo. Inambidi aweke maisha ya kondoo kabla ya raha zake. Bila shaka Petro alikumbuka hotuba ya Bwana Yesu juu ya Mchungaji Mwema katika Yn.10:11-12.

Daima wakumbuke ya kuwa kondoo ni mali ya Mungu, si mali yao, hivyo yawapasa waangalie sana, kwa kuwa wakimpoteza mmoja tu wameipoteza mali ya Mungu!! Mungu analo kundi moja tu nao wamegawiwa baadhi za kondoo ili wawatunze na kuwahudumia.

Katika k.2 na k.3 Petro alitoboa wazi hali zilizotakikana kwa kufanya ulinganifu mara tatu kati ya hali iliyotakiwa na hali isiyotakiwa. Kwanza „si kwa kulazamishwa" bali „kwa hiari". Pili „si kwa kutaka fedha ya aibu" bali „kwa moyo". Tatu „si kama wajifanyao mabwana.." bali „kwa kujifanya vielelezo kwa lile kundi". Wawe na nia safi, wakifanya kazi hiyo kwa moyo bila kuwa na shabaha ya kupata faida, ama ya fedha, au ukubwa, au nafasi ya kutumia mabavu na kusukuma watu. Hasa watawaliwe na nia ya kutumika (1 Tim.3:8; Tito.1:7). Tena waepe kabisa hali za kiburi na kujiinua na kujiona, bali wafuate

kielelezo cha Mchungaji Mkuu, Bwana Yesu, wakiwa na upendo, uvumilivu na subira kwa kondoo. Mapasta na wazee wamepewa wajibu mzito.

Watapewa thawabu, ila haitakuwa katika ulimwengu huo bali katika ulimwengu ujao. Ni vigumu kueleza thawabu watakayoipata ila uzuri wake utapita mawazo yao yote. Siku zile taji ilihusika na ushindi katika vita au michezo, wao wataushiriki ushindi wa Kristo juu ya mateso na mauti.

5.5 Halafu Petro aliwaambia vijana wawatiini wazee. Je! hao ni vijana gani? Huenda ni vijana miongoni mwa wazee, waliowekwa karibuni hivi kuwa wazee, hivyo aliwaonya wasivimbe kichwa. Kama si hao ni vijana wa umri.

Petro aliendelea na neno kwa watu wote „jifungeni unyenyekevu mpate kuhudumiana". Neno „jifungeni" lilitumikwa kwa kujifunga nguo vizuri isilegee, ili mtu asiweze kuivaa na kuivua kwa upesi. Wafuasi wa Yesu waridhike kuwa watumishi kama Bwana wao alivyokuwa. Bila shaka Petro alikumbuka wakati ule Yesu alipotwaa kitambaa akajifunga kiunoni na kuwatawadha wanafunzi miguu, Yeye alifanya hali akijua ametoka kwa Mungu naye anakwenda kwa Mungu (Yn.13:3-5). Hakuna Mkristo yeyote aliye nje ya wajibu wa kunyenyekeana na kuhudumiana, potelea mbali anacho cheo gani au mahali gani katika Kanisa. Kisha Petro akafunga sehemu hiyo kwa kusema wazi juu ya Mungu kuwa kinyume cha wenye kiburi na kuwa upande wa wanyenyekevu akiwakirimia neema yake (Mt.11:29).

5: 6-11 Maagizo juu ya mambo kadha wa kadha

k.6-7 Petro aliendelea na wazo la unyenyekevu kwa kuwaambia wajinyenyekeze kwa Mungu hasa, kwa sababu Yeye Ndiye hodari na mwenye uwezo wa kuwakweza kwa wakati wake. Wafahamu ni Mungu anayetawala mambo yote, kwa hiyo, potelea mbali wapatwa na mateso au shida gani Mungu huwa juu ya yote. Wakifahamu neno hilo hawatasikia kulemewa au kukata tamaa, maana, mwishowe mambo yatageuka kuwa baraka. Ni Mungu aliye na uwezo wa kuwaokoa na kuwapitisha salama katika shida zao, Yeye aweza kuyageuza mambo mabaya kuwa mema (Zab.76:1; Mwa.45:8; 50:20).

Maneno „mkono wa Mungu ulio hodari" yalitumika katika Agano la Kale kuhusu Mungu kuuleta ushindi kwa kujiingiza kwa nguvu katika mambo ya Israeli (Kut.3:20; 7:5; Kum.5:13; 7:8; 9:26; Neh.1:10; Dan.9:15; Yer.32:21; Dan.9:15).

Katika shida zao wajifunze kumtupia Mungu fadhaa zao zote, wasizibebe wenyewe (Zab.55:22). Ajabu ni kwamba Mungu hujishughulisha sana kwa mambo yao. Ni faraja kubwa sana kujua hayo. Wamkabidhi Mungu masumbufu yao, hawatakuwa huru mbali na shida ila waweza kuwa huru na masumbufu (Mt.6:25ku; Rum.5:8; 8:32; Flp.4:6) na ukweli wa unyenyekevu wao utaonekana.

5.8 Iwapo walihitaji kuwa wanyenyekevu siyo kusema kwamba watulie bila kufanya lolote kana kwamba hawamo vitani. Kweli Mungu huwalinda na kuwahifadhi, hata hivyo, ni juu yao kuuangalia mwenendo wao na kujihadhari na adui mkubwa wa roho zao, yaani Ibilisi. Lazima wakeshe na kuwa na kiasi (1:13; 4:7) kwa sababu adui yao ana shabaha moja tu ya kuwameza na kwa sababu hiyo anawatafuta kwa bidii hali akizungukazunguka ili awapate. Mfano wake ni simba angurumaye, ishara ya ukali wake. Shida na mateso yao yaletwa na watu waonekanao kwa macho ya kimwili, ila nyuma yao yuko adui mkubwa asiyeonekana ambaye ni mpinzani mkuu wa Kristo. Wao wameingizwa katika vita iliyopo kati ya Kristo na Shetani. Shetani alishindwa kumpata Kristo kwa hiyo sasa anayo vita kali akijitahidi kuwapata wafuasi wake (Ayu.1:6-12; Zek.3:1; Ufu.12: hasa v.9-12; Efe.6:12). Budi wakeshe na kuwa na kiasi badala ya kulala na kulewa (1 The.5:6-8), maana yake wawe macho kwa kutambua hali halisi, jinsi mambo yalivyo hasa. Wakikaa ndani ya zizi watakuwa salama kiroho ila wakifikiri kujisalimisha kwa kumwasi Kristo ili waepe mateso, watamezwa. Ni kondoo wanaotoka zizini ambao wanapotea. Wakidumu waaminifu kwa Kristo adui hatawapata (1:5). Shetani ni mshtaki, anawashtaki watu kwa Mungu, na Mungu kwa watu, na watu kwa watu, akitafuta kuuchafua ushirikiano wao na Mungu na ushirikiano wao kwa wao.

k.9 Wafanye nini zaidi ya kuwa macho na kukesha na kuwa na kiasi? Petro alisema „wampinge Shetani". Wampingaje? Kwa kuwa thabiti katika imani na kujua kwamba mateso yao si kitu kigeni bali hata Wakristo wenzao mahali mahali huyapata mateso pia. Wasiwe na mashaka na kuanza kujiulizauliza „kwa nini tunashambuliwa namna hii?" Wawe na uhakika kwamba kuteswa ni dalili njema ya kuwa wafuasi wa kweli wa Kristo (Ebr.12:7,8). Vita yao ni sehemu katika Mungu kuyatekeleza makusudi yake.

Bila shaka Petro alikumbuka jinsi alivyoshindwa kukesha katika Bustani ya Gethsemane na jinsi alivyoshindwa kuwa imara alipotakiwa kukiri kuwa mmoja wa wanafunzi wa Yesu (Mk.14: 37-38; 66-72: Lk.22:31-34). Iwapo hapo Petro ametumia mfano wa simba kwa Shetani ni vema tukumbuke ya kuwa katika Maandiko Shetani ameelezwa kwa mifano mingine na ni hatari anapojificha na kutujia kwa njia ya rafiki (Mt.16:22-23) au kama malaika wa nuru akileta ujumbe mtamu usio wa kweli (2 Kor.11:14).

k.10 Mateso yao ni ya muda mdogo. Kwa maneno hayo Petro hakutaka wafikiri kwamba mateso yao yatakwisha hivi karibuni, ila wajue kwamba mateso yote yana mwisho, na kwa kulinganisha na utukufu wa baadaye, ni ya muda mfupi tu (Rum.8:18). Pia mateso yana mwisho katika maana ya kuwa na shabaha, hayawi bure, kwa sababu Mungu huyatumia kwa kuyatekeleza mapenzi yake ya watu kukua katika neema na katika kumjua Bwana (2 Pet. 3:18). Mungu ni Mungu wa neema yote, anayo neema kwa kila hitaji lao, neema itakayowawezesha kupita salama katika mateso na magumu yote (2 Kor.l2:9). Mapenzi ya Mungu ni kuwaleta kwenye utukufu wake wa milele na

mateso ni jambo mojawapo katika njia iendayo kwenye utukufu. Aliwaita kwa utukufu huo wa milele, kwa hiyo wafarijike kwa kujua kwamba mateso yao ni ya muda tu. Walishikilie sana tumaini lao ili wadumu kuwa waaminifu wakati wa siku za shida.

Mungu Mwenyewe atawatengeneza na kuwathibitisha na kuwatia nguvu. Katika ulimwengu wamefanana na mawimbi ya kurushwarushwa katika misukosuko ya dunia hii, ila Mungu huwatengeneza, yaani Yeye huwarudishia afya na nguvu tena na tena ili wapambane na mambo, kusudi wafae kuwa watumishi wake. Neno „kutengenezwa" ni lilelile lililotumika katika Mk.1:19 kuhusu wavuvi kuzitengeneza nyavu zao. Baada ya kuvua walihitaji kuzirudishia nyavu hali nzuri ya kufaa kwenda kuvua tena, ndivyo afanyavyo Mungu kwa watu wake. Pamoja na kuwatengeneza Yeye huwathibitisha na kuwatia nguvu ili daima wawe tayari kwa lolote watakalolikuta katika kumfuata na kumtumikia Kristo kwa uaminifu. (Flp.1:6; 1 The.5:24).

k.11 Ndipo Petro akaifunga sehemu hiyo na sifa kwa Mungu na uweza wake. Siri ya ushindi wao ni katika uweza wa Mungu si katika hali yoyote ya kwao. Wayainue macho yao Kwake, wawe na uhakika juu ya uweza wa Mungu, kwa wakati wa sasa, na kwa baadaye, hata kwa umilele ujao. Ndipo Petro kwa kutilia mkazo akaongeza neno „amina" maana yake „na iwe hivyo".

5: 12-14 Salaam za kuagana

Hapo inaonekana Petro aliichukua kalamu kutoka mkalamani wake Silwano na kuandika kwa mkono wake mwenyewe salaam za mwisho. Inafikiriwa huyo Silwano ni Sila aliyesafiri na Paulo katika Safari za Uinjilisti. Ametajwa mara kwa mara katika Nyaraka na katika Matendo (Mdo.15:22,27,40; 16:19,20,25,37; 1 The.1:1; 2 The.1:2; 2 Kor.1:19). Wazo la kufikiri Silwano alikuwa mkalamani latokana na maneno „nimewaandikia kwa maneno machache.." hakusema „nimetuma". Hivyo ina maana kwamba Sila aliyaandika aliyotaka Petro akiyatumia maneno yake mwenyewe. Ndiyo sababu Kiyunani cha Waraka ni kizuri. Jambo hilo limewatatanisha watalaamu kwa kuwa waliona vigumu kukubali kwamba Petro aliyekuwa mvuvi aliweza kuandika Kiyunani safi kama kile cha Waraka.

Petro alimsifu Silwano kuwa „ndugu mwaminifu kama nionavyo". Je! Silwano alijulikana na Wakristo wa Bithinia na sehemu zile? Je! alikuwa amefanya kazi kati yao? Hatujui.

Petro alisema amewaandikia kwa maneno machache. Pengine kwa kusema maneno machache alitaka kuonyesha kwamba alikuwa na mengi zaidi ya kusema nao. Au pengine mambo yenyewe yalikuwa makubwa yaliyostahili

kuelezwa zaidi, ila kwa jinsi alivyofikiri alikuwa ameyafupisha aliyotaka kuyaandika.

Alishuhudia shabaha aliyokuwa nayo katika kuwaandikia. Alilenga kuwavuta wazingatie sana neema ya Mungu katika Kristo ili waijue katika maisha ya kila siku. Kwa neema, wameokolewa; kwa neema wamepewa tumaini la uzima wa milele; kwa neema wamefanywa kuwa warithi wa uzima wa milele; kwa neema wamejaliwa urithi usioharibika, usio na uchafu, usionyauka, uliotunzwa mbinguni kwa ajili yao. Kwa neema, wamewezeshwa kuyastahimili mashambulio yote ya adui. Hivyo Petro aliwaita wasimame imara katika neema hii ambayo msingi wake ni katika Injili na kweli zake, Injili ya neema.

k.13 „mwenzenu mteule hapa Babeli awasalimu" Huyo mwenzenu afikiriwa kuwa shirika au kanisa fulani pale Babeli. Tena Babeli siyo Babeli hasa bali ni Jiji kuu la Dola, ni Rumi. Kwani asema „Babeli?". Katika Agano la Kale Babeli ulikuwa mahali walipohamishiwa Watu wa Mungu, mahali pageni kwao. Katika Waraka huo alianza kwa kuwataja walioandikiwa kuwa „wateule wa Utawanyiko" tena katika 2:11 aliwaambia ni wasafiri na wapitaji, ambao mahali pao si hapa, ni raia wa mbinguni na nyumbani kwao hasa ni mbinguni. Kwa hiyo, walioandikiwa ni „wateule" na salaam zatoka „mwenzenu mteule hapa Babeli". Mkazo ni juu ya wote kuwa wateule, watu waliochaguliwa na Mungu kuwa wake ambao waishi popote walipo katika hali ya ugeni wakijihesabu ni wapitaji tu.

Halafu mmoja aliyeitwa Marko na kuelezwa kuwa „mwanangu" alituma salaam pamoja na Petro. Huyo ni Yohana Marko aliyetajwa katika Matendo (Mdo.12:12,25; 13:13; 15:37-39; Kol.4:10ku. Fil.24; 2 Tim.4:11). Alikuwa mjomba wa Barnaba. Watalaamu hufikiri kwamba Injili ya Marko iliandikwa na huyo akipata habari nyingi za Yesu kutoka Petro. Ndivyo mapokeo ya kihistoria yasemavyo katika Maandishi ya Papia na Eusebio.

k.14 „busu la upendo" Petro alitaka Wakristo wauonyesha upendo wao kwa wao kwa tendo lionekanalo la busu. Katika Nyaraka za Paulo „busu takatifu"imetajwa (Rum.16:16; 1 Kor.16:20; 2 Kor.13:12; 1 The.5:26). Ilikuwa dalili ya umoja na upendo wao.

Kisha Petro aliufunga Waraka na neno la „amani". Iwapo wamepatwa na dhoruba ya mateso na mashambulio ya adui, hata hivyo, amani ya Mungu ni yao, Mungu huwapa watu wake kipawa cha amani. Asili yake ni katika Kifo cha Upatanisho cha Kristo Msalabani, na wote walio katika Kristo waijua.

MASWALI

4:1-6: Aliwasihi wafanye nini?
7-11: Aliwashauri mambo gani?
12-19: Wayakabili mateso yao magumu kwa namna gani?

5: 1-5: Viongozi katika shirika za Kikristo walijaribiwa kuwa wa namna gani na Petro aliwashauri wawe wa namna gani?
6-11: Alitoa maagizo gani kwa waumini wote?

Umejifunza mambo gani makuu kutokana na Waraka huo?

WARAKA WA PILI WA PETRO MTUME

YALIYOMO

UTANGULIZI

a) Mwandishi
b) Mahali pa Kuandikwa kwa Waraka
c) Walioandikiwa Waraka
d) Tarehe ya kuandikwa kwa Waraka
e) Sababu za kuandikwa kwa Waraka
f) Uhusiano wa Waraka na Waraka wa Yuda

UFAFANUZI

1: 1-2 Salaam
3-11 Wito wa kukua kiroho
12-15 Haja ya kuwakumbusha
16-21 Ushuhuda wa Mitume na wa Manabii
2: 1-3 Manabii wa uongo na maisha yao mabovu
4-9 Ukumbusho wa Hukumu na Wokovu wa Mungu zamani za kale
10-22 Maelezo zaidi ya uovu wa waalimu wa uongo
3: 1-16 Ukumbusho juu ya Kurudi kwa Kristo

UTANGULIZI

(a) Mwandishi

Ni Mtume Petro kama isemavyo mwanzoni mwa Waraka (1.1). Katika 2 Pet.3:1 mwandishi amesema kwamba amekwisha kuuandika Waraka mwingine. Pia ametaja ya kuwa alitazamia atakufa hivi karibuni (1.15; Yn.21:21-23). Katika 1.16-18 alisema juu ya Yesu Kugeuka Sura na ni watatu tu waliopanda Mlimani na kuwa pamoja na Yesu alipovikwa, kwa muda mfupi, utukufu wake wa asili na Petro alikuwa mmojawapo (Mt.17.1ku).

Baadhi ya wataalamu wameona vigumu kukubali kwamba Petro ni Mwandishi. Hasa kwa sababu wameona Waraka wa pili unatofautiana na Waraka wa kwanza katika hali ya lugha, hata hivyo, siyo tofauti sana. Katika Waraka wa Pili hatuna habari ya Petro kutumia mkalamani na kama hakusaidiwa na mkalamani pengine hii ndiyo sababu ya tofauti katika hali ya Kiyunani chake. Pengine alitumia mkalamani mwingine bila kumtaja. Hatujui kwa uhakika.

Tofauti nyingine ni katika mambo yaliyomo. Alikuwa na sababu na shabaha tofauti na zile za Waraka wa kwanza, kwa sababu hali za waumini zilikuwa zimebadilika. Katika Waraka wa Kwanza walikuwa wakiyakabili mateso na Petro alisisitiza jambo la kuwa na tumaini. Katika Waraka wa Pili walikuwa katika hatari ya kuingiliwa na waalimu wa uongo walioleta mafundisho ya uongo na Petro alitilia mkazo jambo la kuwa na ujuzi wa kweli. Alisema sana juu ya tumaini kuu la Kurudi kwa Bwana Yesu.

(b) Mahali pa Kuandikwa Kwa Waraka

Katika Waraka ni vigumu kujua alikuwa wapi, ila inafikiriwa kwamba alikuwa Rumi.

(c) Walioandikiwa Waraka

Petro hakutaja mahali pao kama alivyofanya katika Waraka wa Kwanza. Yadhaniwa ni watu walewale. Katika 2 Pet.3:1 ametaja kwamba amekwisha kuwaandikia Waraka mwingine. Kwa jinsi alivyoandika inaonekana aliwafahamu, aliandika kama amehubiri kwao na kama ameelewa yatakayowapata hivi karibuni (2.1).

(d) Tarehe Ya Kuandikwa Kwa Waraka

Yafikiriwa kuwa kama B.K..63/64 kabla ya Petro kuuawa na Kaisari Nero. Petro alitaja Nyaraka za Paulo ambazo nyingi zilikuwa zimekwisha kuandikwa na kujulikana katika makanisa. Mapokeo husema kwamba Petro na Paulo waliuawa huko Rumi kama B.K..64 hivi. Petro ameandika kama Kurudi kwa Kristo kumechelewa, na twajua kwamba Wakristo wa kwanza walitazamia Kristo atarudi mapema. Baadaye wazo hilo la Yesu kurudi mapema lilipoa, ili wote walikuwa na uhakika wa Kurudi Kwake.

(e) Sababu Za Kuandikwa Kwa Waraka

Petro alitaka kuwaonya juu ya waalimu na mafundisho ya uongo. Mafundisho hayo yalihusu „uhuru wa Kikristo" ambao wengine walieleza kuwa uhuru wa kufanya walivyotaka, kwa sababu hawakuwa chini ya sheria bali chini ya neema. Paulo aliyapinga mafundisho hayo katika Nyaraka za WaGalatia, WaKorintho, na WaKolosai. Petro alionyesha ya kuwa uhuru wa Kikristo hauwi katika kufanya waliyotaka bali katika kufanya yaliyowapasa kwa kumtii Kristo na kufanya mapenzi ya Mungu. Uhuru wa kufanya waliyotaka uliwafanya kuwa watumwa wa tamaa mbaya (2 Pet.2.19; 1 Pet.2:16; Gal.5:13). Kwa njia hiyo walijifanya kuwa mabwana wa maisha yao na kumzuia Kristo asiwe Bwana wao (2.1; 3:4). Hivyo walikana Kurudi Kwake Kristo wakisema habari hiyo ni hadithi za uongo zilizotungwa na Mitume (1.16; 2 Tim.4:4; Tito 1:14). Katika kukana Kurudi Kwake walikataa jambo la kuwepo kwa hukumu ya mwisho. Petro aliwaonyesha kwamba wale wanaozidhihaki kweli hizo wamejaa kiburi. Petro alikaza kwamba Wakristo wapaswa kuishi maisha matakatifu hali wakijua kwa uhakika kwamba Kristo atarudi.

(f) Uhusiano Wa Waraka Na Waraka Wa Yuda

Sehemu kubwa ya Waraka wa Yuda, yaani kutoka k.4 mpaka k.18 yaonekana katika Waraka wa Pili wa Petro, sura ya pili. Katika Utangulizi wa Waraka wa Yuda tutaangalia neno hilo.

UFAFANUZI

1: 1-2 Salaam

Petro alijiita Simoni Petro na kujieleza kuwa mtumwa na mtume wa Yesu Kristo. Katika Waraka wa kwanza hakutumia jina la Simoni, wala hakujieleza kuwa mtumwa. Neno „mtumwa" lina maana kwamba aliji"funga" kumtumikia Kristo, yaani alijitoa kabisa kufanya mapenzi ya Kristo, Bwana wake. Pia alijiita „mtume" mwenye mamlaka ya Kristo na kwa mamlaka hiyo aliwaandikia.

Wasomaji wameelezwa kuwa „wale waliopata imani moja na sisi, yenye thamani". Waumini wote ni wamoja katika kumwamini Kristo, ama ni mtume kama Petro aliyemwona Kristo alipokuwa hapo duniani, ama ni waumini, haidhuru ni wa tabaka, rika, jinsia au kabila gani, wote wanamwamini Kristo, wote hushiriki Imani moja. Maneno „waliopata..." linaonyesha kwamba wote walikuwa wamejaliwa neema ya kuamini, ni kipawa walichojaliwa, haikutokana na ustahili wao (Efe.2:8-9). Kwa neema waliposikia mwito wa Mungu kwa njia ya Injili kuhubiriwa waliitika vema kwa kumpokea Kristo.

Halafu Petro aliendelea kutaja „haki ya Mungu wetu na Mwokozi Yesu Kristo". Wataalamu wengine hufikiri maneno hayo yamhusu Yesu Kristo, na kama ni hivyo Yesu ameitwa „Mungu na Mwokozi wetu". Neno „haki" laonyesha kwamba Mungu hana upendeleo, Yeye hupenda wote waokolewe, na Kristo alikufa kwa ajili ya wote.

k.2 Kama alivyofanya katika Waraka wa Kwanza Petro aliomba „neema na amani iongezwe" akiongeza maneno „katika kumjua Mungu na Yesu Bwana wetu". Neno „kumjua" limetumika mara tatu (1:3,8; 2.2O). Wakristo wengine walidai kumjua Kristo huku waliendelea na maisha mabovu, lakini Petro hakukubali kwamba waweza kumjua Kristo huku wanaishi maisha mabovu. Kwake ujuzi wa kweli hutokeza neema na amani na utauwa (1:3). Ujuzi wa kweli ni kinga nzuri katika kuyakabili mafundisho ya uongo (3:18). Agano Jipya lote lakaza kwamba ujuzi wa kweli huleta mabadiliko mema kimaisha.

1:3-11 Wito wa Kukua Kiroho

k.3-4 Hapo Petro amesema juu ya Mungu kuwakirimia waumini uwezo wa kiroho ili waishi maisha mema ya utauwa (1 The.4:7). Kwa uwezo wa Mungu wamekirimiwa kila kitu wanachohitaji ili waishi kama Mungu awatakavyo. Yesu aliwaahidi wafuasi wake uzima tele (Yn.1O:1O) na Paulo alishuhudia kwamba neema ya Mungu ilimtosha ayakabili mambo magumu sana (2 Kor.12:9). Pia

Paulo alisema „naweza mambo yote katika Yeye anitiaye nguvu" (Flp.4:13). Neno „ametukirimia" laonyesha kwamba uwezo huo ni kipawa, tusichopata kwa kufanya kazi wala kwa ustahili wetu, la, hata kidogo. Hata hivyo Petro alisema kwamba wao, kwa upande wao, waliwajibika kujitahidi sana (k.5).

Kristo aliwaita waje Kwake na kujikabidhi Kwake ndipo kwa maisha yote waendelee kumtegemea ili wapate kumjua zaidi na zaidi. Kristo awaita watu Kwake kwa sababu ya wema wake na utukufu wake. Watu huvutwa na uzuri wa Kristo (Yn.1:14). Bila shaka Petro alikumbuka sana jinsi yeye mwenyewe alivyovutwa na uzuri wa Kristo alipokutana naye. Petro aliwahakikishia kwamba Yeye aliyewaita Ndiye Yeye anayewawezesha.

Halafu Petro alizitaja ahadi kubwa mno za thamani. Ahadi zilihusu kuzishiriki tabia njema za Bwana Yesu na utukufu wake wa baadaye. Lengo la kumfuata Kristo ni kufanana naye zaidi na zaidi. Walipompokea walifanywa „wana" (Yn.1:12) iliyopo sasa wazidi kufanana na Baba yao kusudi wawe „wana" halisi (Rum.8:15-17,29; 1 Yoh.3:1-3). Kufanywa wana ni sawa na „kuzaliwa upya" na „Mungu kutuzaa" (Yak.1:18).

Baada ya kuokolewa na uharibifu uliomo duniani, uharibifu uliosababishwa na tamaa, wamekuwa „washirika wa tabia ya Mungu". Ahadi ni za thamani kwa sababu Kristo alikufa ili atupatie msamaha wa dhambi na uzima wa milele na uwezekano wa kuishi kwa uwezo wa Mungu (1 Pet.1:19).

Hivyo, Petro alikaza kwamba upo uwezekano wa watu kuokolewa na maovu yaliyomo ulimwenguni. Katika Kristo Mungu amewakirimia uwezo wa kushinda dhambi, uwezo wa kufanywa wana wa Mungu na uwezo wa kuzaliwa kwa mara ya pili na Roho Mtakatifu (Yn. 1:12; 3:1ku). Mungu kwa njia ya Injili ya Kristo huwaita watu waje kwa Kristo (Jiwe hai - 1 Pet.2:4) ili wapate kumjua zaidi na zaidi, si kujua habari zake kwa kichwa bali wamjue kibinafsi, ujuzi unaotokana na kushirikiana naye (Flp.3:10; Rum.8:9; Gal.2:20; 1 Yoh.5:1, 1 Pet.1:2). Kwa kawaida watu hufikiri na kuamini kwamba haiwezekani kuishi maisha matakatifu katika ulimwengu huo mbovu.

k.5ku. „naam, kwa sababu iyohiyo..." Kwa sababu ya kuzaliwa kwa mara ya pili na kwa kupewa ahadi kubwa za thamani juu ya uwezo wa Mungu Petro alisisitiza kwamba iwapo ni kweli kwamba wamekirimiwa uwezo wa Mungu wa kuishi maisha matakatifu, hata hivyo, wao, kwa upande wao, wapaswa wawe na juhudi sana. Neema ileile inayowawezesha ndiyo inayowadai juhudi (Flp.2:12). Ndipo Petro alizitaja tabia njema zilizowapasa. Neno „tieni" lina maana ya kupamba maisha yao na uzuri mbalimbali. Wasiridhike na hali ya kawaida tu, bali waruhusu neema na uwezo wa Mungu kufanya kazi tele maishani mwao wakitumia nguvu na nyakati zao kwa kuishi maisha bora.

Petro alianza na „imani" ambayo ni msingi wa maisha ya Kikristo. Kwa imani yao watie „wema". Neno wema ni lilelile la k.3 kuuhusu wema wa Kristo Mwenyewe, yaani wafanane na uzuri wa Ukristo, wawe na uvutiko kama Yeye. Ndipo kwa wema watie „maarifa" ili ufahamu wao wa kiroho ukue, na kwa hekima waamue na kufanya yampendezayo Mungu. Ndipo kwa ufahamu watie „saburi" ili wastahimili magumu na vipingamizi, hali wakijikabidhi kwa Mungu na kujua hakika kwamba mwisho utakuwa mzuri (Ebr.12:2). Halafu kwa saburi watie „utawa" wamche Mungu na kuwaheshimu wanadamu wenzao, wawe waaminifu kwa Mungu katika mambo yote. Ndipo Petro aliwaambia kwa „utawa" watie „upendano wa ndugu" kwa kuwa uhusiano wao na waumini wenzao ni wa maana sana. Ni tabia iliyokazwa sana katika Agano Jipya (Rum.12:10; 1 The.4:9; Ebr. 13:1; 1 Pet.1:22; 1 Yoh.5:1). Kisha Petro alitaja tabia iliyo kiini cha maisha yote ya Kikristo yaani „upendo" (1 Kor.13:13; 1 Yoh.3:16). Ni upendo uleule uliotajwa juu ya Mungu kuupenda ulimwengu na wa Bwana Yesu kutoa maisha yake Msalabani kwa ajili yetu (Yn.3:16).

Petro aliandika kwa mfano wa ngazi orodha ya tabia njema za maisha ya kiroho, nazo ni ufafanuzi wa tabia za Mungu (k.3).

k.8-9 Wajitahidi kukuza tabia hizo katika maisha yao ya kiroho ili wazae matunda. Kadiri watakavyoshirikiana na Yesu na kumjua ndivyo watakavyozaa matunda (Kol.1:10; Efe.1:4).

k.9 Kinyume cha hayo Mkristo asiyejitia bidii katika imani yake, akiishi kwa mradi tu, bila kutafuta kuwa na zile tabia zilizotajwa, basi, Petro alisema kwamba mtu wa namna hiyo ni kipofu, yaani ni mtu asiye na utambuzi katika mambo ya kiroho. Ni kama amefumba macho yake kwa kusudi ili asipate kuiona nuru ya kiroho, kama mtu asiye tayari kuyapokea yale mazuri yaliyo mbele yake. Ni mtu aliyemezwa na mambo ya karibu ya dunia hii. Mtu wa namna hiyo amesahau kwamba alipompokea Kristo alisamehewa dhambi zake. Hivyo Petro amefundisha kwamba Mkristo asiyesonga mbele yu katika hatari ya kurudi nyuma na kufa kiroho.

k.10-11 Hapo tena twaona uhusiano kati ya kuitwa na kuteuliwa kwao (Yn.15:16; 1 Pet.1:2) na wajibu wao wa kujitahidi sana. Kweli Mungu kwa neema yake amewachagua na kuwaita, kwa hiari yake Mwenyewe, bila wao kustahili, hata hivyo, hawawezi kustarehe na kusema, Mungu ametuchagua, basi tu". Ni juu yao kufanya imara kuteuliwa na kuitwa kwao. Wakifanya hivyo hawatajikwaa, maana yake hawatashindwa kabisa, maana sote hujikwaa katika makosa (Yak.3:2). Uteule wao watoka kwa Mungu peke yake, ila kwa maisha yake mtu ama anaushuhudia ama anaukanusha uteule wake. Uwezo wa kutenda mema hutokana na msaada na neema ya Mungu, ila budi Mkristo atende matendo mema kwa kuwa ni wajibu wake (Efe.2:8-10; Flp.2:12-13). Bila shaka Petro alikuwa akiwapinga waalimu wa uongo waliodai kwamba waliitwa na kuchaguliwa na Mungu, lakini hawakuona haja ya kuishi maisha mazuri,

walihesabu kule kuteuliwa kwao kuliwaruhusu kuishi jinsi walivyojisikia. Paulo katika Waraka kwa Warumi aliyapinga mafundisho ya aina hiyo (Rum.6:1,15).

Petro aliwasihi wakaze mwendo na kusonga mbele ili mwisho wa safari wapate kuuingia Ufalme wa milele wa Bwana Yesu, hali wamefaulu sana. „mtaruzukiwa kwa ukarimu kuingia" maneno hayo yaeleweka tukiwaza mfano wa wanafunzi wawili walioikabili mitihani yao. Wa kwanza aliamua kufanya juu chini ili afaulu akilenga kupata maksi kubwa. Wa pili, mvivu, aliamua kufanya ya kutosha ashinde, mradi apate maksi za pasi tu. Mungu ni mkarimu, yu tayari kuwapa uwezo wote na neema yote ili wafaulu vizuri maisha yao ya kiroho, wawe kama mwanafunzi aliyepata maksi kubwa. Amewapa ahadi nzuri za kuurithi Ufalme wa Mungu. Kwa hiyo, wao kwa upande wao, wawe „wakarimu" katika kujitoa na kutii kwao, wanenepe kiroho, ndipo watapokelewa kwa mikono miwili katika Ufalme wa Mungu. Wakumbuke kwamba wamejaliwa kuuingia Ufalme huo kwa sababu Yesu aliufungua kwa Kifo Chake (Ebr.10: 19). Ni Ufalme wa milele, na ni Ufalme wa Bwana Yesu, nao wataingia kwa njia ya kushirikiana vema naye. Baadhi ya Wakristo hawajali jinsi waishivyo, hawatii maanani imani yao, hao ni mfano wa wale waliozungumzwa katika 1 Kor.3:10-15 hasa k.15 „watu kuokolewa kama kwa moto".

1:12-15 Haja ya kuwakumbusha

Petro aliona amewajibika kuwakumbusha juu ya neema na uwezo wa Mungu na jinsi iwapasavyo kufanya juhudi ili wathibitike katika imani yao. Alifanya hivyo hali akikubali kwamba waliyajua mambo hayo na ya kuwa wamethibitika katika kweli. Ila alikumbuka jinsi yeye mwenyewe alivyojiona kuwa imara iwapo Bwana Yesu alimwonya, ndipo akaanguka, lakini pamoja na kumwonya, Yesu alimpa kazi ya kuwaimarisha wengine (Lk.22:31-34). Alitambua ya kuwa hata wao waweza kurudi nyuma, hasa kwa sababu ya waalimu wa uongo na hila yao.

Aliona ni vema awakumbushe, alisema „ni haki" kwa sababu yeye mwenyewe alitazamia atauawa hivi karibuni. Kama mmoja wa wale walioandama na Yesu alipokuwa hapo duniani alitaka wawe na uhakika juu ya mambo waliyoyaamini, na ya kuwa yalitokea kweli kweli kihistoria, na ni mambo ambayo manabii wa kweli walitoa unabii juu yake. Katika kuwaandikia mambo hayo wao watakuwa na ukumbusho baada ya yeye kuondoka duniani.

k.13 „maskani" yaani „hema" (2 Kor.5:1-4). Neno hilo ni neno zuri kwa sababu ni ukumbusho kwamba kuwapo kwetu hapa duniani ni kwa kitambo tu, tu wasafiri na wapitaji tu.

k.14 Miaka kama thelathini iliyotangulia Bwana Yesu alimwambia Petro kwamba atauawa kama mfia dini (Yn.21:18-19; 13:36). Sasa Petro ni mtu wa umri wa miaka sitini au zaidi, na Nero, mkatili sana, ni Kaisari wa Dola ya

Kirumi. Wakristo walizidi kuwazwa vibaya na kuhesabiwa wasaliti kwa kuwa walimpa „Mfalme" wao Kristo utiifu wao wa kwanza. Hivyo Petro alizidi kuona wasiwasi juu ya usalama wake, akidhani kwamba maneno ya Bwana Yesu juu yake hivi karibuni yatatimia.

k.15 „kufariki kwangu" neno hilo lina maana ya „kutoka" nalo lilitumika kuhusu Kifo cha Yesu (Lk.9:31) ni neno lililotumika mara chache sana katika kueleza kifo. Petro alikuwa akiwaza nini hasa aliposema „watapata kuyakumbuka maneno hayo". Inakubalika na wengi kwamba aliwaza Injili ya Marko kwa sababu inafikiriwa kwamba Marko alizipata habari za Bwana Yesu kutoka Mtume Petro, shahidi wa maisha na huduma ya Yesu, ndipo alizitumia habari hizo kwa kuandika Injili yenye jina lake. Ndivyo watalaamu wengi waonavyo, na Papia, mwandishi wa Kikristo kama B.K.130 alisema hivyo pamoja na mababa wa Kanisa akina Klementi na Ireneo. Kwa njia ya Injili ya Marko wasomaji wake watakuwa na ukumbusho wa daima wa Maisha na Huduma ya Bwana Yesu, na inaonekana Petro alikuwa na mzigo juu ya jambo hilo, maana alisema atajitahidi. Yawezekana alikuwa katika shughuli hiyo alipokuwa akiuandika Waraka huo.

Ni jambo la maana kwa wote wanaochunga roho za watu kuwakumbusha watu wao kweli za imani wasije wakazisahau. Mara kwa mara kweli hizo zapotoshwa na wafundishao uongo. Tena watu wavutwe kusikiliza sauti za dunia hiyo. Daima Mungu aliwaita watu wake wakumbuke matukio muhimu yaliyotokea katika historia yao (Hes.15:40; Isa.46:9; Mal.4:4; Kut.13:3; Yos.1:13; Mdo.20:35; Rum.15:15; 1 Kor.11:24-25; Flp.3:1). Petro alisema kwamba walijua na kuthibitishwa katika kweli (k.12) hata hivyo aliwakumbusha juu yake. Bila shaka alikumbuka jinsi yeye mwenyewe alivyojiona kuwa imara asiweze kuanguka na jinsi Yesu alivyomkumbusha udhaifu wake pamoja na kumpa kazi ya kuwaimarisha ndugu zake baadaye (Lk.22:31-34).

1:16-21 Ushuhuda wa Mitume na wa Manabii

Petro alitia muhuri ukweli wa Imani ya Kikristo kwa kukaza jinsi yeye na Mitume wenzake walivyokuwa mashahidi waliomwona Yesu Kristo na nguvu na ukuu wake, akitaja jambo la kuwapo pamoja naye Alipogeuka sura mlimani na kuvikwa kwa kitambo utukufu na kuisikia sauti ya Baba yake. Baba alimshuhudia Yesu kuwa Mwana wake, mpendwa wake, na ya kuwa alipendezwa naye, maana yake ni Mwana wa kutimiza mapenzi yake. Jambo hilo lilionyesha uwezo wa Kristo na kudokeza Kuja Kwake tena (Mt.24:30; 28:18). Pia lilidhihirisha utukufu wake na adhama yake (Dan.7:14; Eze.16:10). Wingu lilikuwa ishara ya Kuwapo Kwa Mungu na Utukufu Wake na sauti ya Baba ilikuwa ishara ya heshima kuu ya Mwana, hasa kwa jinsi Mungu alivyomwita, „Mwanangu" „Mpendwa wangu" „ninayependezwa naye". Jambo hilo lilikaa sana katika mawazo ya Petro, hakuweza kulisahau. Mambo yaliyotokea wakati wa Yesu kugeuka sana, kwa upande wao na kwa namna

fulani, yalizidi yaliyotokea wakati wa Kufufuka Kwake. Wao hawakuona matukio yenyewe Yesu alipofufuka, hawakuona jiwe likiondolewa n.k. ila walimwona Yesu yu hai baada ya tukio lenyewe la kufufuliwa. Mitume waliomwona Yesu mlimani walihesabu ni thibitisho la Kurudi Kwake tena katika utukufu, wakati wa waumini wote kuushiriki utukufu wake (1:4).

Petro alikuwa akisema hayo kwa kuonyesha mamlaka yake ya kufundisha watu Imani hasa juu ya Kristo kuwa Mwana pekee wa Mungu Baba, na kwa sababu hiyo aliwajibika kuwapinga wote waliofundisha kinyume chake (1 Yoh.1:1-2; 2 Pet.2:1-3).

Waalimu wa uongo walimshtaki Petro na wenzake kwamba wamezitunga na kuzitangaza hadithi za uongo (Tit.1:14; 2 Tim.4:4). Petro alikana kabisa neno hilo akiwashuhudia kwamba aliwaletea habari sahihi za mambo yaliyotokea kweli hapa duniani ambayo mwenyewe aliyaona. Kwa sababu ataendelea kusema juu ya Kristo Kurudi tena, neno ambalo waalimu wa uongo walikataa, Petro aliona jambo hilo la Yesu kurudi tena lilipata nguvu kutokana na habari za Yesu kugeuka sura, bila shaka kwa sababu wakati ule Yesu alivikwa na utukufu wake wa asili.

Lakini Petro aliona lipo jambo jingine linalotia nguvu ukweli wa Imani wanayoihubiri na kuifundisha, nalo ni jambo la unabii. Manabii wa kale walitoa unabii juu ya Kristo kabla ya Kuja Kwake mara ya kwanza. Petro alitaja neno hilo kuwa imara, tena kuwa kama nuru inayong"aa gizani. Liliangaza njia ya Kristo ambaye Petro amemwita „Nyota ya Asubuhi". Yesu ameitwa hivyo katika Ufu.2:28;22:16; Mal.4:2; Hes.24:17. Si wazi ni nini maana ya maneno hayo, wengi hufikiri yahusu Kuja Kwake Kristo mara ya pili, ila baadhi huona yahusu Kristo kuangaza waumini mioyoni mwao.

Petro alitoa onyo juu ya unabii. Alisisitiza kwamba unabii ulitoka kwa Mungu na kupitia kwa watumishi wake manabii hali wakiongozwa na Roho Mtakatifu, hivyo unabii usitafsiriwe kwa kufuata mapenzi ya mtu mmojammoja tu, bali utafsiriwe na Kanisa (kundi la waumini) katika hali ya kumtegemea Roho Mtakatifu Awaongoze ili waifahamu maana yake. Hasa hoja ya Petro ni kwamba kama mengi yaliyotabiriwa na manabii kuhusu Kuja Kwake Kristo mara ya kwanza yalitimizwa ni busara kuujali unabii unaohusu Kuja Kwake mara ya pili, kwa kuwa ni ufunuo uliotoka kwa Mungu kwa njia ya Roho Mtakatifu.

2: 1-3 Manabii wa uongo na maisha yao mabovu
(ling. na Yuda 4-18)
Petro alitaka kuwaonya wasomaji wake juu ya hatari ya manabii na waalimu wa uongo. Aliwaambia kwamba hata zamani za Agano la Kale walikuwepo nao watatokea mara kwa mara katika maisha ya Kanisa, kama Bwana Yesu

alivyosema (Mt.24:24ku). Ni faida kubwa kuwa na manabii wa kweli kama Petro alivyosema katika 1:19 maana unabii ni taa ing"aayo mahali pa giza. Kwa sababu hiyo ni vema waujali unabii wa kweli, ila aliwaonya kwamba unabii usitafsiriwe na mtu mmojammoja tu bali katika jamii ya waumini kwa kuutegemea uongozi wa Roho Mtakatifu na kwa wengi kukubaliana pamoja juu ya maana yake.

Hasa alitaja mambo matatu ya hatari kuwahusu manabii na waalimu wa uongo. Kwanza, hatari moja ni hali yao ya kuingiza mafundisho yao kwa werevu, wakiyachanganya na kweli ili uongo uliomo usipate kuonekana wazi. Petro aliyaita mafundisho yao „uzushi wa kupoteza". Neno „uzushi" zamani zile lilikuwa na maana ya mafundisho „mengine" aliyoyapenda mtu au watu kadha, baadaye Kanisa lilitumia neno hilo kwa mafundisho ya uongo. „uzushi" huleta mafarakano na kusababisha mtu au watu kadha kwa kusudi na kwa kiburi kujitenga na kuamini tofauti na wenzao (Gal.5:20; 1 Kor.11:18-21; Tito.3:10). Petro alifafanua zaidi kwa kusema kwamba „walimkana Bwana aliyewanunua, wakijiletea uharibifu usiokawia". Tangu Yesu Kuja duniani njia ya kweli ni moja tu (Yn.14:6) kwa hiyo kumkana Kristo ni kuondoka katika kweli na kuondoka katika kweli ni sawa na kumkana Kristo. Katika kusema „Bwana aliyewanunua" Petro aliwakumbusha gharama ya ukombozi wao, wamewekwa huru ila si uhuru wa kuamini na kufanya watakavyo, wamewekwa huru ili wawe watumishi wa Kristo, kwa hiyo haiwezekani wajipendekeze hata katika yale wanayoyaamini. Inaonekana hao watu walifanya zaidi ya kutoa maoni, kwa kusudi walizikataa kweli za Mungu. „wakijiletea uharibifu usiokawia" Hayo yote husababisha hukumu kwa wahusika pamoja na mafundisho yao.

k.2 Waalimu wa uongo walikuwa wajanja wakichanganya kweli na hadithi walizozitunga ili wavute watu upande wao. Lakini sikitiko kubwa lilikuwa waliwavuta si kwa mafundisho yao tu bali kwa maisha mabovu. Bila shaka waliwapaka mafuta huku wameificha hila yao. Walipenda sana neno la uhuru wakikaza uhuru usio na wajibu na kufundisha kwamba dhambi yoyote yasameheka kwa sababu wameokolewa kwa neema, kwa hiyo, waumini wafanye wapendavyo, watasamehewa tu. Petro alihuzunika sana, aliona kwamba Imani ya Kikristo itawazwa vibaya na njia ya kweli itatukanwa. Mafunzo hayo yalilisumbua Kanisa la Korintho na makanisa mengine na Mitume kama akina Paulo na Petro walifanya juu chini kutoa mafundisho yaliyopinga mafundisho hayo. Wakati wote walihimiza Wakristo kuishi maisha matakatifu kulingana na wito wa Mungu Mtakatifu aliyewaita.

k.3 Hali nyingine ya waalimu wa uongo ilikuwa kutamani fedha na faida kutoka waumini waliotekwa na mafunzo yao. Hawakuwa na mzigo juu ya mafundisho yao, wala juu ya watu, ila juu ya mfuko wao. Walitamani na kutafuta faida. Shabaha yao ilikuwa kuwadanganya watu. Wao wenyewe waliishi maisha mabovu, dhamiri zao zilikufa ganzi, na Petro alisema kwamba imewabakia hukumu ambayo imekaa macho imeandaliwa tayari na kuwangojea.

2:4-9 Ukumbusho wa Hukumu na Wokovu wa Mungu zamani za kale

Petro aliendelea kwa kuukaza uhakika wa hukumu ya Mungu kwa waalimu wa uongo iwapo ilionekana imekawia. Ila pamoja na kukaza hukumu pia alitaja jinsi Mungu alivyowaokoa waliomcha kama Nuhu na Lutu. Katika kuhukumu na kuokoa Mungu huonyesha kwamba hukumu yake haina upendeleo. Petro alitoa mifano mitatu kutoka Kitabu cha Mwanzo, habari za malaika walioanguka (k.4) na watu wakati wa Nuhu, Gharika ilipowaangamiza (k.5) na wakati wa Lutu na miji ya Sodoma na Gomora kuangamizwa (k.6-8). Petro alifunga sehemu hiyo kwa kusema „Bwana ajua kuwaokoa watauwa na majaribu" (k.9) kwa hiyo neno la mwisho ni huruma.

k.4 „malaika waliokosa" (Mwa.6:1-4; Yud.6; Ufu.12:7) Katika Mwanzo 6 kosa lao lilikuwa tamaa mbaya. Petro ametaja kosa lao kuwa uasi na kiburi kilichosababisha uasi wao. Kabla ya kukosa walikaa katika nuru kuu ya ajabu ndipo wakatupwa shimoni na kulindwa penye giza kuu wakiingojea Sikukuu ya Hukumu.

k.5 Ling. na Mwanzo 7:1ku. Huenda Petro alitaka kuonyesha uhusiano kati ya malaika waliokosa na maovu makubwa ya wanadamu wengi yaliyofuata taz. Mwa.6:1-7. Petro alilinganisha jinsi Mungu alivyomhifadhi Nuhu na familia yake, watu wanane tu, na maagamizi ya wengine wote, watu wengi sana. Bwana Yesu alitumia habari hiyo alipotoa onyo juu ya Kuja Kwake mara ya pili (Mt.24:37-39) na Petro aliitumia katika Waraka wa Kwanza (1 Pet.3:20). Petro alieleza Nuhu kuwa „mjumbe wa haki". Katika Kitabu cha Mwanzo hatuambiwi juu ya kuhubiri kwake, inawezekana alihubiri wakati wote wa safina kujengwa kama miaka mia na ishirini. Kama alihubiri au siyo ni wazi kwamba maisha yake mazuri yalikuwa hotuba kali sana, akiendelea siku kwa siku kumcha Mungu na kumtii kwa kuijenga safina. Watu hawakuwa na udhuru wowote, maana kazi yake ilikuwa wazi kwa wote kuiona, na bila shaka alipoulizwa sababu aliwaelezea watu juu ya hukumu ya Mungu inayokuja ikiwa hawatatubu na kutengeneza maisha yao. Ameitwa „mtu mwenye haki, mkamilifu.. alikwenda pamoja na Mungu" (Mwa.6:9). Petro alikaza wokovu wa watu wanane na maagamizo kwa njia ya maji ya watu wengine wote. Alitaka kuwatia wasomaji wake moyo wa kudumu kuwa waaminifu kwa Mungu iwapo waalimu wa uongo watajitahidi kuwadanganya na kuwaondoa kwenye utiifu wao kwa Kristo. Wote wangaliokoka kama wangalitubu na kuacha dhambi zao. Picha ni ya watu watepetevu ambao hawataka kujali aliyosema Mungu.

k.6-8 Miji ya Sodoma na Gomora: (Mwa.19; Yud. 7). Habari hii ilitokea baada ya Gharika, hukumu ya moto ilifuata hukumu ya maji (2 Pet.3:7). Dhambi ya wenyeji wa miji hiyo ilikuwa nini hasa? Petro alitaja kutokumcha Mungu; Yuda alitaja uasherati. Bwana Yesu alitaja habari hiyo aliposema juu ya Kurudi Kwake (Lk.17:28-29). Petro alikaza jinsi Mungu alivyomwokoa Lutu huku

wenyeji wengi waliangamizwa. Alisema ni onyo kwa wote wasiomjali Mungu na kuishi maisha mabovu, watapatwa na hukumu.

Petro alichora picha ya Lutu, mara tatu alimwita „mwenye haki" „alijitesa roho yake" mtu aliyesikitishwa sana kwa mabaya yote aliyoyaona na kuyasikia alipoishi kati ya watu. Tunaposoma habari zake katika Mwanzo picha ni tofauti, alionekana kuwa mtu wa kujipenda (Mwa.13:10-14). Aliwakaribisha wageni lakini alikuwa tayari kutoa binti zake wawili ili awatulize wale waliotaka kufanya dhambi na wale wageni (19:1ku.) wala hakuwa na nguvu ya kuamua mambo (19:16). Iwapo alichukizwa na dhambi za wenyeji wa Sodoma hata hivyo alikuwa ametulia pale. Alitolewa kwa nguvu sana ili asipatikane katika hukumu yake. Ni kwa huruma na neema ya Mungu tu aliokolewa. Jambo moja zuri lilikuwa dhamiri yake ingali ilifanya kazi, kwa hiyo alitambua dhambi ni dhambi na kujua ni chukizo mbele za Mungu.

k.9ku. Hapo Petro alijumlisha hoja yake juu ya uwezo wa Bwana kuwaokoa watauwa wakati wa majaribu yao. Iwapo Nuhu alizungukwa na umati mkubwa wa wanadamu waliomwasi Mungu, alidumu mwaminifu, ndipo baada ya muda mrefu Mungu alimwokoa kwa njia ya safina na wingi wa maji, maji yaleyale yaliyowaangamiza ule umati wa watu. Vivyo hivyo na Lutu, baada ya kukaa muda mrefu katika Sodoma na kuteswa sana rohoni kwa kuuona ubaya wao, Mungu alimtoa kwa nguvu huku akiwaangamiza wenyeji wa Sodoma na Gomora kwa moto. Wakati wote katika historia ya watu wake Mungu amewaokoa waliomcha kwa kuwalinda kuwa waaminifu Kwake na hata kuwaokoa kwa ajabu wakati mwingine (1 Kor.10:13). Kama Yakobo alivyosema majaribu na mateso huleta baraka kwa wale wayapokeayo kwa furaha (Yak.1:2,3,12). Kama Paulo alivyofundisha si ajabu watu wateswe na kusumbuliwa na wabaya kwa sababu maisha mema ya waumini ni hukumu juu ya maisha mabovu ya watu. Tena wabaya wanaachiwa wasiwe na udhuru kwa mabaya yao.

Bila shaka Petro alikuwa akiwawaza wasomaji wake na waalimu wa uongo waliowasumbua. Hata ikiwa Mungu huonekana kama hafanyi lolote juu yao, muda si muda, hukumu itawapata. Pamoja na hayo waasi „wamewekwa" kwa siku ya hukumu. Kama watahukumiwa wakati huo au baadaye, Bwana anao uwezo wa kuhukumu wakati wowote. Wakijitenga na Mungu aliye asili ya uzima na amani hawawezi kujua hali hizo wakati wa sasa wala baadaye, wakipenda wasipende budi waingojee hukumu ya siku ya mwisho. Si wazi kama Petro alifundisha kwamba wataendelea kuadhibiwa wakati wote (Lk.16:24) wala si wazi kama Petro alifikiri kwamba pamoja na adhabu itapatikana nafasi ya toba (1 Pet.3:10; 4:6).

2:10-22 Maelezo zaidi juu ya uovu wa waalimu wa uongo

Hapa ni picha ya waalimu wa uongo. „waufuatao mwili katika tamaa ya mambo machafu" wengine huwaza kwamba hao watu walikuwa wafiraji/walawiti kama watu wa Sodoma. Kama ni hivyo au siyo ni wazi kwamba waliishi katika uasherati na uchafu wa mwili (Yud.7) „kudharau mamlaka" mamlaka ipi? huenda ni ya Bwana (k.1) au ni mamlaka ya viongozi wa Kanisa mahali walipo.

k.11 „wenye ushupavu" hao watu hawakujali haki, wala mahitaji, wala maoni ya wengine. Walifuliza matakwa yao bila kujali wengine hata bila kujijali wenyewe. Hapa si wazi Petro alikuwa akiwaza nini hasa, pengine alitaka kuonyesha jinsi walivyofanana na watu wa Sodoma ambao hawakuwaheshimu wale malaika wawili waliomjia Lutu (Mwa.19:1ku) au pengine alitaka kuonyesha jinsi walivyofuata mfano wa malaika walioanguka (Mwa.6:1-4) Au pengine aliwaza viongozi wa mashirika yao. Bila shaka hao viongozi waliwakemea na wao waliitika kwa kuwatusi vibaya sana. Petro aliwapambanisha na malaika ambao huwazidi kwa uwezo na nguvu, hata hivyo, hawathubutu kuleta mashtaka mbele za Mungu (Yud.9). Kwa jumla picha ni ya watu ambao hawakuogopa kusema vibaya juu ya wakuu wao, au hata juu ya viumbe vya mbinguni kama malaika. Hawakutia maanani mambo ya kiroho, na kwa sababu hiyo hawakukubali madaraka ya Mungu wala ya watumishi wake katika shirika zao.

k.12 Waliishi kama watu wasio na akili, walitawaliwa na tamaa si kwa akili, hivyo walifanana na wanyama wanaoishi kwa silika (Yud.11). Wanyama huzaliwa na kuishi kisha hukamatwa na kuchinjwa au kuraruliwa na wanyama. Vilevile hao watu watanaswa katika udhalimu na kuangamia. Walidai kujua mambo, kumbe, wamekuwa wapumbavu wakiyatukana wasiyojua (1 Pet.2:15).

k.13 Matokeo ni kuvuna walichopanda (Gal.6:8) watavuna madhara, ujira wa udhalimu wao. Dhambi ina uvutiko mkubwa, inatoa ahadi ya raha, lakini mwishowe mtenda dhambi hapati ile raha aliyoitafuta, mfano wa mdanganyifu ambaye mwenyewe akadanganywa akakosa ujira wa udanganyifu wake. Dhambi kamwe haishibi wala haileti raha. Walizidi kuharibika hata kiasi cha kufanya mabaya yao wakati wa mchana, dalili ya kuharibika sana, maana hawakusikia aibu yoyote. Walihudhuria karamu za upendo zilizofanyika wakati wa Ushirika Mtakatifu. Wakristo walizoea kukutana na kula pamoja kwanza ndipo wakala Chakula cha Bwana. Shida ilitokea katika karamu hizo, Paulo alieleza shida iliyotokea katika Kanisa la Korintho (1 Kor.11:20ku). Kumbe! hata katika karamu hizo hao watu hawakutulia, macho yao yalijaa tamaa ya wanawake wakitafuta wale wasio imara na kuwapotosha. Daima waliendeshwa na tamaa, hawakusimama hata dakika moja katika kutenda dhambi, kama Petro alivyoandika „wenye mioyo iliyozoezwa kutamani", walijaa choyo, na kujitafutia faida ya kimwili. Petro aliwaeleza kuwa „mawaa" na „aibu" katika mikutano yao, kinyume cha wito wao katika Kristo kuwa „bila mawaa" na „bila aibu" (3:14) na tofauti na Kristo Mwenyewe aliyekuwa „bila madoa na mawaa"

(1 Pet.1:19). Kisha Petro aliwaita „wana wa laana" watu walio chini ya laana ya Mungu kama walivyo watu wote wasiomwamini Kristo. Yeye Kristo aliichukua laana yetu ili isiwe juu yetu (Gal.3:10,13). Hao ni „wana wa kuasi" „watoto wa hasira" (Efe.2:2,3).

k.15 Hapo Petro alieleza jinsi walivyopata kuwa kama walivyo. Kwa kusudi waliondoka katika njia iliyonyoka, wakapotea. Njia ya kunyoka ni njia ya kweli (2:2) ni njia ya utii kwa Mungu. Ndipo Petro aliwafananisha na Balaamu, nabii wa zamani, aliyewapotosha Waisraeli. Yeye pia alipenda ujira wa udhalimu. Habari zake zimeandikwa katika Hesabu 22-24 na mkazo ni juu ya choyo yake. Ni yeye aliyesababisha uzinifu wa Waisraeli pale Baal-peori (Hes.31:16; Hes.24; 1 Kor.10:8; Ufu.2:15).

k.16 Inaonekana hao watu walifundisha kwamba Agano la Mungu na watu wake ni imara sana wala hakuna jambo lolote liwezalo kulivunja, wala uasherati wala kuabudu sanamu. Machoni pao mambo hayo yalikuwa madogo sana yasiyoweza kulivunja Agano la Mungu na watu wake. Kwa hiyo walifundisha watu kuridhiana katika maisha ya kijamii na ya kisiasa. Lakini hata wakisema nini ni wazi kwamba Mungu wa kweli haridhiani na dhambi, hakufanya wakati wa Balaamu, wala hata wakati wao hataridhiana na dhambi. Mungu alitumia punda asiyeweza kusema katika kumkemea na kumwonya Balaamu. Huyo punda alikuwa na utambuzi wa kiroho kupita nabii „wazimu" aliyeharibika kimaisha na kiakili kwa sababu ya kupenda faida. Kitu kikubwa kilikuwa ujumbe uliosemwa na punda si uwezo wa punda kusema. Hao waalimu wa uongo walijifariji kwamba hawatapatikana na hukumu ya Mungu, lakini hakika watapata „mshahara wao wa haki" (Mdo.1:18) na mshahara wa dhambi ni mauti (Rum.6:23).

k.17 Hao waalimu wa uongo walileta hali ya „utupu". Petro alitumia lugha „visima visivyo na maji" yaani hawakutoa ile raha na shibe ya maisha iliyotazamiwa; pia walikuwa „mawingi yachukuliwayo na tufani" picha ya watu wasio na msimamo, watu wa kubadilibadili mafundisho yao kulingana na „hewa" ya mazingara yao (Efe.4:14) au pengine maana yake ni kueleza jinsi walivyokosa kuleta maburudiko, au mawingu ni picha ya kitu kinachozuia mwanga, hivyo maana yake ni kwamba hao watu hawakuleta baraka wala wema wowote. Mwisho wao ni „weusi wa giza" walisababisha giza maishani mwa watu nao watavuna giza. Petro alisema „wamewekewa" neno ambalo alitumia kwa waumini kuwekewa urithi usioharibika...(1 Pet.1:4). Ni Kristo tu aliye chakula na maji ya uzima (Yn.4:13-14; 7:38; Yn.6.35).

k.18 Hao watu walisema makubwa, ni kama walivimba katika kusema kwao, kwa kiburi walitumia maneno makubwa wakilenga kuwadanganya Wakristo wachanga ambao hivi karibuni walikuwa wamemwamini Kristo. Hao walikuwa rahisi kunaswa, kwa sababu walikuwa bado hawajaimarika katika imani. Hao

waalimu wa uongo walikuwa wajanja sana, walidai kujua mambo, tena waliwategea kwa ahadi za uongo, kama samaki hutegwavyo na chambo.

k.19 Waliwaahidi nini? Jibu ni „uhuru". Uhuru wa aina gani? uhuru wa kuishi watakavyo bila kujali amri na mapenzi ya Mungu. Kweli wameokolewa kwa neema, bure, bila sheria. Ila shabaha ya kuokolewa kwao ilikuwa waishi maisha mema ambayo hapo nyuma yaliwashinda walipokuwa hawana Kristo wala Roho maishani mwao (Gal.5:13; Mdo.15:29; 1 Pet.2:16). Uhuru walioahidi haukuwa uhuru wa kweli. Hata wao wenyewe walishuhudia uhuru wao kuwa „utumwa" kwa kuwa walitawaliwa na tamaa mbaya (Yn.8:34; Rum.6:16). Uhuru wa kweli ni katika kumjua Kristo na uwezo wake wa kushinda dhambi (1:3-4).

k.20 Inaonekana kwamba hao waalimu wa uongo walimjua Kristo, ama kwa kichwa au kwa moyo hatujui (Mt.13:20-21) ndipo wakarudi nyuma kisha hali yao ya mwisho ilizidi kuwa mbaya kuliko ya kwanza (Mt.12: 45; Lk.11:26). Hatia yao ilizidi kwa sababu waliijua Injili halafu wakaiacha. Wamo hatarini maana hamna njia nyingine ya wokovu. Nguvu yao ya kukataa dhambi ilipungua sana kwa sababu walikuwa wameirudia na kuikumbatia dhambi tena.

k.21 Afadhali wale wasioijua Injili, maana hao hawawezi kulaumiwa kama waalimu wa uongo ambao wamefanya dhambi juu ya nuru waliyokuwa nayo na kuyakataa mafundisho matakatifu waliyopewa. Zaidi ya kuyaacha, wameyapotosha na kuwashawishi wengine na kuwadanganya na mapotovu yao. Ni sawa na kuibadili nuru kwa giza, ni kosa kubwa na uovu mkubwa.
k.22 Mbwa na nguruwe hawabadili tabia yao, hata wakioshwa warudia hali yao na mazoea yao ya kutapakaa katika uchafu (Mit. 26:11; Mt.7:6). Hao watu hawakubadilika kwa ndani, tofauti na Mkristo wa kweli. Mungu hutia muhuri yake kwa yale ambayo mtu ameyachagua. Wao wameyachagua mabaya na Mungu ametia muhuri uchaguzi wao, nao watapatwa na mabaya.

Twaona Petro ameandika kwa kirefu sana juu ya hali za hao waalimu wa uongo. Alikuwa na mzigo sana juu ya wasomaji wake, alikuwa pasta mwenye wajibu wa kuwalinda wasitiwe sumu ya mafundisho ya uongo, wasilogwe na hao watu. Sumu ilikuwa tamaa mbaya, choyo, ulevu, ulafi, kiburi, kuasi mamlaka, n.k. Hatari ilikuwa kwamba sumu hiyo ilifichwa katika peremende tamu sana, ili watu wavutwe na utamu bila kutambua sumu iliyomo ndani. Peremende ilivaa nguo ya dini!!!! hata leo ndivyo ilivyo.

3:1-16 Ukumbusho juu ya Kurudi kwa Kristo

Tumeona ya kuwa katika utunzaji wa Wakristo Petro alifanya mawili hasa. Kwanza aliwatia moyo wa kuishi maisha matakatifu. Pili aliwaonya sana juu ya waalimu wa uongo akitoboa wazi hali zao mbaya na hukumu itakayowapata. Ndipo katika hiyo sura ya tatu amerudia kuwatia moyo kwa kuwakumbusha juu ya Kuja kwa Bwana Yesu, akieleza sababu za kukawia Kwake.

3:1 Alianza na neno la uvutiko sana „wapenzi" akilitumia tena katika k.8,14,17. „Waraka huu ndio wa pili niwaandikiao ninyi" Je! ni Waraka wa kwanza unaotajwa na huu ni wa pili? Wengine wamesikia shida katika kukubali ni Waraka wa Kwanza uliosemwa. Kwa nini? kwanza, Waraka wa Kwanza hausemi juu ya Kurudi kwa Bwana. Pili, Petro hakusema anawakumbusha mambo fulani.

Liko wazo la kufikiri kwamba Petro alikuwa amewaandikia Waraka ambao umepotea. Halafu liko wazo lingine lisemalo kwamba Petro aliandika sura za I na 2 na kuzipeleka ndipo sura ya tatu ilikwenda peke yake. Hayo yote ni mawazo tu hatujui kwa hakika, ikiwa ni Waraka wa Kwanza ni kama Petro amejumlisha mambo yake na kusema ni ukumbusho.

k.1-2 Petro aliweka wazi shabaha yake, alitaka kuwaamsha nia zao safi kwa njia ya kuwakumbusha mambo kadha. Hao waumini ni tofauti sana na watu waliotajwa katika sura ya pili, maana hawakukubali kuambukizwa na mawazo na mabaya ya waalimu wa uongo. Nia zao zilikuwa safi, nao walistahili sifa kwa kuwa wamejilinda na hewa mbaya iliyowazunguka. Petro aliandika kwa hali ya kuwa na matumaini mazuri juu yao. Alitaka kwa njia ya ukumbusho kuwafanya wadumu kuwa watu wa kuyakumbuka mambo makubwa. Kwanza wayakumbuke maneno ya manabii wa zamani pamoja na maneno ya Mitume, Neno la Injili na mafundisho ya Bwana Yesu. Haya maneno ni ujumbe wa kweli wa Mungu na katika msingi huo Petro alijenga hoja ya Kurudi kwa Kristo. Ni ujumbe mwenye mamlaka na ni neno la kutegemewa tofauti na lile la waalimu wa uongo (1:16). Hao waalimu wa uongo walijaribu kuutikisa ujumbe wa Mitume wakisema ni hadithi zilizotungwa.

k.3-4 Petro aliendelea kwa kuwaonya juu ya wale waliodhihaki habari za Kurudi kwa Bwana Yesu. Huenda walikuwa waalimu wa uongo wa sura ya pili (k3b „wafuatao tamaa zao"). Hao watu walijitahidi kutikisa imani katika Kurudi kwa Kristo, maana walijua kwamba wakifaulu kuleta mashaka juu ya Kristo Kurudi, ndipo hofu ya hukumu itapungua na bila hofu ya hukumu wengine hawatajali jinsi waishivyo. Pia wakitia shaka juu ya neno hilo la Kristo Mwenyewe (Mt.10:23; 24:3) basi shaka itaenea kwa mengine yaliyosemwa na Yesu.

Katika dhihaka zao walisema kwamba tangu zamani za kuumbwa kwa ulimwengu haujatokea jambo la ajabu, vyote vimekaa bila mabadiliko, wala Yesu hajarudi kama Alivyosema. Kwa hiyo, „Yuko wapi?" ndilo swali lao la dhihaka. „babu zetu" ni akina nani? yawezekana ni watu kama Stefano, Yakobo, na Wakristo wa kwanzakwanza ambao walikufa kati ya B.K.30-60, au pengine ni mababa wa Agano la Kale, maana maneno „tangu mwanzo wa kuumbwa" yawaingiza hao. Labda Petro aliwaza watu wakati wa Gharika maana katika k.5-7 alitaja habari za Gharika. Lakini si neno walikuwa wakiwaza

akina nani dhihaka yao ilisimama kwamba watu wamekufa na ahadi ya Kristo Kurudi bado haijatimizwa, huku muda unaendelea.

k.5-7 Kwa nini wasomaji wake wasizijali dhihaka zao? Ni kwa sababu hao watu wamesahau, bila shaka kwa kusudi, (hufumba macho yao) kwamba Mungu alijiingiza kwa nguvu wakati wa Gharika na kuhukumu vikali wale walioasi. Wao walisema vitu vyote vimekaa vilivyo, lakini si kweli, Gharika ilibadili sana hali zilizokuwepo. Dunia ya zamani ilitokea kwa Neno la Mungu, yaani kwa mapenzi ya Mungu. Baada ya Gharika Mungu aliahidi kwamba dunia haitaangamizwa na maji tena, bali imewekwa akiba kwa maangamizi ya moto wakati Mungu atakapoleta hukumu ya mwisho juu ya waasi wote, watu wasiofundishika, wasiokumbuka matukio ya historia. Yesu alitumia habari za Gharika katika mafundisho yake kuhusu Kurudi Kwake (Mt.24:37-39). Historia ya ulimwengu imo mikononi mwa Mungu, Muumba na Mhukumu wake.

k.8-10 Yawapasa Wakristo watofautiane na hao waliofumba macho (k.5), wawe na ufahamu, wajue kwamba „wakati" kwa Mungu huwa tofauti na „wakati" kwa wanadamu. Neno hilo ni silaha katika kuwapinga wenye dhihaka. Mungu hatawaliwi na wakati kama sisi, Yeye yu nje ya wakati, kwa hiyo hana haraka ya kufanya mambo (Zab.90:4) „kwa Bwana siku moja ni kama miaka elfu na miaka elfu ni kama siku moja". Kwa hiyo wanapofikiri muda umekuwa mrefu ni kama siku moja kwa Mungu. Lakini wasisahau kwamba miaka elfu ni kama siku moja Kwake, hivyo, aweza kuja wakati wowote. „Wakati" ni kipawa cha Mungu kwetu, naye ametuambia tuutumie vema kwa kukesha, kuomba, na kufanya kazi. Wakiinua macho yao kwa Mungu aliye „nje ya wakati" hawatatawaliwa na matakwa yao ya sasa.

k.9 Ni dhahiri kwamba baadhi ya waumini walifikiri kwamba Bwana Yesu amekawia kurudi, kwa hiyo, Petro alitoa sababu ya maana kuhusu jambo hilo. Ame"chelewa" kurudi, si kwa sababu ya ulegevu, wala udhaifu, bali hasa sababu ni uvumilivu wake, ili atoe nafasi nyingi kwa watu wengi zaidi kutubu na kuokolewa. Kristo atakaporudi, haitakuwepo tena nafasi kwa watu kutubu. Mungu hapendi mtu yeyote apotee. Neno hilo ni la ajabu, nalo laonyesha upendo mwingi wa Mungu kwetu sisi. (Rum.2:4; 11:32-32; 1 Tim.2:4). Petro alikwisha kutaja uvumilivu wa Mungu wakati wa Gharika (1 Pet.3:20) na hapa uvumilivu unahusu hukumu ya mwisho. Mungu haufurahii mauti ya waovu, bali ataka sana na kusubiri sana ili wauacha uovu wao na kuishi (Eze.18:23,30-32). Lakini, hata hivyo, si wote watakaotubu, wengine wataendelea katika uasi, nao wataangamia (k.7).

k.10 Kisha Petro alirudia kusema juu ya uhakika wa Kurudi kwa Bwana. Atakuja kwa siku asiyotazamiwa, kama mwizi afanyavyo (Mt.24:42,43;25:13; 1 The.5:2) ndipo makubwa yatatokea, mbingu zitatoweka, viumbe vya asili vitaunguzwa, na nchi na kazi zake zitateketea, maana yake, hamna kitu kitakachosalia. Yesu ataonyesha mamlaka yake juu ya vitu vyote, wanadamu

wote na uumbaji wote. Ila Petro hakutaka wawaze huo mwisho wa vitu vyote bali wajue kwamba Yesu atakaporudi makusudi ya ukombozi yatatimia na mbingu mpya na dunia mpya zitatokea (Rum.8:19-21).

k.11 Hayo ni mambo muhimu sana yahusuyo Wakristo wote na kugusa maisha yao. Kurudi kwa Bwana ni uvutiko mkubwa kwa Wakristo kuishi maisha matakatifu (1 Yoh.2:28). Ulimwengu huu ni wa muda tu na Mungu anawaandalia watu wake mambo mema zaidi yatakayofuata baada ya ulimwengu huu kutoweka. Neno moja kubwa ni tabia za mtu. Ni muhimu sana wawe na tabia njema, waishi kufuatana na wito wao na katika nuru ya Kurudi kwa Bwana wao, wakijiandaa kwa maisha ya baadaye katika mazingira ya haki (k.13; Lk.12:35; Rum.13:11; 1 The.5:3; 1 Pet.1:13; 4:7-17).

k.12 Wakristo wamngojee kwa hali ya kumtazamia, wawe na hamu ya kufika kwa Siku ile, wakeshe kama Bwana alivyosema na waendelee kumtumikia kwa moyo, kwa sababu kwa kufanya hivyo wataihimiza. Kwa kufanya kazi pamoja na Mungu, yaani kwa kuyafanya mapenzi yake Wakristo husimama bega kwa bega na Mungu katika mipango yake ya kuleta Ufalme wake. Hili ni jambo la ajabu. Ni mambo gani yatakayohimiza hiyo Siku ije? Uinjilisti (Mk.13:10, Mt.24:14; Mdo.3:18-21). Maombi, Yesu alituambia kuomba „Ufalme wako uje". Maisha Mema. Kwa mambo hayo mtu anajenga juu ya mwamba si mchanga (Mt.7:24-27). Kurudi kwa Bwana ni Siku ya Mungu (Ufu.16:14). Ni Siku ya hukumu yake ya moto (k.10; Mal.3:3,4:1; 1 Kor.3:10-15)

Ni faraja na furaha kubwa kwa watu wake kujua kwamba maovu yote yataangamizwa, hata hivyo, Mungu analo neno bora zaidi, ni timizo la ahadi yake ya kutokea kwa mbingu mpya na nchi mpya ambayo haki yakaa ndani yake. Uhusiano kati ya Mungu na watu wake utakuwa mzuri sana na uhusiano kati ya mtu na mtu utakuwa mzuri sana, dhambi haitakuwepo, wala uovu wa aina yoyote haitazuka tena (Ufu.21:1ku). Hasara yote ya Anguko la Adamu itageuzwa kuwa baraka na mapenzi ya Mungu yatafanyika hapo duniani kama huko mbinguni. Ni vigumu kwa sisi wanadamu kujua jinsi hayo yote yatakavyokuwa, hatujui mwili wa ufufuo utakuwaje, wala hatujui dunia mpya itakuwaje, ila twajua kwa hakika kwamba Mungu anakusudia kuleta hayo. Kwa hiyo ni vema tusijibane katika kuwaza ya dunia hii na ya wakati huu tu, wala tusijifikirie sisi wenyewe tu, bali tujue kwamba Mungu anaunda jamii mpya wa wanadamu watakaoishi katika mazingara hayo mpya.

k.14-16 Ndipo Petro aliwaita wafanye bidii katika kuishi kwao (1:10) akiwavuta na neno „wapenzi". Alitaka waonekane mbele za Bwana katika Siku ya Kurudi Kwake, hali hawana mawaa wala aibu ili wawe kama Bwana Yesu (1 Pet.1:19) na wawe tofauti na hao waalimu wa uongo (2:13). Hivyo hawatasikia wasiwasi bali watakuwa na amani mbele zake. Wasiwe hivyo kwa sababu ya Bwana Kurudi tu, bali zaidi waishi hivyo kama shukrani zao kwa Bwana na wokovu wake, na kwa sababu ya uvumilivu wake uliowasubiri mpaka walipofika kwenye

toba na kumpokea Kristo. Pia waishi hivyo kama shukrani zao kwa nafasi zote za kukua kiroho katika kumjua na kumpenda Bwana Yesu.

k.15 Petro alimtaja Paulo kuwa mtu aliyeandika mengi kuhusu Kurudi kwa Bwana. Alisema vizuri sana juu ya Paulo akimwita „ndugu yetu mpenzi" na alisema kwamba aliandika „kwa hekima aliyopewa" maana yake hakutoa mawazo yake ya kibinafsi bali yale aliyofundishwa na Roho Mtakatifu. Paulo alikuwa mnyofu, mafundisho yake yalipatana „katika Nyaraka zake zote". Petro alikiri kwamba alisikia shida katika kuelewa mengine yaliyoandikwa na Paulo na alisema kwamba watu wengine, wasio na elimu na wasio imara walikuwa wameyadaka na kuyapotosha. Walifanya hivyo hata kwa maandiko ya watu wengine siyo ya Paulo tu. Pengine alisemea waalimu wa uongo ambao waliwashtaki Mitume kutunga hadithi za uongo (1:16). Hao watapotea kwa sababu wameisukumia mbali ile kweli iliyoweza kuwasaidia.

k.17-18 Kisha Petro aliufunga Waraka kwa kuwaita na kuwaonya tena akiwavuta kwa kutumia tena neno la „wapenzi". Kweli alisikia mzigo sana juu yao, aliwapenda sana, wala hakutaka wadanganywe na waalimu wa uongo. Tangu mwanzo hoja yake imekuwa moja, ya kwamba, Kristo amefanya yote ya kuwasaidia na wao kwa upande wao wamewajibika kujitahidi sana na kuendelea kukua kiroho (1:3). Kwa kufanya hivyo hawatachukuliwa na hao wahalifu wala hawatanaswa na mafundisho yao mabovu. Hivyo neno la mwisho la Petro kwao ni „jilindeni nafsi zenu" „kueni katika neema na katika kumjua Bwana wetu na Mwokozi Yesu Kristo". Kujua habari za hao watu na mafundisho yao ni silaha kubwa katika maandalio ya kupambana nao. Watawapinga watu wenyewe pamoja na kuyakataa mafundisho yao. (Mk.13:5,9,33).

Mwishowe kabisa Petro alifunga na maneno ya sifa kuu kwa Kristo. Yeye Kristo Atosha kabisa kwa maisha ya sasa hadi mpaka watakapofika kwenye umilele. Utukufu una Mungu. Petro alimtaja Yesu kuwa ameustahili utukufu sawa na Mungu. Vema tumheshimu Mwana sawa na Baba (Rum.11:36; Yud.25; Yn.5:33).

MASWALI
Petro alikuwa na shabaha kubwa ipi katika kuwaandikia Waraka huu wa pili?

1: 3-11 Petro aliwaita kuthibitisha wito na uteule wao kwa njia zipi? Aliwashauri wafanye nini kuhusu imani yao?
12-15 Aliona wamewajibika kufanya nini?
16-21 Kwa nini Petro alitaja ushuhuda wa Mitume na Manabii?

2: 1-3 Kwa nini Petro alisema kwa ukali juu ya waalimu wa uongo? Hatari yao ilikuwa nini?
4-9 Kwa nini Petro alisema juu ya hukumu na wokovu wa Mungu zamani za kale? Alitaka waumini wafahamu nini? Alitaka waalimu wa uongo wafahamu nini?
10-22 Jumlisha hali mbovu za hao waalimu wa uongo.

3: 1-16 Kwa nini Petro aliwakumbusha waumini juu ya Kurudi kwa Bwana Yesu?

Katika Kanisa la leo na mahali ulipo Je! wapo waalimu wa uongo na waumini wa uongo? Kama wapo hao hutoa mafundisho gani? Je! waonaje juu ya Kanisa kuwachukulia hatua? Kanisa liwafanyaje?

NYARAKA ZA YOHANA

YALIYOMO

UTANGULIZI

a) Mwandishi
b) Wakati Waraka ulipoandikiwa
c) Sababu za Kuandikwa Kwake
d) Ukristo wa kweli una nini?
e) Waraka unafanana na Injili ya Yohana
f) Maelezo mafupi ya unostiki
g) Ufafanuzi wa Waraka wa Kwanza wa Yohana
h) Ufafanuzi wa Waraka wa Pili wa Yohana
i) Ufafanuzi wa Waraka wa Tatu wa Yohana.

UFAFANUZI

Waraka wa Kwanza wa Yohana

1: 1-4 Uzima wa milele ulidhihirishwa katika Yesu Kristo
1: 5 – 2:2 Ujumbe Wa Ki-Mitume na madai yake ki-maisha 2:
3 – 27 Vipimo Vitatu Vya Kupima Imani Ya Kweli
2: 28 - 4:6 Mkusanyiko wa vile vipimo vitatu
2: 28 – 3:10 Kutenda Haki
3: 11 – 18 Kipimo cha Upendo
3: 19 – 24 Amani na ujasiri mbele za Mungu
4: 1 – 6 Uhakikishio wa Roho wa kweli
4: 7 – 5:5 Kipimo cha Upendo
5: 6 – 17 Yohana anataja mashahidi matatu 5:
18 – 21 Mambo matatu wanayoyajua

Waraka wa Pili wa Yohana

1 – 3 Uhusiano wa ukweli na upendo kati ya Yohana na wao
4 – 6 Wadumu katika kweli na upendo
7 – 11 Jinsi ya kuwakabili waalimu wa uongo
12 – 13 Taraja la kuja kwao

Waraka wa Tatu wa Yohana

1 – 8 Ujumbe kwa Gayo
9 – 11 Diotrefe
12 Demetrio
13 – 15 Kuufunga Waraka na Salaam

UTANGULIZI

a) Mwandishi

Kwa desturi ya siku zile mwandishi alijitaja, lakini sivyo ilivyo katika waraka huo, hakujitaja. Kwa hiyo mwandishi atakuwa nani? Mtume Yohana alitajwa na Irenio kuwa mwandishi, na Eusebio alifikiri ni yeye. Mtume Yohana aliishi kwa muda mrefu, akimtumikia Bwana kwa uaminifu, akionja neema tele ya Mungu maishani mwake. Mapokeo yenye nguvu yasema kwamba aliishi kwa muda mrefu pale Efeso akiongoza Kanisa la pale na makanisa ya jirani ya Asia Ndogo.

b) Wakati Waraka Ulipoandikwa

Wengi hufikiri ni baada ya mitume wengine wote kuwa wamefariki dunia na miaka zaidi ya 20 tangu Paulo kuimaliza huduma yake. Kama ni hivyo Kanisa limepitia mateso makali ya Kaisari Nero na limetia mizizi mahali pengi. Lakini sasa linashambuliwa vikali na mafundisho ya uongo ya Unostiki, na waumini wako katika hatari ya hila sana ya kudanganywa nao.

c) Sababu Za Kuandikwa Kwake

Yohana aliwaandikia waumini katika makanisa kwa sababu alikuwa na mzigo wa ki-uchungaji juu yao. Pengine wamo katika makanisa ya Asia Ndogo yaliyotajwa katika Kitabu cha Ufunuo, sura ya 2 na ya 3.

Ni wazi kwa lugha anayotumia ya „mimi" „sisi" „ninyi" kwamba anawafahamu binafsi, anawaita „watoto wangu wadogo", anajua hali zao na historia yao kiroho. Anawapenda sana, na shabaha yake ni kuwalinda wasipotoshwe na waalimu wa uongo na mafundisho yao yasiyo kweli - taz. 1 Yoh 2:26 na 3:7. Vilevile wasidanganywe na uvutiko wa dunia 2:18,22; 4:1-6 na 2 Yoh 7. Asili ya hayo yote ni Shetani na uovu.

Yohana anatamani sana kuwajenga katika imani, upendo na utakatifu 1:4 wakikua katika hayo furaha ya wote itatimilika ili wasifanye dhambi 2:1. Pia anataka wawe na uhakika wa uzima wa milele 5:13. Wakristo walivutwa kuiepa shida kwa kuridhiana na mambo mbalimbali, baadhi yao walioridhiana ni Wanikolai - taz. Ufunuo 2:6, 14-15. Unostiki umeinua kichwa chake, mwalimu wake mmoja aliyeitwa Cerinthus aliishi Efeso. Kwa waraka huo twajifunza kwamba tayari waumini wengine wameacha Kanisa 2:19 hata wengine wamekuwa tayari kuyaeneza mafunzo yao ya uongo 4:1, 2 Yoh 7. Hata hivyo wengine wamebaki, na ni hao ambao Yohana anawaandikia, akitaka kuwasaidia na kuwatia moyo wadumu katika imani ile ile waliyo nayo.

Ilimbidi Yohana apambanue kati ya Wakristo wa kweli na wasio wa kweli. Anakaza uhusiano muhimu wa imani ya kweli na maisha mema. Wasio wa kweli walimkana Yesu kuwa Mwana wa Mungu aliyezaliwa kuwa mwanadamu

kweli 2:22. Walitofautisha Yesu wa mbinguni na huyo aliyezaliwa duniani, ndiyo sababu Yohana anatilia mkazo wa Yesu kuzaliwa kweli na kuwa mwanadamu kweli.

Kitabu hicho kinatusaldia kuipata picha ya Kanisa na maisha yake wakati likikaribia mwisho wa karne ya kwanza. Kwetu msaada mkubwa unapatikana ili sisi nasi tuwe na uwezo wa kupambanua Ukristo wa kweli na usio *wa* kweli, kwa vile iwapo aina ya mafundisho ya uongo si ile ile hata hivyo wengi hudai kuwa wakristo huku ama mafundisho yao au maisha yao si ya kweli.

d) Ukristo wa kweli una nini?

Katika waraka huo twajifunza Ukristo wa kweli ni:

1. Kumwamini Yesu ni Kristo Mwana wa Mungu, aliyezaliwa kweli na kuwa mwanadamu kweli:
2. Wajibu ni kuzitii amri zake:
3. Kupendana sisi kwa sisi.

e) Waraka Unafanana Na Injili Ya Yohana

Yohana hupenda sana kupambanua mawili yapinganayo kama nuru na giza; uzima na mauti; pendo na chuki; kweli na uongo; watoto wa Mungu na watoto wa Shetani, wasio wa ulimwengu huu na walio wa ulimwengu huu; walio na uzima na wasio na uzima wa milele, wanaomjua Mungu na wasiomjua Mungu. Hakuna nafasi kwa „ya katikati".

Alipoiandika Injili aliiweka wazi shabaha yake katika Yoh.20:30-31. Vilevile katika waraka - taz. 1 Yoh 5:l3 „nimewaandikia ninyi mambo hayo, ili mjue ya kuwa mna uzina wa milele, ninyi mnaoliamini Jina la Mwana wa Mungu".

f) Maelezo Mafupi ya Unostiki

Aina nyingi za mafundisho ya Unostiki zilitokea. Nyingine hazikutumia lolote la Kikristo, wala kugusa Kanisa. Hatari ilitokea kwa wale waliodai kuwa Wakristo na kumweka Kristo ndani ya mafundisho yao. Kwa hiyo ni vigumu kueleza aina zote za Unostiki isipokuwa kuchukua makubwa yaliyotokea mara nyingi katika mafundisho yao. Walisema kwamba wako wachache waliojaliwa kuwa na „nukta ya nuru", hao ni wa kipekee kiroho. „Mwili" na „vitu" vina asili katika uovu, ndiyo sababu walimkana Yesu kufanyika mwili kweli, ila alionekana kama ni mwanadamu tu, lakini hakuwa mwanadamu kwelikweli. Kama ni hivyo wengine walifundisha kwamba mtu hana budi kujiepusha kabisa na mambo yote ya dunia hii. Wengine walifundisha kinyume cha hayo wakisema kwamba basi, kama vyote vina asili katika uovu, si kitu, tuvishiriki, mradi tu, tunayo hiyo nuktu ya nuru, kitu kikubwa ni roho zetu, mwili si kitu.

Yohana aliyajibu hayo kwa kukaza tabia ya Mungu kuwa nuru, na jinsi anavyojifunua wazi (si kwa siri) kwa yeyote amtafutaye 1 Yoh 1:5. Ni imani katika Yesu Kristo inayotuletea kwenye kushirikiana na Mungu. Ndiyo sababu

Yohana anakaza umuhimu wa Wakristo kufahamu, kujua, wawe na uhakika, wawe wajasiri.

WARAKA WA KWANZA WA YOHANA

1: 1-4 Sura ya Kwanza

Kama tulivyoona katika utangulizi hamna salaam wala kujieleza. Mara Yohana anaeleza ujumbe halisi wa KiMitume. Mwana wa Mungu ni wa milele, hali akiwa na Baba katika huo milele. Ndipo aliingia ulimwenguni kwa kufanyika mwili, akiitwa Yesu Kristo. Uthabiti wa mambo hayo ni kwamba Mitume walimwona na kumsikia, walimgusa na kumtazama, uhakikisho wa nguvu wa Yesu kufanyika mwili kweli. Katika hao waliomgusa na kumwona ni Yohana mwenyewe. Kwa sababu yeye na wenzake walishirikiana na Yesu kwa ukaribu sana walistahili kuwekwa na Yesu kuwa mashahidi wa kuona.

Hakuna mwanadamu awaye yote ambaye angeweza kumwona Yeye aliye na Baba milele na milele bila Baba kuchukua hatua ya kumdhihirisha kwa wanadamu. Kuzaliwa kwa Yesu Kristo ni tukio la ki-historia, na kazi ya Mitume iliyo muhimu ilikuwa kumshuhudia na kuzitangaza habari zake.

Kwa jinsi alivyoyaandika maneno ya kwanza ya waraka ni dhahiri kwamba ni Kristo wa milele aliyezaliwa hapa duniani, Yeye ni mmoja akiwa Mungu kweli na mwanadamu kweli.

Yohana alitaka waumini waushiriki ujuzi huo huo waliokuwa nao mitume taz. k.3. na ushirika huo ni kati ya mitume walio mashahidi wa kuona, na waumini walioupokea ushuhuda wao pamoja na kuwa ushirika kati ya hao wote na Mungu Baba. Kwa neno hilo Yohana anawapinga Wanostiki waliodai kwamba kuna baadhi tu waliojaliwa „nukta ya nuru". Yohana anafundisha kwamba wote walio tayari kuupokea ushuhuda wao huingia huo ushirika wa Baba sawa na Mitume, Kanisa si chama cha siri. Furaha yao hutimilika katika kuutoa ushuhuda wa kweli juu ya Kristo ili waumini waletwe kwenye nafasi njema na baraka kubwa ya kushirikiana na Baba kwa njia ya Yesu Kristo.

Mitume walipewa mamlaka ya kuutoa ushuhuda huo. Je! awezaje mtu kulishuhudia jambo fulani bila kuliona mwenyewe? Waliwekwa na Yesu na ujasiri wao ulitokana na mawili, (i) walimwona Mwenyewe (ii) waliagizwa na Yesu kumshuhudia. Katika kuishuhudia kweli ilimbidi Yohana awapinge wapinzani walioukana ukweli wa Yesu kuzaliwa na kuwa mwanadamu kweli.

Kwa njia ya Injili Yesu anakusudia kuuunda ushirika unaoendelea miaka kwa miaka, ni wa watu ambao wameunganika pamoja kwa kuwa wamepatanishwa

na Baba na upeo wake utafikiwa katika uzima wa milele watakapoishi pamoja na pamoja na Baba na Mwana huko mbinguni, upeo wa furaha yao - Zab. 16:11.

1:5 - 2:2 Ujumbe Wa Ki-mitume na madai yake ki-maisha

k.5 Kama ambavyo tumekwisha kuona, Yohana hakuuunda ujumbe wake, ulitokana na kuona, na kusikia kwake. Mungu ni nuru, kwa hiyo tabia yake ni „kujifunua". Zamani alijifunua kwa njia ya Torati - taz. Zab.119:105,130. Mithali 6:23. Alijifunua kwa njia ya manabii - 2 Petro 1:19. Halafu alijifunua kwa njia ya Kristo aliyeitwa „nuru ya wamataifa" Isaya 42:6, na 49:6, 2 Kor 4:6. Yesu Mwenyewe alijidai kuwa „nuru ya ulimwengu" Yoh 8:12. Paulo na Baranaba walieleza huduma yao kuwa wa kuleta nuru - Mdo 13:46/47 na 26:18,23.

Mungu ni Nuru na giza hamna ndani yake, kwa hiyo haiwezekani asijali maovu na dhambi na kuridhiana nayo. Tena Mungu ni kweli, na nuru inayozungumzwa ni nuru ya „ufahamu" na „ujuzi wa kweli" Giza ni kutokufahamu na kupotoka katika kweli. Nuru na „mema" „haki" ni mamoja - taz. Isaya 5:20, Efeso 5:8-15, Yoh 3:19-21. Lakini haitoshi kuijua kweli - hatuna budi tuifanye; wala haitoshi kuwa na nuru, twapaswa tutembee ndani yake. Mara kwa mara „kweli"imewekwa kama ni kinyume cha maovu (si kinyume cha uongo) Warumi 1:18, 2 Thes 2:12.

Yohana anatumia lugha „kama tukisema....." kama anawajibu watu fulani, wale waliofundisha kinyume. Walikuwa wakisema nini? (1) walidai kwamba walikuwa wakishirikiana na Mungu, huku wanatembea katika „giza" la mwenendo mbovu. (2) walidai „hatuna dhambi" na „hatukufanya dhambi".

Msingi wa Yohana akiyajibu mafundisho hayo ni kusisitiza kwamba yapasa kutazama mwenendo wao. Kama Mungu ni nuru imani na matendo vyaenda pamoja. Atawezaje mtu kushirikiana na Mungu aliye Nuru ikiwa anaishi „gizani" Kuna ushirika gani kati ya Nuru na Giza? Hao waalimu wa uongo hawakuchukua kwa uzito jambo la dhambi, baadhi yao walikana kuwepo kwa dhambi katika utu wetu, hawakuhesabu ni kitu kibaya, wala hawakukubali inagusa uhusiano wetu na Mungu.

Mungu ni nuru, kwa hiyo njia ya kushirikiana naye ni kuukiri ukweli wa dhambi na ubaya wake, kuiungama, na kuupokea utakaso alioutupatia Yesu Kristo kwa kufa kwake - taz. 1:7, 9 na 2:1-2.

Kwa njia gani Wanostiki walifundisha kwamba dhambi haiharibu ushirika wetu na Mungu? Kwao roho haiguswi na matendo ya mwili, mwili ni kama bahasha ya roho tu, kitu cha maana si bahasha, bali „roho" iliyo ndani. Pia wengine walifundisha kwamba kuna wa kiroho sana, hao wamefikia hatua ya mbele wasiweze kuguswa na dhambi.

Katika habari ya „dhambi" Neno la Mungu lasema wazi kwamba dhambi huleta shida na utengano kati ya mtu na Mungu - taz. Zab 5:4, 66:18, Isaya 59:1-2, 2 Kor 6:14 „tukisema hatuna dhambi na tukidai tunashirikiana na Mungu huku tunafanya dhambi, twasema uongo".

k.7 „kutembea nuruni" ni nini? ni kuwa bila hila wala udanganyifu wala kujificha. Watembeao nuruni wana baraka mbili, (a) wanashirikiana vizuri na wengine na (b) wanatakaswa daima na damu ya Kristo, mawaa ya dhambi husafishwa kila siku na kila saa, „damu ya Kristo yatusafisha" yaani inaendelea kutusafisha moyoni bila kukoma.

k.8-9 Wazushi hawakukubali ya kuwa dhambi imo katika utu wetu, au ikiwa imo, waliona hatuna hatia nayo. Mkristo wa kweli huzikiri dhambi zake na kuziungama na kuupata msamaha ulioahidiwa katika Agano Jipya, Mungu ni Yeye ashikaye Agano - taz. Yer 31:34. Mungu amedhihirishwa kuwa Mwaminifu na wa Haki kwa kutupatia utakaso maana aliziadhibu dhambi zetu katika Yesu Kristo - Yesu alifanywa kuwa dhambi, na dhambi zetu ziliwekwa juu yake taz. 2 Kor. 5:21 na Isaya 53:5. Kwa gharama hiyo alidumu kuwa wa Haki, akiichukia dhambi kabisa kabisa na kutupenda upeo akitupatia njia ya kusamehewa na kuishinda. Si tamko la ahadi kama maneno tu, ni tendo lililofanyika Yesu alipokufa msalabani. Itikio letu ni kuziungama dhambi zetu, tunaonywa tusizifiche Zab 32:1-5, Mithali 28:13.

Kuukana ukweli wa kuwepo kwa dhambi, na kuupunguza uzito wake ni sawa na kumfanya Mungu kuwa mwongo.

2:1 Tuiwazaje dhambi? Kwa sababu imo katika utu wetu, Je! turidhiane nayo? la. Kwa sababu Mungu yu tayari kutusamehe eti tusiiwaze kwa uzito? Mungu anapotusamehe anataka sisi tuzidi kuutambua ubaya wake na kuichukia, ili tuisendelee katika dhambi. Yohana anafundisha habari hiyo kwa shauri la „msitende dhambi" hata hivyo anafahamu haiwezekani kuishi bila dhambi yo yote, tutaangka bila kukusudia kuanguka, kwa hiyo ameweka mlango wa kupitia tunapoanguka -„mtu akifanya". Kweli anatamani sana waumini waishi bila kutenda dhambi, anawasihi sana „msitende dhambi". Kuna tofauti kati ya kutokujali dhambi na kuwa na uzoefu nayo na kujitahidi kutokufanya dhambi huku mara kwa mara tutafanya dhambi fulani. Hatuwi wakristo wa kweli tukiendelea katika dhambi bila kujali. Tukumbuke Yesu alipomsamehe mama mmoja aliyefumaniwa, alimwambia „usitende dhambi tena" Yoh 8:10-11.

k.1-2 Katika vifungo hivyo Yesu ameelezwa kuwa:

(a) Mwombezi kwa Baba, anafanana na mteteaji wa baraza, asimamaye upande wa aliyeshtakiwa ili amtetee. Mbinguni Yesu anampinga mshtaki wetu Ibilisi Ufunuo 12:10. Katika kututetea hauonyeshi uzuri wetu, la! ila anaweka kifo chake upande wetu kuwa faida yetu.

(b) Yesu Kristo mwenye haki: Mwokozi aliyetuokoa alifanya kwa msingi wa haki, alidumu mwaminifu kwa Baba, kwa maisha yake yasiyo na dhambi na kwa kufanya mapenzi ya Mungu kikamilifu, amestahili kututakasa sisi na udhalimu wetu wote.
(c) „naye ndiye kipatanisho kwa dhambi zetu" Msalabani alitupatanisha na Mungu na kukivunja kiambaza cha uadui kilichosababishwa na dhambi zetu, ili atulete kwa Baba Ef.2:14-16, 1 Petro 3:18.

Mungu daima huwa na ghadhabu juu ya dhambi, ila si ghadhabu isiyo na kanuni, isiyotawaliwa, imekazwa katika hali ya tabia yake. Ghadhabu yake kwa dhambi haipishwi kwa rushwa, wala kwa kuridhiana nayo, wala kwa kuipatia udhuru, La! Ghadhabu yake imetulizwa na Kifo cha Upatanisho wa Yesu Kristo, na katika tendo hilo la ajabu Pendo la Baba na Mwana limedhihirika na kuonekana wazi.

k.2 „dhambi za ulimwengu wote" maana yake ni kwamba katika kifo cha Yesu uwezekano upo kwa dhambi yo yote, wakati wo wote, mahali po pote kusamehewa. Ni wale wenye kuungama na kuupokea msamaha ambao watafaidiwa na kifo chake. Hakuna njia nyingine iwayo yote ya dhambi kusamehewa, faraja ni kwamba hakuna aliye nje yake akiwa tayari kuungama.

2:3-27 Vipimo Vitatu Vya Kupima Imani Ya Kweli

Katika sehemu hii Yohana anatoa vipimo vitatu vya kupima imani. Kimoja chahusu maisha, nacho ni utii. Kingine chahusu jamii, nacho ni upendo, na cha tatu chahusu imani, nacho ni kumwamini Kristo.

2:3-6 Kipimo cha Utii Tazama k.3 na 5 „kwa njia hii tunaweza kujua" Kujua nini? Kujua kama tunampenda Mungu kweli kwa kuzishika amri zake.

k.5 „katika hili twajua ya kuwa tumo ndani yake". Wanostiki walidai ujuzi wa kipekee na wa siri. Yohana anaonyesha dai lao kuwa si la kweli ikiwa maisha yao hayapatani na Neno la Mungu - kif.4 na 6. na Tito 1:16. Si kosa mtu adai „anamjua Mungu" taz. Yer.31,34, Yoh 17:3, kosa ni kudai hivyo huku maisha yanakanusha madai yake kwa sababu maisha anayoishi ni kinyume cha tabia ya Mungu, Ni uongo, na Yohana haogopi kutumia lugha kali na kuwaita „waongo". Mtu atajua na kuwa na hakika ikiwa anamtii Mungu na kuzishika amri zake. „Kujua" maana yake hapa ni kushirikiana na Mungu, si kujua kwa kujibu kwa usahihi maswali ya kumweleza. Si jambo la akili bali ni jambo la utii. Mtu anayetaka kumtii Mungu atajitahidi kuyafahamu mapenzi yake na kuyafanya.

k.6 Kuwa „ndani ya Kristo" ni kumjua na kumpenda ni sawa na maana ya „uzima wa milele" tazama maneno ya Yesu katika Yohana 17:3.
Yohana anayajibu yaliyosemwa na watu k.6 „yeye asemaye". Mkristo apaswa kufanana na Bwana wake na kukifuata kielelezo chake.

2:7-11 Kipimo cha Upendo
Yohana aliona amri hii ni ya zamani kwa sababu ni ya msingi, tena ni mpya kwa sababu ya Yesu kuikaza na kuitilia maana mpya. Ni kupenda kwa jinsi Yesu alivyotupenda, bila kujijali na kwa kujitoa mpaka kufa.

k.8 Yesu ameanzisha dahari au wakati mpya. Wakristo wamewekwa huru Gal 1:4, wanazionja nguvu za dahari mpya Ef 6:5, 1 Kor 10:11. Amri ya kupendana yahusu dahari hiyo mpya ni kama „hewa" yake.

k.8-9 Nuru na upendo vyakaa pamoja na kinyume chake ni giza na chuki, navyo vyakaa pamoja. Mtu akidai kwamba anatembea nuruni hali anayo chuki, tayari amelikanusha dai lake la kuwa nuruni. Mkristo wa kweli anamtii Mungu, na anampenda ndugu yake, ushirikiano wake na Mungu ni sawa, pia ushirikiano wake na watu ni sawa.

k.10-11 Jinsi tunavyoishi na watu ni picha kamili ya kuwa „nuruni" au „gizani" Chuki inatupofusha tusiweze kuhukumu vizuri. Upendo huleta kuona vizuri, na tunapohukumu wengine hukumu zetu zitaelekea kuwa za haki.

k.12-14 Kabla ya kuendelea na maelezo ya kipimo cha tatu cha imani ya kweli, Yohana ameona vema aseme na Wakristo anaowaandikia, maana anawahesabu kuwa wa kweli. Amewaweka katika vikundi vitatu, „watoto" „baba" na „vijana" huenda si mpango kufuatana na umri zao, bali kwa hali zao kiroho. Kama ni hivyo „watoto" watakuwa wakristo wapya, ambao karibuni hivi wameanza maisha ya Kikristo. „Baba" watakuwa hao wa siku nyingi walio na ujuzi mwingi ki-binafsi wa maisha ya kiroho, wenye kukomaa kiroho, wazima wa imani. „Vijana" watakuwa wakristo walio vitani wanaopigana kwa ushujaa na Shetani, dunia na mwili. Wana nguvu kutokana na Neno la Mungu, wakifahamu vizuri maana ya kuwa Wakristo.

2:15-17 Mkristo na uhusiano wake na dunia hii
„Dunia" ni nini? neno „dunia" linajumlisha maisha na mipango ya wanadamu vinavyotengenezwa bila kumjali Mungu na mapenzi yake, na „dunia" katika hali hiyo ni chini ya Shetani. Mkristo wa kweli hana budi kuichukia, Yohana asema „msiipende dunia".

Yohana alishauri hivyo kwa sababu mbili:
(a) haiwezekani kumpenda Baba na kuipenda dunia, maana vinapishana kabisa:
(b) dunia ni ya wakati huu wa sasa tu, haitadumu, tofauti na Mungu ambaye ni wa milele na mapenzi yake yatadumu milele na wote wanaoyafanya pia.

Kwa hiyo, Yohana anatufundisha kumpenda Mungu 2:5 na kumpenda ndugu 2:10 na kutokuipenda dunia 2:15.

Tukumbuke ya kuwa dunia ilimkataa Yesu Kristo alipokuja duniani. „tamaa ya mwili" ni katika utu wetu wa asili -„tamaa ya macho" ni kuvutwa na vitu vionekanavyo, vya nje, bila kuwaza „thamani ya kweli", ni kupenda vitu kuliko kupenda tabia njema za ndani kama wema, upendo, uvumilivu n.k. Twakumbuka watu kama „Hawa" (Mwa 3:6) na Akani (Yos 7:21) na Daudi (2 Sam 11:2) „kiburi cha uzima" ni hali ya kujivuna na kujitegemea na kujiona, kufurahia cheo, sifa, anasa, na vitu tulivyo navyo.

k.17 „dahari mpya imefika tayari" Ile iliyopo imekwishahukumiwa. Inaendelea kupita na kuufikia mwisho wake wa kuondoka kabisa isiwepo tena. Dahari mpya ipo nayo itazidi kuendelea kuwepo na kuufikia upeo wake katika uzima wa milele na kukamilishwa kwa Kuja kwake Kristo mara ya pili. Wote waliomo katika dahari mpya wataendelea kuwepo na kuufikia uzima wa milele - taz. Mko 3:35, Yoh 8:35; 12:34.

2:18-27 Kipimo cha imani ya kweli
Katika vipimo vya Yohana kuhusu Mkristo wa kweli, hicho ni cha tatu. Yohana anapambanua Mkristo wa kweli na asiye wa kweli. Tukumbuke ya kuwa wanaoandikiwa wanawafahamu wenzao, waliosali pamoja nao na sasa wamewaacha na kufuata mafundisho mengine wakisema kwamba wamepata ujuzi mpya. Yohana anasema juu ya hao walioondoka „hawakuwa wa kwetu" maana yake hawakuwa wa kweli, kama wangalikuwa wa kweli wasingaliondoka. Waliobaki wamethibitishwa kuwa wa kweli, watu wasiopotoshwa - taz. Luka 12:2, 1 Kor 3:13; 4:5. Alama moja ya wateule ni kudumu kwao Mko 13:13.

Si kwamba wokovu ni thawabu ya wenye kudumu, la, si thawabu, ila kudumu kwao huwa ishara thabiti ya „uteule" wao Ebr 3:14. Yohana ametumia lugha „mpinga Kristo" Wapinga Kristo huunga mkono kazi ya Shetani, wanashiriki tabia yake ya uongo, upinzani, na udanganyifu, waalimu wa uongo waliitwa manabii wa uongo 4:1.

k.20 Pengine ni afadhali kusoma „ninyi nyote mnajua" badala ya „mnajua yote" Kiyunani hakiwi wazi. Mkristo amepewa Roho Mtakatifu, kipawa kwa kila muumini na kwa kipawa cha Roho Mkristo anaweza kuutambua ukweli.
k.22-23 Wazushi walisema Yesu aliyezaliwa duniani si Mwana wa Mungu. Alionekana kama mwanadamu lakini hakuwa mwanadamu kweli. Kwake Yohana kumkana Yesu ni sawa na kumkana Baba, kwa sababu Baba alimshuhudia Yesu kuwa Mwana wake, na kuwa yule wa kumfunua kikamilifu, pamoja na kuwa yule aliyeufanya upatanisho kati yake na wanadamu.
Ni kitu gani kitakachotusaidia kuupinga uzushi? taz. k.24-27 ni „neno kutoka mwanzo" lile neno la mashahidi wa kuona, ushuhuda wa Mitume. 2 Tim 3:1-7, 4:3. Neno lao ndilo la kutuongoza na kutawala imani yetu na maisha yetu, tunao urithi mzuri katika Maandiko. Mambo ya msingi hayabadiliki, na ushuhuda wa KiMitume ni wa kutegemewa.

Pasipo kukaa humo itakuwa rahisi kudanganywa na mafundisho mbalimbali. Roho ni Roho wa kweli. Tunapookolewa tumejaliwa „Neno" na „Roho" walinzi wazuri wa imani yetu.

2:28 - 4:6 Mkusanyiko wa vile vipimo vitatu

Katika sehemu hiyo Yohana amekusanya pamoja vipimo vyake vitatu. 2:28-3:10 Utii na kutenda haki; 3:11-18 upendo: na 4:1-6 imani ya kweli.
2:29 Mkristo ameelezwa kuwa yeye aliyezaliwa na Mungu, hapo nyuma ameelezwa kwa lugha ya kusema anamjua Mungu. Tena anaongeza maelezo kwa kusema kwamba Mkristo anakaa ndani ya Baba na Mwana. Kukaa ndani ya Kristo na ndani ya Baba na kutembea katika nuru kwawezekana kwa sababu ya Mungu kutuzaa. Tumeshirikishwa uzima wa Mungu na tabia yake na matokea ki-maisha ni hatufanyi dhambi 3:9, twafanya haki 2:29, twampenda ndugu yetu 3:10-14 na tunamwamini Kristo kuwa Mwana wa Mungu aliyezaliwa kuwa mwanadamu 5:1.

2:28-3:10 Kutenda haki

Uhakikisho wa sisi kuwa watoto wa Mungu ni kutenda haki. Anayeamini kwa dhati ya kuwa Yesu Kristo alikuja kweli na atakuja tena, kwake ni vigumu awe na uzoefu katika dhambi. Hatapenda kufanya dhambi na atasikia uvutano wa kutenda haki na kuwa mtakatifu, maana amezaliwa na Mungu. Wanostiki walisema mtu huzaliwa mara ya pili kwa kupitishwa kwenye ibada za siri zenye vitendo vya ajabu kama kunyunyiziwa damu ya fahali n.k.

3:1 Yohana anaustaajabia sana upendo wa Mungu jinsi ulivyo mwingi sana. Ni la ajabu tufanywe kuwa watoto wake, si kwa kupewa jina tu, bali zaidi sana tumefanywa kuwa, kwa neema yake. Ila ulimwengu hautuelewi hivyo - taz. Rumi 8:16-19, Kol 3:3, 1 Kor 2:15-16.

k.2 Tu „wana" sasa. Ya mbele Yohana anakiri „hatujui" isipokuwa neno moja analifahamu, nalo ni hilo „tutafanana na Kristo" Sura ya Mungu iliyoharibiwa na dhambi itarudishwa kwa ukamilifu, hatua kwa hatua kwa Roho Mtakatifu Efeso 4:24, Kol 3:10, 2 Kor 3:18, 1 Yoh 2:6.

Ni lengo la Mungu katika kututeua - Rumi 8:29, Fil 3:21, 1 Kor 15:49. Mwishoni tutakuwa PAMOJA NA KRISTO NA KUFANANA NA KRISTO. Licha ya kuwafundisha Wakristo Yohana alitaka kuwagusa maishani mwao. Kuwa na uhakika wa kujua tumefanywa kuwa watoto wa Mungu kunaleta wito na wajibu wa kutakasa maisha. Damu ya Kristo yatusafisha dhambi tulizozifanya ila pia ni wajibu wetu kujitakasa maana yake kupigana na dhambi na kuikataa.

3:4-10 Sehemu hii inaweka wazi kusudi la Kristo kuja duniani ambalo lilikuwa kuiondoa dhambi na kuziharibu kazi za Shetani. Hivyo kuendelea katika dhambi ni kubatilisha kusudi hilo, ni upinzani wa mapenzi yake.

k.4-7 Dhambi ni nini? Ni uasi wa sheria ya Mungu. Dhambi yenyewe ni uasi, ni hali yake si matokeo yake. Yesu hakufanya dhambi na zaidi alifanya haki, akiishi maisha matakatifu, alitafuta kumtii Baba kikamilifu katika yote. 2:29, 3:3,7. Maana ya maneno „Mkristo hatendi dhambi" ni hana uzoefu katika dhambi, si kawaida yake, hakusudii kuifanya. Kristo na dhambi havipatani kamwe, vilevile Mkristo na dhambi havipatani, ndiyo sababu Yohana anasema „atendaye dhambi ni wa Ibilisi". Dhambi na Shetani hupatana.

k.7 Kwa upendo sana Yohana anawasihi waumini „watoto wangu wadogo" ili wawe macho kwa waalimu wa uongo na mafundisho yao kusudi wasidanganywe nao. Wao walisema kwamba mtu aweza kuwa mwenye haki bila kutenda haki. Kwa Yohana kipimo cha kweli ni utendaji wa mtu si katika asemavyo na kudai.

k.8-10 Asili ya dhambi ni Shetani, na lengo lake ni kuvuta watu kutenda dhambi, yaani kumwasi Mungu, akiyapotosha mawazo yao. Yesu alimshinda, na ametushirikisha ushindi wake, na aliye ndani ya Kristo hawezi kuonewa na Shetani. „hatendi dhambi" „hawezi kutenda dhambi" Ndani ya mtu aliyezaliwa na Mungu imo mbegu ya kuichukia dhambi. Maneno hayo hayana maana kwamba kamwe hatatenda dhambi,la, ila ataichukia na kutafuta kuishinda. Linganisha maneno hayo na sura ya kwanza 8 -10. Tunapozaliwa na Mungu twashirikishwa tabia yake ya haki na utakatifu 1 Petro 1:23 na 2 Petro 1:4.

k. 10 Kwa hiyo tunajitambulisha kuwa wa Mungu au wa Shetani kwa kuishi kwetu.

3:11-18 Kipimo cha Upendo

Hapo Yohana anapambanua pendo na chuki, kujitoa na uuaji. Kaini ni mfano wa mtu aliye na hali ya dunia hii. Waalimu wa uongo walijivunia mafundisho yao kuwa mapya. Yohana alirudi kwa mafundisho ya asili, kweli za tangu mwanzo, zilizo muhimu kwa waumini wote, zinazoeleweka bila shida. Wanostiki walisema kweli zao ni za wachache tu, watu wa ki-pekee, wenye kujaliwa hiyo „nukta ya nuru" ya kutambua mambo ya siri.

Shetani alikuwa nyuma ya chuki ya Kaini, na kwa sababu ya chuki Kaini alimwua ndugu yake Yoh 8:44. Na kwa nini alifanya hivyo? ni kwa sababu alichukizwa na maisha ya haki ya Habili, akamwonea wivu. Sawasawa na makuhani na wakuu wakati wa Yesu. Uadui upo kati ya Wakristo na watu wa dunia hii Yoh. 15:18,19,25; 16:1 na 17:14. Katika kuwachukia Wakristo ulimwengu unajishuhudia hali yake ya „mauti" 1 Petro 4:12ku.

Upendo unathibitisha kuwepo kwa „uzima" na kiini cha upendo ni kujitoa.

k.16-18 „Sisi twapenda", ni ishara thabiti ya uzima wa milele, ni ushuhuda mzuri wa kuwa na huo uzima, na uhakika wa ukweli wa imani yetu 1 Kor 13, Gal 5:22. „asiyependa" yu gizani, ni wa mauti. Yohana ameweka pamoja „upendo" „nuru" na „uzima" na kwa upande wa pili „chuki" „giza" na "uuaji" - ukosefu wa upendo ni ishara ya mauti ya kiroho, na chuki ni kama uuaji.

Kujitoa ni kiini cha upendo.

k.16 Mwuaji humnyanganya mtu maisha yake na kufanya hiyo ni dhambi kubwa. Apendaye hutoa maisha yake Mwenyewe kwa ajili ya wengine, sawa na alivyofanya Kristo Mwenyewe, naye ndiye kielelezo chema kwetu.

k.17 Tusifikiri hayo yahusu mambo makubwa tu, la twapaswa kupenda kwa kujitoa kufanya madogo tu kama kuwashirikisha wengine wanaohitaji vitu mbalimbali. Ni juu ya kila muumini kufanya hivyo, Yohana atumia lugha ya „mmoja" „mtu akiwa .....kisha akamwona ndugu yake ....." Hatunao upendo wa Mungu ndani yetu kama tumeshindwa kumsaidia mhitaji. Pendo la Mungu lakaa ndani yetu, linafanya kazi ndani yetu, linatafuta kutokeza matunda maishani mwetu.

k.18 Matendo yetu yasema kwa nguvu kuliko maneno yetu.

3:19-24 Amani na ujasiri mbele za Mungu

Hapa Yohana ameacha hoja yake ili aseme machache kuhusu mioyo yetu ikituhukumu au haituhukumu. Kitu kitakachotusaidia ni Kweli.

k.19-20 Twahitaji msaada wa kuhakikishiwa tunaposikia hukumu moyoni. Hatuwezi kuitegemea dhamiri peke yake, maana inaweza kuhukumu vizuri au kwa kosa. Maneno „mbele yake" yanatuonyesha njia ya kupitia, kwa sababu tukiwa wa kweli tutapenda kujua kweli kwa kumwendea Baba na kupata maoni yake. Ni vema kuuchunguza moyo na kuona kama upendo wa kujitoa umo, maana hii ni dalili nzuri, kwa sababu upendo wa namna hii hautokani na utu wa asili bali kwa utu upya na tunda la upendo ni ujasiri. Yohana ametaja matatu:
(1) ni moyo wangu, ambao unanihukumu, (2) ni mimi mwenyewe nikijitetea (3) ni Mungu aliye hakimu wa kweli. Kwa hiyo ni vema tumtegemee Mungu na kuona kwake, na Yeye ni mwenye rehema pia Zab.103:14, Yoh 21:17. Ufahamu pia waweza kuutuliza moyo, sisi wenyewe tunatambua kama tunawapenda wengine kwelikweli, huku Mungu anazifahamu nia na sababu zinazotuongoza.

k.21-24 Baraka zinazopatikana kutokana na moyo usiohukumu ni ushirikiano mzuri na Mungu na maombi kujibiwa. Wajibu wetu ni kutii na kukaa ndani ya Kristo k.24. Roho anafanya kazi mioyoni mwetu na bila shaka ataendelea kutusaidia kila tunapohitaji msaada.

4:1-6 Uhakikishio wa Roho wa kweli

Yawezekana wasomaji wa waraka walielekea kuyakubali mafunzo yaliyotolewa katika hali ya uvuvio. Yohana aliwashauri wayachunguze na kupima asili yake. Yesu alisema „kwa matunda yao mtawatambua" Math 7:20. Yohana amekwisha kutoa vipimo vya maisha vya kutumiwa kwa kuupima ukweli wa imani ya mtu, kutazama matendo yake kama anatenda haki, na kupenda ndugu yake. Kipimo kingine chahusu „theologia" ya mtu, kama anamwamini Yesu Kristo kuwa Mwana wa Mungu aliyezaliwa kuwa mwanadamu kweli.

Mungu ametoa Roho Mtakatifu ila ziko roho zingine zifanyazo kazi ulimwenguni, hizo amfanya mtu kuamini yasiyo kweli - Yohana asema wazi „msiamini kila roho" bali tuzijaribu, yaani tuzipime. Nabii ni mtu aliye kama „mdomo" wa roho, ama Roho wa kweli au wa uongo, Roho wa Mungu au roho atokaye kwa Shetani. Kila muumini amejaliwa uwezo wa kuzitambua roho, na ni lazima tuzipime, maana „manabii wa uongo" wanayasambaza mafundisho yao ya uongo.

Tutazame ukiri, ukiri wa kweli ni kwamba Yesu Kristo amezaliwa kweli, wala si kukiri kwa akili tu, bali kwa kujitoa kuishi kufuatana na ukiri huo.

Wenye kumkana Yesu Kristo wasimkubali Kuwa Mungu Mwana hao waitwa wapinga Kristo. Hivyo kwa kukiri au kwa kukana twadhihirishwa kuwa na Roho Mtakatifu au sio. Katika 2:18-23 tulionyeshwa kuwa tunaye Baba au sivyo. Kristo ni msingi wa imani ya kweli.

k.4 „mmewashinda" kwa njia gani wameshinda? kwa sababu Mwovu hakufaulu kuwadanganya, na yeye hakufaulu kwa sababu walikuwa na Roho wa kweli aliyewalinda ki-imani.

k.5-6 Yohana alikuwa miongoni mwa Mitume na ni ujumbe wao unaosikilizwa na kupokelewa na watu wa Mungu, na ujumbe wao unakataliwa na ulimwengu. Wanaoupokea ni wale aliowataja Yesu „kondoo zangu waisikia sauti yangu"Yoh 10:4,5 na 18:37 na 8:47. Usalama unategemea uaminifu kwa ujumbe wa asili uliofundishwa kwanza na Mitume.

4:7-5:5 Kipimo cha Upendo

Kwa mara ya tatu Yohana anarudia kuzungumza kipimo cha upendo, na kila mara uzito unazidi. Upendo tupaswao umefungamana na tabia ya Mungu, Mungu ni pendo kwa hiyo kila atendalo ni katika pendo. Mara 3 amewasihi wawe na upendo wa kupendana-k.7 ni kama mwito wake - wawe na upendo;

k.11 amesema ni wajibu wao na k.12 amesema ni muhimu kupita yote, ni msingi hasa.

Katika Yesu Kristo Mungu amejifunua kuwa „upendo wa kujitoa" Mungu aliye Pendo, katika Kristo ametupenda upeo, na sasa anaendelea kupenda kwa njia ya waumini wake, kusudi tupendane sisi kwa sisi kwa pendo lake analomimina mioyoni mwetu. Yeye ni mwanzilizi wa upendo wote wa kweli, kwa hiyo wale wenye upendo wa kujitoa wamezaliwa na Mungu na kumjua. Hata katika kazi ya hukumu Mungu huhukumu kwa msingi wa pendo lake. Kwa pendo lake dhambi imedhihirika ilivyo hasa, na ajabu ni kwamba amepata njia ya kuiadhibu bila kummaliza mwenye dhambi. Kristo aweza kumwokoa mwenye dhambi badala ya kumwangamiza. Kwa kuwa Mungu ni pendo itafuata kwamba „asiyependa" hamjui, haidhuru huyo atasemaje na kudai anamjua. Upendo ni dalili sahihi ya kumtambua Mkristo wa kweli aliyezaliwa na Mungu.

k. 9-11 Pendo la Mungu si hali tu, linafanya kazi katika ulimwengu huu. Mungu kwa pendo lake alimtuma Kristo, ni tendo lisilokanushwa. Mara nyingi ameonyesha upendo wake kwa njia mbalimbali ila upeo ni katika kumtuma Kristo. Tena pendo lake halitegemei neno lo lote, halisababishwi na jambo lo lote ni tabia yake ya asili Mungu NI pendo. Pendo letu ni itikio kwa pendo lake. Hakuwa na kipawa cha thamani kuliko Mwana wake, wala hakuna tendo lo lote la upendo kuliko kumtoa 2 Kor 9:15, tena alimtoa kwa sisi wenye dhambi tusiostahili kamwe kupendwa kwa namna hiyo.

Kila aliyelionja pendo la msalabani katika kusamehewa dhambi hupaswa kupenda

k.12 Mungu anaendelea kupenda akitia pendo lake ndani yetu ili tuwe chombo chake akiwapenda watu kwa njia yetu. Awezaje Mungu kuonekana leo? Wawezaje watu kujua Mungu ni pendo na kulionja? Walio wake wamfunulie leo wanapopenda na kupendana. Ametupa Roho Mtakatifu atuwezeshe kupenda. Si kwamba tunapoanza kupendana ndipo Mungu hutia pendo lake ndani yetu, la sivyo, bali Mungu anatia pendo lake ndipo twaanza kupendana, na kwa jambo hilo ushuhuda kamili wa kumjua Mungu hutolewa.

Yohana amesema neno moja la ajabu sana, nalo ni hili, tunapopendana ndipo pendo la Mungu linakamilika, si pendo letu bali ni pendo lake linalokamilika. Pendo la Mungu laanzia ndani yake Mwenyewe 4:7-8; pendo la Mungu lilidhihirishwa kwa njia ya Kristo 4:9-10 na pendo la Mungu lakamilishwa kwa njia ya wafuasi wake 4:12. Kwa mambo hayo matatu Yohana anatusihi tupendane.

<u>Mungu kukaa ndani yetu</u>
Kipimo cha imani 4:13-16 chaunganishwa na kipimo cha upendo 17-21. Uwezekano wa kuamini kwamba Baba alimtuma Mwana, na uwezekano wa kumpenda Baba, na kupendana sisi kwa sisi watoka kwa Roho Mtakatifu.
k.13 „sisi ndani yake na Yeye ndani yetu"

k.15 „kila akiriye Yesu ni Mwana wa Mungu" Mungu hukaa .....na yeye ndani yake"
k.16 „akaaye katika pendo, hukaa ndani ya Mungu na Mungu hukaa ndani yake".

Tusitenganishe hayo matatu, Baba kumtuma Mwana, na Yesu kuwa Mwana wa Mungu, upendo wake kwetu na upendo wetu Kwake, na sisi kupendana. Ni mambo hayo yanayotufanya kuwa na uhakika, wa kukaa ndani ya Mungu na Mungu kukaa ndani yetu, kwa kuwa ametupa Roho wake
k.13. Ni Roho anayetusaidia kumtambua na kumkiri Yesu kuwa Mwana wa Mungu
k.15, pia Roho ndiye anayetusaidia kuamua kuishi kwa pendo
k.16. Kuamini na kuishi kwa pendo si masharti ya Mungu kukaa ndani yetu, la, bali ni ushuhuda wa mambo hayo „katika hili twafahamu".

4:17-21 Kukamilika kwa pendo
Tusifikiri kwamba hatutakuwa na upungufu na kosa au kasoro katika neno hilo, maana ya kukamilika ni tutaendelea kukua na kukomaa, kiasi cha mtu kuwa amekaza kumpenda Mungu.

k.17 Alama moja la pendo kamili ni mtu kuwa na ujasiri mbele za Mungu. Ujasiri umetajwa 2:28 3:21, 4:7 na 5:14,15. Ni kwa sababu tu watoto wake hatuisikii hofu juu ya siku ya hukumu, twaushiriki ujasiri wa Yesu aliokuwa nao mbele za Baba yake.

k.18 Pendo lizaalo ujasiri lafukuza hofu maana pendo na hofu havipatani. Twamkaribia Baba kwa pendo pamoja na kumcha Ebr 5:7, Rumi 8:14-15, 2 Tim 1:7. Pengine maana yake ni kwamba hofu huleta mawazo ya adhabu na kwa watoto wa Mungu waliosamehewa hawana haja ya kuwaza adhabu tena. Au pengine ina maana kwamba ni hofu yenyewe iliyo adhabu, kwa sababu anayehofu anateswa na hofu yake.

k.19 Alama kubwa ya Wakristo ni „twapenda" si „twahofu". Pendo letu ni itikio letu kwa pendo la Mungu lililotangulia, pendo limetoka kwa Mungu, hofu hutoka utu wetu wa asili.

k.20 Alama ya pili ya pendo kamili ni kumpenda ndugu. Pendo latupa nje chuki. Mkristo asiyeishi kwa pendo ni mwongo.

Waraka umetaja uongo tatu zilizo kubwa:

1. Tukisema tunamfahamu Mungu na kushirikiana naye, huku tunatembea gizani, wala hatumtii, basi tu waongo.
2. Tukidai tunaye Baba huku tunamkana Yesu kuwa Mungu Mwana, tu waongo.

3. Tukidai kuwa tunampenda Mungu, huku tunamchukia ndugu, tu waongo. Mambo hayo yahusu maisha yetu ya kiroho, maisha yetu ya ki-jamii, na kuamini kwetu.

k.20 Hata tukidai kwa nguvu kuwa Wakristo tukiwa na mwenendo katika dhambi na kumkana Kristo kuwa Mwana wa Mungu, tukiwa na chuki hali tunajipenda tu, basi tu waongo. Ni rahisi kumpenda jirani aliye karibu nasi kuliko yule asiyeonekana. k.21 Kumpenda Mungu na kumpenda jirani ni sehemu mbili katika amri moja. Ni Yesu aliyeunganisha maneno ya Kumb 6:4 na Lawi 19:18 na kufundisha kwamba torati na manabii yote yatimizwa na amri hii. Tukimpenda Mungu twazishika amri zake 2:5 na 5:3 na amri aliyotupa ni kumpenda jirani yetu kama nafsi yetu.

5:1-5 Mwungano wa vipimo vitatu

Kuhusu imani 5:1,4,5 -kuhusu upendo 5:1, 2, 3; na kutii na kushika amri 5:2, 3. Vipimo hivyo vitatu vyafanana na nyuzi tatu na waraka umefumwa na nyuzi hizo, zimeshikana na ni vigumu kuzifumua. Msingi ni katika mtu kuzaliwa na Mungu, aliyezaliwa na Mungu anazo hali hizo tatu.

k.1 Kama tulivyokishaona juu ya pendo, kuamini ni tukio la kuzaliwa na Mungu si asili wala sababu ya kuzaliwa.

k.2-3 Haiwezekani mtu ampende Mungu huku akikosa kuwapenda wengine hasa walio waumini wenzake. Tena haiwezekani mtu ampende Mungu na kukosa kuzishika amri zake. Twajidhihirika kwa matendo yanayoonekana. Wala tusihesabu neno la utii kuwa neno gumu, Yohana anasema „amri zake si nzito" hazifanani na zile za Mafarisayo zilizowalemea watu. Mapenzi ya Mungu ni mema kwetu Rumi 12:2 ni mapenzi ya Baba wa pendo amtafutaye mtoto wake mema na maisha bora. Pia Mungu hutupatia nguvu ya kuzishika Kol 1:13 na tunapozaliwa na Mungu uvutano mbaya katika utu wa kale umevunjwa na kunyonya nguvu yake.

k.4-5 Mara tatu Yohana anataja „kuushinda ulimwengu". Ni nani anayeushinda?" ni yule aliyezaliwa na Mungu na kuamini. Yawezekana Yohana anawawaza wasomaji wake ambao wameonyesha imani thabiti walipoyakataa mafundisho mengine yaliyozuka kati yao, wakiwakataa waalimu wa uongo. Walidumu katika shirika zao 4:4 kwa hiyo wameuonja ushindi wa imani yao. Yohana amechora duara: Wakristo wauminifu ni watoto wa Mungu, wamezaliwa na Mungu, watoto wa Mungu wanapendwa na wote wampendao Mungu; wampendao Mungu huzishika amri zake; wanazishika amri kwa sababu wameushinda ulimwengu; waushinda ulimwengu kwa sababu ni wauminifu kwa Mungu, maana wamezaliwa naye. Tunapozaliwa na Mungu uhusiano wetu na dunia wakatwa na twaungamanishwa na Mungu, na tokeo

lake ni tunazishika amri zake; kuamini na kutii, kuamini na kupenda - imani, upendo, utii.

5:6-17 Yohana anataja mashahidi matatu

Twawezaje kumwamini Yesu Kristo? Twahitaji ushahidi - shahidi la kwanza - Yesu Kristo ameelezwa kuwa „alikuja" katika „maji" na katika „damu" Ni vigumu kuelewa maana na lugha hiyo. Huenda ni lugha ya kukaza umoja wa maisha yake tangu kuzaliwa hadi kufa. Katika Unostiki wengine walifundisha kwamba Kristo alimshukia mtu fulani alipobatizwa au wakati mwingine na kumwacha tena kabla ya kusulibiwa. Yohana anataka kukaza kwamba yule aliyezaliwa ndiye yule aliyesulubiwa, na aliyezaliwa ni Kristo siyo mwingine.

Shahidi wa pili ni Roho Mtakatifu. Daima ni kazi ya Roho kumshuhudia Kristo. Yeye ni Roho wa kweli Yoh 15:26, 16:13. Hao wawili, Yesu Kristo aliyeonekana wazi hapa duniani, na Roho amshuhudiaye mioyoni mwetu 2:20,27 4:1-6, 3:24, 4:13. Maneno yaliyofungwa katika mraba hayaonekani katika nakala za zamani za kabla ya karne ya tano.

k.8 Roho, maji, damu, vitatu vinavyopatana katika ushuhuda, kwa sheria lazima mashahidi wawili au watatu wapatane Kumb 19:15.

k.9 Mungu Mwenyewe pia humshuhudia Mwanawe akiuunga mkono ushuhuda uliotangulia.
Alipokuwa hapa duniani Mungu alimshuhudia Yesu na tangu Pentekoste Roho ameendelea kumshuhudia. Ushuhuda wa Mungu ni mzito mno, wala haiwaziki tuukatae, hasa kwa sababu tunaupokea ushuhuda wa wanadamu mradi wawili au watatu wapatane.

k.10-12 Shabaha ya Mungu kumshuhudia Mwanawe ni kutusaidia tumwamini Kristo, kumwamini Kristo ni sawa na kumwamini Mungu, na Roho hutupa uhakika moyoni. Anayekataa kuamini si bahati mbaya bali ni dhambi kubwa ni kumfanya Mungu kuwa mwongo na kumpinga aliye kweli 1:10. Baraka ya kuamini ni kuwa na uzima wa milele, Uzima huo ni kipawa cha Mungu Yoh 17:3, umo katika Kristo, kwa hiyo yeye aliye nje ya Kristo hana huo uzima. Yesu Mwenyewe ndiye huo uzima 1 Yoh 1:2, Yoh 11:25, 14:6.
Matatu kuhusu uzima wa milele:

1. Ni kipawa tusichostahili
2. Kinapatikana katika Kristo
3. Ni kipawa twaweza kuwa nacho sasa Ling. Yoh 20:31.

Ni shabaha ya Injili ya Yohana na Waraka wake umejengwa juu ya shabaha iyo hiyo - „ili mjue mna uzima" na „kuwa na uhakika kuwa nao".

Ni wema tukumbuke ya kwamba Yohana anawapinga waalimu wa uongo waliowatilia mashaka wakristo. Kwa upande wake Yohana anataka wawe

thabiti katika imani yao, amewapa vipimo vya kuwasaidia kuipima imani yao vizuri. Tusifikiri mtu amekosa unyenyekevu akiwa na uhakika wa wokovu wake. Si vizuri kuwa na mashaka juu ya Neno la Mungu na ushuhuda wa Mungu ulio ndani yake.

k.14-15 Maombi kujibiwa: Aliye na uhakika amwomba Mungu kwa ujasiri, anajua atasikilizwa, kwa sababu ya ushirikiano uliopo. Kwa upande wetu tutaomba yale tunayofahamu ni mapenzi yake na kupatana na tabia yake, na Mungu atayajibu. Katika maombi tunajinyenyekeza na kutafuta mapenzi yake, maombi si njia ya kubadili mipango ya Mungu.

„atatusikia" na „tunazo zile haja" Kwa njia ya maombi muumini anawakumbuka wengine na haja zao kimwili na kiroho. Kama mmoja amenaswa katika dhambi fulani wenzake watamwombea. Juu ya dhambi kubwa, Yohana hasemi wazi kama wamwombee au siyo. ling. na Yer 7:16, 11:14, 14:11 Yeremia alikatazwa asiwaombee watu wa Yuda.

„dhambi ya mauti ni dhambi ipi?" Torati ilipambanua dhambi - zingine zilihesabiwa kuwa na adhabu ya mauti Lawi 20:1-27, Hes 18:22. Pia katika Agano la Kale tofauti iliwekwa kati ya dhambi za kujua na kutokujua Zab 19:13. Za kujua hazikuwa na msamaha. Mababa wa Kanisa kama Origen pia walitoa mafundisho ya kupambanua dhambi. Katika Agano Jipya jambo hilo si wazi sana. Huenda „dhambi ya mauti" ni uasi, yaani kumkana Kristo na kuondoka katika imani - taz. Ebr 6:4-6, 10:26, 12:16-17. Tukumbuke ya kwamba Yohana amekwishafundisha kwamba aliyezaliwa na Mungu hatendi dhambi. Wazo lingine dhambi hiyo huenda ni kumkufuru Roho Mtakatifu, kuupinga ukweli ulio wazi na kwenda kinyume cha ufahamu na dhamiri. Math 12:28, Mko 3:29, Yoh 3:18-21 na 8:24.

Kwa nini yaitwa „dhambi ya mauti" ni kwa sababu mwisho wake ni hasara ya kuukosa uzima wa milele, na kutengwa na Mungu aliye hai. Labda Yohana anawaza wale waalimu wa uongo, wasio waumini wa kweli 2:19.

5:18-21. Mambo matatu wanayoyajua

Hapo Yohana anatilia mkazo misingi ya waraka, mambo tuliyopaswa kuyajua kwa uhakika. (1) „Kila" aliyezaliwa na Mungu hatendi dhambi, bali anadumu kuwa mtoto wa Mungu, mwenye baraka mbalimbali, na mwenye wajibu mbalimbali. „hatendi dhambi" ndiyo kawaida ya maisha yake na mazoea yake. „hujilinda" 1 Tim 5:22, Yak 1:27, Yuda 21. Tafsiri nzuri ni „Yesu huwalinda". Tufahamu twahitaji kulindwa maana Shetani hapumziki katika kuleta majaribu.

k.19 Sisi ni wa Mungu aliye asili ya uzima wetu kiroho. Dunia yote hukaa katika „Mwovu" neno „hukaa" laleta picha ya ustarehe, wametulia kama mtoto mikononi mwa mamaye.

k.20 „Ila Mwana wa Mungu ameishi kuja", tayari amefanya kazi njema za neema, amemfunua Mungu Baba, na ametukomboa na dhambi zetu. Bila Yesu kamwe tusingemjua Mungu jinsi alivyo, wala kumjua kibinafsi, wala tusingeupata msamaha wa dhambi na kuishinda.
„Huyu ndiye Mungu wa kweli wa uzima wa milele" maneno hayo yaweza kumhusu Baba au Mwana au wote wawili Yoh 17:3.

k.21 Hatujui sababu ya Yohana kutaja „sanamu" kama neno la kuufunga waraka wake, bila shaka ipo hatari fulani kwa waumini ambayo hakuieleza zaidi.

WARAKA WA PILI WA YOHANA

Neno kuu la Waraka huu na wa Tatu ni juu ya kukaribisha wainjilisti na wakristo waliokwenda huko na huko kwa shughuli mbalimbali. Warumi walikuwa wametengeza barabara nyingi nzuri, na askari walizilinda nchi walizozitawala na mipaka yake, kva hiyo amani ilikuwepo, hivyo wengi walisafiri kwa ajili ya biashara n.k. Vivyo hivyo wakristo walijitoa kuihubiri Injili wakisaidiwa na baraka hizo za amani na usafiri mzuri. Tena pamoja na baraka hizo lugha ya Kiyunani ilifahamika mahali pengi, ikiwasaidia katika kazi yao ya kuieneza Habari Njema.

Ila tatizo moja lilikuwa „wakae wapi" „wakae na nani"? Nyumba za wageni hazikuwa na sifa njema, kwa hiyo iliwapasa wakristo wawe tayari kuwakaribisha. Ndiyo sababu mara nyingi katika nyaraka twaona shauri la kuwa wakarimu, wenye kukaribisha wageni. Taz. Mdo 16:16 Lidia alimkaribisha Paulo na wenzake; Mdo 17:7 Yasoni vilevile; Mnason Mdo 21:1,16; Gayo wa Korintho Rumi 16:23; na Filipo pale Kaisaria Mdo 21:8.

Lakini shida moja ipo, watawezaji kuwatambua kuwa wakristo wa kweli. Baadaye „ndugu" wa uongo waliwafikia hao wakristo na kuwalemea wakikaa muda mrefu, wakijifanya ni wakristo wa kweli. Katika ukarimu wao wakristo waliwalisha bure na kuwapa msaada wa kuendelea na safari. Wengine waliitumia njia hii ya kueneza mafundisho kinyume cha yale waliyopokea, wakitafuta faida yao.

Ni katika mazingira hayo nyaraka hizo ziliandikwa. Yohana anawaambia wakristo kwa nguvu juu ya nani wa kukaribishwa na ni nani wa kutokukaribishwa akitoa na sababu. Mtumishi wa kweli wa Kristo atatambulikana kwa ujumbe anaouleta na kwa tabia zake 2 Yoh 7 na 3 Yoh 6-7.

(Kuna andiko moja, laitwa „Didache" lililoandikwa kama mwisho wa karne ya kwanza, yadhaniwa katika Shamu, ambalo lazungumzia jambo hilo kwa kirefu na kuwashauri wakristo wayachunguze sana hali za wageni waliowafikia. Waangalie hali yao kwa kuhusu fedha, na muda wa kukaa, maelekeo yao ya kufanya kazi ili wapate riziki kama wakitaka kukaa zaidi, pamoja na mwenendo wao. Mwandishi aseme „aombaye fedha, na akaaye zaidi ya siku 2 au 3' ahesabiwe si wa kweli).
Andiko hilo laonyesha wazi kwamba jambo hilo lililisumbua Kanisa sana.

2 Yoh 1-3 Uhusiano wa ukweli na upendo kati ya Yohana na wao

Yohana amejitaja kwa neno „mzee" si kwa sababu ya umri wake tu bali kwa sababu ya heshima yake katika makanisa, wakristo walipenda kumwita „mzee". „mama mteule" Je! huyo ni mama fulani? Huenda siye! Pengine ni lugha ya

Yohana kwa kanisa fulani mahali fulani. Na kama ni hivyo „watoto wake" ni waumini wa pale k.4 na 13.
Sababu ya kufikiri hivyo ni lugha ya „upendo" ambayo yafaa kwa kundi kuliko mtu binafsi 1,2,5, ni vigumu kuweka „amri" kwa watu binafsi. Pia Yohana amechanganya lugha kwa „mmoja" na kwa „wengi" - taz. „wako" „nakuandikia" na „mlivyosikia" „msiyapoteze" „kwenu" „msimkaribishe" „ndugu yako mteule" pengine ni kanisa la jirani taz. 3 Yoh 9.
Tukilinganisha na Waraka wa Tatu ni mtu mmoja Gayo ambaye ameandikiwa na Yohana alitumia lugha ya „mmoja" tangu mwanzo hadi mwisho wa waraka.

k.1 Ni kitu gani kilichomhusianisha Yohana na kanisa hilo? Ni „kweli" za „Kristo" na kweli hizo ziliwatenga na waalimu wa uongo na kumfanya Yohana awe na mzigo wa kuwalinda wakristo hao kusudi wasipotoshwe katika imani ya kweli. Waipendao hiyo kweli wamefungana katika upendo.

k.2 Kwa nini Yohana alilipenda kanisa hilo? - ni kwa sababu „ya hiyo kweli" Wakristo wapaswa kuwapenda jirani zao hata na adui zao, ila kifungo kinachowafungamanisha wakristo wao kwa wao ni „kweli". Yohana amekaza sana neno „kweli" amelitumia mara nne katika vifungo vitatu vya kwanza. Sisi wakristo tunapendana si kwa sababu tunaafikiana mambo fulani au kwa sababu kuna uvutano fulani au damu zinasikilizana, la, sivyo, bali ni „kweli tunazozishiriki" zinazotufunga pamoja. Kweli hizo zamhusu Kristo, nazo zatuongoza mpaka uzima wa milele. Na kweli hizo zadumu kuwepo potelea mbali wengine wataziacha. Ni hatari kabisa kuzipunguza kwa ajili ya kupatana. Umoja hauna budi kujengwa juu ya kweli na bila msingi wa kweli hautakuwepo umoja wa kweli na kupendana kwa kweli.

k.3 Salaam za waraka huu zafanana na nyaraka za Paulo ila tofauti ipo. „Rehema" imeingizwa kama ilivyoingizwa katika Nyaraka za Timotheo na Tito. Kristo ameitwa „Mwana wa Baba" na mkazo ni Yesu kuwa sawa na Baba katika hali ya kuwa chemchemi zitokazo baraka za neema, rehema na amani. Shirika la wakristo laundwa kwa watu kuiamini kweli ya Kristo ndipo kujiunga pamoja na kuionyesha kwa kuishi kwa upendo. Katika pendo „utambuzi" uwepo wa kupambanua wasio na mafundisho ya kweli na wanaoishi kinyume cha mwenendo wa Kikristo.

k.5 na 7-11 Vifungo hivi vinatoa shauri la kutokuwakaribisha waalimu wa uongo, amewaita „wadanganyifu" na „wapinga Kristo". Kwa hiyo mawili yanakwenda pamoja „kweli" na „pendo" - kweli isikose kuwa na pendo na pendo lisikose kuwa na kweli, Maandiko yanatuamuru kupendana katika kweli na kushika kweli katika pendo.

k.4 Anawasifu waliodumu kuwa wauminifu kwa kweli, akiwasihi waishike amri ya kupendana.

k.8 Wajihadhari sana na wale wanaotafuta kuwanasa kwa mafundisho mengine akiwashauri wasiwasaidie kwa jambo lo lote maana wakiwasaidia watakuwa wanaishiriki kazi yao mbovu.

k.4. Katika shirika hilo mengi yalimfurahisha „mzee" ila alisikitika kwa sababu ya wale wasioenenda katika kweli. Si kweli fulani za kushikwa kwa kichwa, bali kweli za kuishi kwazo. Kuiacha kweli ni jambo la „kutokutii" au kuasi maana „amri ya Baba" ni kuenenda katika kweli. Kweli imetoka kwa Mungu, ni ufunuo juu yake, twapaswa kuishika na kuifuata kikamilifu, wala si kama tuamuavyo wenyewe.

k.5. Ila Baba anayo amri nyingine pamoja na hiyo ya kuenenda katika kweli, nayo ni „kupendana". Kuwa Mkristo ni kumwamini Kristo na kupendana 1 Yoh 3:23, Kol 1:4, 2 Tim 1:3. Tukimkana Mwana au tukikosa kupendana hatuna Mungu wala hatumjui 1 Yoh 2:23, 4:8. Imani na upendo ni ishara za kuzaliwa na Mungu 1 Yoh 5:1, 4:7. Ni amri si shauri. Kuamini ni itikio letu la utii kwa Ufunuo wa Mungu katika Yesu Kristo. Kutokutii ni dhambi Yoh 16:8,9, 3:18.

k.6 Upendo na utii vinaingiliana na kuwiana Yoh l4:15,21, 15:10, 1 Yoh 5:2-3, Rumi 13:8, Math 22:40, kwa hiyo pendo na sheria vinawiana, havipingani. Katika sehemu hiyo Yohana anaeleza maisha ya Kikristo kwa kusema juu ya amri, neno „amri" ametumia mara nne, taz.k.3,4.6a, 6b. Uhuru alio nao Mkristo haupingi „sheria" wala „upendo". Mkristo hauwi chini ya sheria kwa kuupatia wokovu, hata hivyo aliyeokoka hakuachishwa kabisa mbali ya sheria, bali wajibu wake kutokana na wokovu wake ni kushika sheria - taz. Math 5:17-20, Rumi 8:4, 13:10. Uhuru wetu si wa kuvunja torati bali wa kuishika, uhuru umetupatia uwezekano wa kuishika Zab. 119:45.

k.7-11 Jinsi ya kuwakabili waalimu uongo

Yohana anao mzigo, hataki waalimu wa uongo wafaulu kuwadanganya wakristo. Anasema wametokea wengi wenye shabaha ya kuwadanganya. Anawaita wapinga Kristo kwa sababu wanaukana ukweli wa Yesu kuwa Mwana wa Mungu. Anawashauri mawili (a) wajihadhari 8-9 na (b) wasiwasaidie kwa kuwakaribisha na kuwapa riziki n.k. 10-11. Yesu Mwenyewe aliwaonya mitume kwamba watainuka watu wa aina kiyo, na sasa wametokea MKo 13:22- 23 Baba yao, yaani Shetani, amewatuma kuueneza uongo na kuwapinga Wakristo ambao wametumwa kuieneza kweli. Walijitoa kwenda huko na huko wakijaribu kupenya shirika za Wakristo. Huenda baadhi yao walifikiri ni watumishi wa Kristo, wasijitambue wamekuwa wadanganyaji. Uongo wao, hawamkiri Yesu Kristo kuwa amekuja katika mwili 1 Yoh 4:2.

k.8 Yohana aliona kuna ujanja katika uongo wao basi lazima wakristo wajihadhari ili wasipoteze walioyatenda kusudi wapate thawabu timilifu. Hapo

nyuma wamemtumikia Kristo basi utumishi huo usiwe bure. Wakidumu katika imani waliyo nayo watapata thawabu.

k.9 „apitaye cheo" inaonekana wazushi walijidai kuwa na maendeleo kimafundisho na kuzidi katika ujuzi wao, kiasi cha kuyatupa mafundisho ya kwanza waliyoyapata wasikae nayo. Yohana anaona kweli kwamba „wameendelea mbele" lakini kumbe wamemwacha Mungu nyuma!!! Haiwezekani kuzikana kweli za msingi kumhusu Kristo na kubaki kuwa na Mungu 1 Yoh 2:22-23. Hakuna awezaye kuwa na Baba bila kumkiri Mwana, kwa sababu Mwana ni ufunuo halisi wa Baba Yoh 1:18, 14:7,9, 1 Yoh 5:20, Math 11:27. Pamoja na hayo Mwana ni njia ambaye kwaye twaweza kumfikia Baba Yoh 14:6, 1 Tim 2:5. Wengi wanamtaka Mungu bila kuwa na Yesu Kristo, wala haiwezekani. Hakuna mafundisho ya „maendeleo" zaidi ya Agano Jipya, maendeleo tunayohitaji ni katika kulifahamu na kulifuata.

k.10 Yohana anatoa mwongozo wa namna ya kumkabili mwalimu wa uongo. Asikaribishwe nyumbani, na „msimpe salamu" maana yake kumtakia heri ya safari. Anapofika mahali fulani, asikaribishwe, na anapoondoka asipewe heri. Ni wajibu wa Wakristo kuwakaribisha wageni - Rum 12:13, 1 Tim 3:2, 5:3-10, Tito 1:8, Ebr 13:2, 1 Petro 4:8-10, 3 Yoh 5-8.
Shauri la kutokuwakaribisha ni baada ya kusema juu ya kupendana. Mtu akija katika hali ya kuwa mwalimu tena analeta mafundisho ya uongo, ni kama mtembezi wa mafundisho hayo, ni huyo ambaye asikaribishwe kwa sababu shughuli zake hazikubaliani na Injili. Pengine maana yake ni asipewe nafasi katika shirika kama kuhubiri katika ibada n.k. Huenda Yohana alifahamu wengine wako njiani wakikusudia kuwafikia wanaoandikiwa. Tena ni wale wanaomkana Kristo. Haina maana kwamba tusimpokee ye yote anayeachana
nasi kwa mambo fulani. Wanaozungumziwa amewaita „wapinga Kristo" na ni hao ambao twapaswa kutokushirikiana nao.
Tukifikiri Yohana amekuwa mkali sana tujue ya kwamba alikuwa na mzigo sana juu ya Utukufu na Sifa za Bwana Yesu na juu ya usalama wa roho za watu. Mafundisho yanaweza kumpeleka mtu Mbinguni kama ni kweli au Jehanum kama si ya kweli, twapaswa kuwa na mzigo juu ya mafundisho yanayotolewa.

k.12-13 Taraja la kuja kwao

Yohana ana mengi ya kuwaambia ila anapenda kusema nao uso kwa uso maana ni njia bora, ni rahisi kueleza maana kwa sababu sauti na uso zasaidia kuleta maelewano. Kwa hiyo anatarajia kuwafikia, shabaha yake wote wapate kufurahi pamoja. Agano Jipya lina habari ya furaha ya kweli ipatikanayo, kwa kushirikiana sisi kwa sisi na katika ushirikiano mwema wa Baba na Mwana 1Yoh 1:3-4.

k.13 ni salaam za wakristo wa kanisa lingine pale Yohana alipokuwepo wakati wa kuandika.

WARAKA WA TATU WA YOHANA

Katika waraka huu neno linalozungumzwa ni lile lile la waraka wa pili, kuhusu waalimu wa uongo kutembelea makanisa. Vilevile mkazo ni uleule wa kweli na pendo. Tofauti ni kwamba barua hii ni kwa mtu mmoja, Gayo, yawezekana alikuwa kiongozi wa kanisa fulani. Pamoja naye wakristo wawili wametajwa, Diotrefe k.9 na Demetrio k.12. Gayo amesifiwa kwa sababa amewakaribisha waalimu wa kweli na Yohana anamsihi aendelee kufanya hivyo. Diotrefe amekemewa sana maana hakuwakaribisha wageni, hata amewapinga pia amewazuia waliotaka kuwakaribisha. Kwa hiyo barua hiyo inafafanulia vizuri juu ya wajibu wa kukaribisha wageni na „mpaka" wake.

k.1-8 Ujumbe kwa Gayo

Hatujui Gayo huyo alikuwa nani, jina ni la wengi, kuna Gayo wa Korintho 1 Kor 1:14, Rumi 16:23; na Gayo wa Makedonia Mdo 19:29; na Gayo wa Derbe Mdo 20:4. Wengine wamewaza kvamba aweza kuwa Gayo wa Derbe ambaye kuwa mapokeo ya kusema aliteuliwa na Yohana kuwa Askofu wa kwanza wa kanisa la Pergamo na ni yeye aliyeandikiwa. Hatujui kwa hakika. Ameonekana kuwa na wajibu mkubwa katika kanisa la pale alipoishi, wainjilisti waliotembelea makanisa walizoea kukaa naye. Ni vigumu kuona kwa nini Yohana alimwandikia kama hakuwa na madaraka fulani, hasa aliposema kwa nguvu juu ya Diotrefe.

k.1 Anaitwa „mpenzi" taz 2,5,11. Alimpenda kva ajili ya kweli, pengine aliokolewa kwa huduma ya Yohana k.4. alimtakia mafanikio mema kimwili na kiroho, alifurahi sana kwa maendeleo yake ki-roho

k.3. Alikuwa amepata habari za Gayo kwa ndugu waliokuwa kwake na kuishuhudia tabia yake. Yohana ametaja mambo mawili ya sifa „anaenenda katika kweli" k.3 na „katika pendo" k.6.

k.4 Yohana anamwita „mtoto wake" hata na waumini pia, akijihesabu kuwa baba yao kiroho, ndiyo sababu alifurahiwa sana na hali zao kiroho - ling. 1 Thes 3:1-10. Gayo alikuwa mkarimu

5-6a. aliwakaribisha wageni akipenda kuwasaidia, na Bwana Yesu alifundisha kwamba kumkaribisha amwaminiye ni sawa na kumkaribisha Yeye Mwenyewe Math 10:40ff, 25:35,38. Amefanya kwa uaminifu na imeitwa „kazi" kwa sababu ilitokana na imani yake.
6b. Kuhusu mambo ya mbele, huenda Diotrefe atafaulu kumshawishi aliache tendo hilo la ukaribishaji, maana picha ya Diotrefe ni ya mtu anayejitahidi kuwazuia waumini wasikaribishe wageni. Yohana anamshauri Gayo aendelee kuwapokea hata na kuwasaidia kwa cho chote watakachohitaji wakati wa

kuondoka na kwenda mahali pengine. Wamestahili msaada kva sababu wanamtumikia Mungu.

k.7 Hao wanaokuja ni watu wa pekee, kwa sababu wameondoka kwao kwa ajili ya Bwana Yesu, ni vema wasaidiwe na wakristo wenzao kuliko wasioamini. Si kwamba wasipokee cho chote kwa wasioamini, ila tazamio lao hasa liwe kwa wakristo si kwa wasioamini.

k.8 Ni haki yao kukaribishwa maana hawana msaada nje ya huo. Wanaowasaidia huwa washiriki katika kazi yao njema ya kuieneza Injili.

k.9-11 Diotrefe

Yeye alitofautiana sana na Gayo kwa tabia ya ukaribishaji. Alijipenda sana, alikataa kabisa kuwapokea wageni, tena aliwazuia kwa nguvu waliokuwa tayari. Jambo hilo limeiva hata kwa Yohana kuliandikia kanisa ila hatunayo barua hiyo kwenye Biblia. Yawezekana Diotrefe alikataa kuisoma kwa waumini, hatujui, ila tujualo ni hilo hakulikubali shauri la Mzee Yohana akipinga mamlaka ya Ki-mitume aliyokuwa nayo Yohana, akijichukulia madaraka ya kuwatenga wengine. Hasa shida yake ilikuwa nini? ilikuwa alipenda kuwa „wa kwanza".

k.10 Yohana ameandika vazi kwamba akija atakemea kwa wazi matendo yake mabaya na maneno yake, maana asili yake ni „yule mbaya". Alikuwa na mambo matatu hasa (a) maneno ya upuzi juu ya Yohana, Gayo na wengine (b) kukataa mamlaka ya Yohana na shauri lake jema (a) aliwakataza waumini wa mahali pale wasilifuate shauri la Yohana, akiwatenga waliolifuata. Hawakupenda wale wageni walioyatembelea makanisa kwa ajili ya Yesu, alitaka atukuzwe yeye si hao.

k.11 Inaonekana Yohana anaogopa kwamba atafaulu kumvuta Gayo ndipo maisha yake kiroho yatapoa.

k.12 Demetrio

Huenda ni yeye aliyemletea Gayo barua hii. Anamweleza ni nani, kwa hiyo inaonekana Gayo hamfahamu, ili Gayo asiwe na mashaka juu yake. Demetrio ana sifa 3 (a) ameshuhudiwa na waumini wote kuwa Mkristo wa kweli (b) hali yake imemshuhudia kuwa wa kweli (c) Yohana mwenyewe anamfahamu Kwa hiyo Gayo aweza kuipokea ripoti hiyo juu yake bila wasiwasi.

k.13-15 Kuufunga Waraka na Salaam

Anatazamia kumfikia Gayo karibuni hivi na kusema mengi naye. „amani kwako" ni neno la maana kama Gayo anaongoza kanisa huku Diotrefe anawachochea watu. Anataka kila mkristo apate salaam zake ki-binafsi kwa jina lake.

(MAD0ND00 KUTOKA ANDIKO LA DIDACHE) „mtume asikae zaidi ya siku 1 ila kama ni lazima ndipo akae siku 2. Akikaa siku 3 ni mtume wa uongo. Anapoondoka apewe chakula cha kutosha kwa safari yake. Akiomba fedha ni mwongo. Kama nabii anadai anatoa unabii kwa Roho ndipo akiomba fedha au kitu kwa watu, wasimwamini, isipokuwa ameomba kwa ajili ya wahitaji. Manabii wa kweli wanaweza kukaa kama ni wa kweli. Mkristo anayesafiri asilishwe bure zaidi ya siku 2 au 3. Akipenda kukaa zaidi afanye kazi na kujitegemea kwa riziki zake. Akikataa ihesabiwe kamba anatumia jina la Kuwa Mkristo kama njia ya kuishi bila kufanya kazi)"

MASWALI MATATU

Moja kuhusu dhambi
Moja kuhusu kweli
Moja kuhusu pendo.

1. Je! katika makanisa yetu ya leo watu wasema nini kuhusu dhambi ?
Je! wako watu wasemao kwamba Mungu ni pendo kwa hiyo hawezi kutuadhibu kwa dhambi zetu, atasamehe tu?
Je! wako watu wasemao kwamba tu wanadamu dhaifu kwa hiyo haiwezekani tuishi maisha ya kushinda dhambi?
Je! wako watu wasemao kwamba upo uwezekano va kuishi bila kufanya dhambi?
Jibu la Yohana kwa watu kama hao ni nini?
Jumlisha mafundisho ya Yohana kuhusu dhambi.

2. Je! ni kiburi kuwa na uhakika wa kuwa na imani ya kweli na uzima wa milele?
Je! Yohana alitaka wakristo wawe na uhakika? Toa vifungu na lugha ya kuthibitisha jibu lake.

Je! kwa nyaraka hizo twajifunza imani na dini zote ni sawa au vipi?
Je! ni vizuri kuwa na mzigo juu ya kweli ya Injili? Je! tufanyaje tunapokabili imani zingine?

3. Je! Kwa nini Pendo ni kitu kikubwa katika maisha ya Mkristo?
Je! ni dalili ya nini hasa?
Je! Mungu atawezaje kuonyesha Pendo lake na kuendelea kupenda siku hizi?

Itakuwa vizuri msomaji akijaribu kuandika kwa kifupi msaada ambao ameupata kwa maisha yake kutokana na kuzisoma na kuzichunguza nyaraka hizo za Yohana.

WARAKA WA YUDA

YALIYOMO

UTANGULIZI

a) Mwandishi
b) Mahali pa Kuandikwa kwa Waraka
c) Walioandikiwa Waraka
d) Tarehe ya kuandikwa kwa Waraka
e) Sababu za kuandikwa kwa Waraka
f) Uhusiano wa Waraka na Waraka wa pili wa Petro

YALIYOMO

1 - 2 Salaam
3 - 4 Mwito wa Kuishikilia Imani ya kweli
5 - 7 Ukumbusho wa hukumu za Mungu za hapo nyuma
8 -13 Dhambi za ndugu wa uongo
14 -16 Faida ya unabii wa Henoko
17 -23 Maneno ya Mitume na maisha yawapasayo
24 -25 Kuwakabidhi kwa Mungu na Sifa kuu kwa Mungu.

UTANGULIZI

(a) Mwandishi

Katika kifungu cha kwanza mwandishi amejieleza kuwa Yuda, ndugu yake Yakobo. Huyo ndugu Yakobo ni yupi maana katika Agano Jipya wametajwa Yakobo mbalimbali; kuna:-

(1) Yakobo, mwana wa Zebedayo, ndugu wa Yohana, aliyeitwa na Yesu awe miongoni mwa Mitume 12;
(2) Yakobo wa Alfayo (Mt.10:3) yeye pia alikuwa miongoni mwa Mitume 12;
(3) Yakobo Mdogo, mwana wa Mariamu (Mk.15:40). Huyo amedhaniwa kuwa Yakobo wa Alfayo;
(4) Yakobo, baba wa Mtume Yuda, (si Yuda Iskariote) (Lk.6:16; Mdo.1:13) Katika Mt.10:3 na Mk.3:18 ameitwa Thadayo.
(5) Yakobo, Ndugu wa Bwana Yesu (Mt.13:55)
(6) Yakobo, mwandishi wa Waraka wa Yakobo (Yak.1:1)

Katika hao wote wako wawili tu waliotajwa pamoja na Yuda kwa ukaribu. Mmoja ni Yakobo, baba wa Mtume Yuda. Katika Luka 6:16 (orodha ya Mitume waliochaguliwa na Yesu) „Yuda wa Yakobo" ametajwa. Kwa kawaida kuandika hivi ina maana ya kuwa „mwana wa.." si „ndugu wa.." Aliyebaki ni Yakobo,

ndugu wa Bwana Yesu, hivyo, mwandishi Yuda alikuwa ndugu wa Bwana Yesu (Mat.13:55; Mk.6:3)

Mwandishi hakudai kuwa Mtume wala hakuandika kwa mamlaka ya KiMitume. Alijitofautisha na Mitume (k.17). Yeye, sawa na ndugu yake Yakobo aliyeandika Waraka wa Yakobo, hakusema juu ya kuwa ndugu wa damu wa Bwana Yesu. Wote wawili walijiita „watumwa wa Bwana Yesu" wakishuhudia utayari wao wa kumtumikia „ndugu yao" Yesu kwa uaminifu na utii.

Sababu nyingine inayoongoza watu kuwaza huyo Yakobo kuwa ndugu wa Bwana Yesu ni kwamba Yuda amemtaja bila mapambo yoyote, dalili ya kuonyesha kwamba alijulikana sana katika Kanisa. Kumtaja tu kulitosha kwa watu kutambua ni nani, na Yuda mwenyewe alikuwa radhi ajulikane kama „ndugu wa Yakobo" yaani ndugu wa kiongozi maarufu mwanzoni wa Kanisa pale Yerusalemu (Mdo.12:17; 15:13). Alimwamini Kristo baada ya Kufufuka Kwake (1 Kor.15:7).

(b) Mahali pa Kuandikwa kwa Waraka

Wengi wafikiri kwamba Waraka uliandikwa sehemu za Palestina, pengine Antiokia wa Shamu. Waraka unataja sana mambo ya Agano la Kale. Pia Yuda amedondoa mengine kutoka maandishi ya Kiyahudi. Ndiyo sababu ya kufikiri hivyo.

(c) Walioandikiwa Waraka

Mwandishi hakutaja mahali walipoishi. Alituma salaam kwa „hao walioitwa, waliopendwa katika Mungu Baba, na kuhifadhiwa kwa ajili ya Yesu Kristo". Maneno hayo yahusu Wakristo wa mahali pote, ila ni wazi kwamba alikuwa akiwaandikia watu aliowajua na kufahamu hali zao na mazingara yao na yanayotokea kwao (Taz.k.3-5; 17-18, 20).

(d) Tarehe ya kuandikwa kwa Waraka

Mafundisho ya uongo yaliyotajwa yalizuka katika makanisa karne ya kwanza. Pia tumaini kuu la Kurudi kwa Bwana lilikuwa na nguvu katika siku za kwanza za Kanisa. Hasa k.18 chaonyesha kwamba wengi walioandikiwa walikuwa wamewasikia Mitume, hivyo Waraka uliandikwa kabla ya wengi wao kufariki dunia. Pia Yakobo ametajwa bila mapambo. Yeye aliuawa kama B.K.62 na ni vigumu kufikiri angalitajwa hivyo bila kumwita Yakobo Mwema au Yakobo Mbarikiwa, au kuongeza neno fulani.

(e) Sababu ya Kuandikwa kwa Waraka

Kutokana na k.3 Yuda alikusudia kuwaandikia hao watu Waraka juu ya „wokovu ambao ni wetu sisi sote". Lakini alipopata habari ya watu fulani kujiingiza kwa siri katika shirika, watu wenye kusudi la kuleta mafundisho

mapotovu, basi aliona vema kuwaandikia Waraka kwa shabaha ya kuwaonya sana juu ya hao watu na mafundisho yao. Alitoboa wazi yaliyomo katika uzushi wao. Hivyo Yuda aliacha shabaha yake ya kwanza ya kuwaandikia kuhusu wokovu na kuwaandikia kwa nguvu sana juu wa hao walioingia kwao akiwasihi waumini wa kweli wasimame imara katika imani waliyoipokea (k.3b).

(f) Uhusiano wa Waraka wa Yuda na Waraka wa Pili wa Petro

Sehemu kubwa ya Waraka wa Yuda imeonekana katika Waraka wa Pili wa Petro. Yuda. 4-16 yaonekana katika 2 Petro 2. Swali ni Je! Waraka wa Yuda ulitangulia Waraka wa Pili wa Petro na Petro alikopa kwa Yuda? au Waraka wa Petro ulitangulia na Yuda alikopa kwa Petro? Ni vigumu kujua kwa hakika, maana kila wazo lina mambo ya kulisimamia. Hata baadhi ya wataalamu wamewaza kwamba pengine lilikuwapo andiko lingine lililotumiwa na Kanisa la kuwasaidia waumini kuyapinga mafundisho ya uongo, na hasa mafundisho yaliyozuka mahali pengi kuhusu uhuru wa Kikristo. Wengine walidai kwamba Kristo amewaweka uhuru, nao wameokolewa bure kwa neema ya Mungu, hivyo si kitu jinsi waishivyo. Paulo alikutana na mafundisho hayo na kuyapinga sana hasa katika Waraka kwa Warumi na Waraka kwa Wagalatia. Iwapo katika sehemu hiyo vifungu vingi vimefanana maneno yaliyotumika yametofautiana, kwa hiyo, hawakukopa moja kwa moja, kila mmoja alitilia mkazo kulingana na shabaha yake.

UFAFANUZI

k.1-2 Salaam

Salaam zilifuata kawaida ya siku zile. Kwanza mwandishi alijitaja, ndipo walioandikiwa, halafu salaam zenyewe. Mwandishi alijitaja kuwa Yuda, ndugu yake Yakobo. Katika utangulizi jambo hilo limezungumzwa, na imeonekana Yuda, ndugu wa yule Yakobo aliyeandika Waraka wa Yakobo, ndiye mwandishi. Huyo Yakobo amefikiriwa kuwa ndugu wa Bwana Yesu, kwa hiyo Yuda pia alikuwa ndugu wa Bwana Yesu, na majina yao yameonekana katika orodha ya ndugu zake Bwana Yesu (Mk.6:3; Mt.13:55).

Yuda alijieleza kuwa „mtumwa wa Yesu Kristo" hakutaja undugu wake na Yesu wala hakujiinua kwa sababu hiyo. Alikuwa radhi kujiita „mtumwa" wa Yesu Kristo, na kumpa utiifu na kuwa mwaminifu kwake. Wala hakudai kuwa Mtume, wala hakudai mamlaka ya KiMitume kwa Waraka.

Hakusema mahali walipoishi wasomaji wake, ila ni wazi walikuwa Wakristo wa mahali fulani, maana aliwafahamu, na kujua yaliyokuwa yakitokea kwao (k.4; k.17-18).

Aliwaeleza kuwa „walioitwa, waliopendwa katika Mungu Baba, na kuhifadhiwa kwa ajili ya Yesu Kristo". Walikuwa wameitika mwito wa Injili wa kutubu na

kumwamini Yesu Kristo. Jambo la kuitwa lilikuwa muhimu na kutajwa mara nyingi katika Agano Jipya. Wameitwa kwa karamu ya Arusi ya Mwana Kondoo (Mt.22:3; Ufu.19:9) Wameitwa watoke gizani na kuingia kwenye Nuru ya ajabu ya Mungu (1 Pet.2:9) Wameitwa kumtumikia Bwana Yesu aliyewaokoa na baadaye wataitwa kutoa hesabu ya utumishi wao (Lk.19:13,15). Wameitwa kuishi maisha matakatifu kwa kuwa aliyewaita ni Mtakatifu.

„Kupendwa katika Mungu Baba" Ni hapa tu katika Agano Jipya maneno „katika Mungu Baba" yametumika. Kwa kawaida waumini wameelezwa kuwa „katika Kristo" na „katika Bwana". Huenda Yuda aliacha nafasi baada ya neno „katika" kwa mahali fulani kuingizwa na mjumbe aliyekwenda na nakala za Waraka. Hivyo kifungu kingalisomwa „kwa hao katika .....(mahali) wanaopendwa na Mungu Baba. Mungu alionyesha upendo wake katika kumtuma Kristo awakomboe ndipo akawaita waje Kwake. Wamefanywa kuwa „wana" nao wameingizwa katika familia ya Mungu.

Pia ni watu waliohifadhiwa kwa ajili ya Yesu Kristo. Wako chini ya himaya yake Mungu, wamelindwa na nguvu zake. Wamelindwa na yule mwovu tayari kwa Kuja Kwake Kristo na kwa Ufalme utakaosimamishwa Atakapokuja (Yn.6:39,44,45; 1 Kor.1:8; 1 The.5:23; 2 Tim.1:12; 1 Yoh.5:l8). Mungu hataki kumpoteza hata mmoja wa wale aliowaita. Yuda alikaza jambo hilo kwa sababu shabaha yake katika kuwaandikia ilikuwa kuwaonya juu ya hatari ya wale watu waliojiingiza kwao kwa siri na kuleta mafundisho ya kuwapotosha. Haja yao kubwa ni kulindwa wasinaswe na hao watu na mafundisho yao. Mungu katika kuwapenda na kuwahifadhi ataendelea kufanya kazi ndani yao na kati yao.

Aliwatakia nini? Alitaka waongezewe baraka kubwa za Injili, rehema, amani, na upendano. Ni kwa rehema zake Mungu aliwaokoa wanadamu kwa njia ya Yesu Kristo. Kwa ukombozi wa Kristo wameletwa katika uhusiano mwema na Mungu na kuonja amani mioyoni mwao, matokeo ya dhambi zao kusamehewa. Halafu wameingizwa katika familia ya Mungu, na kitu kikubwa katika familia hiyo ni upendo, kila mmoja kumpenda mwenzake, na jumuiya yote kupumua „hewa" ya upendo, na wote kuishi katika Pendo la Mungu. Yote hayo ni kipawa cha Mungu, hayatokani na bidii zao. Alitaka wawe na mambo hayo tele. Mungu azidi kuwahurumia hasa kwa ajili ya hatari iliyowakabili, wajaliwe neema na uwezo wa kutosha. Twajua wakati wa shida ni rahisi amani itoweke, lakini Yuda alitaka wazidi kujua amani, ushirikiano wao na Mungu uendelee na ushirikiano wao kwa wao uzidi kuwa na nguvu, hasa wakati wa imani yao kutikiswa na hao waliojiingiza kwao. Zaidi ya yote walihitaji kuongezewa upendo, upendo kwa Mungu, wasimlaumu kwa ajili ya shida iliyopo, pia wazidi kupendana wao kwa wao, ili ushirika wao usipenywe na hao watu. Wakishikana wao kwa wao kwa nguvu na kumshikilia Mungu basi watapita salama katika mashambulio. Ombi hilo lawafaa Wakristo wakati wote na wa mahali pote.

k.3-4 Mwito wa kuishikilia Imani ya Kweli

Yuda alianza na neno „wapenzi" (alilitumia tena k.17,k.20) akitoa sababu ya kuwaandikia (2 Pet.3:1,8,14,17). Neno hilo linaonyesha upendo aliokuwa nao kwao, upendo wa kweli, maana hakusita kuwaonya juu ya watu kadha walioingia kwao. Bila shaka hakupenda kuandika barua nzito na kali, lakini aliona imemlazimu awatahadharishe.

Alikuwa amekusudia kuwaandikia Waraka, pengine alikuwa ameuanza ila aliposikia habari za hao watu kuingia kati yao waliokusudia kuyaingiza mafundisho yasiyopatana na kweli ya Injili, basi, alibadili shabaha ya kwanza ya kuwaandikia juu ya „wokovu ulio wetu sisi sote" ili awaonye juu ya hatari ya hao watu na mafundisho yao na kuwashauri mambo yatakayowasaidia kupambana nao. Hivyo, badala ya kuwaandikia kwa upole na kwa utaratibu ilimbidi afanye haraka na kuwaandikia kwa uzito na ukali.

Alitaka wafanye nini? k.3b „mwaishindanie imani waliyokabidhiwa watakatifu mara moja tu". Yuda amewaza „Imani" ni kweli za Imani ambazo Mitume walizihubiri na kuzifundisha na kuzikabidhi kwa waumini ili na wao wazikabidhi kwa wale watakaoamini baadaye (Mdo.2:42; 1 Kor.1-4; 2 The.3:6). Yuda alionyesha kwamba yalikuwepo mafundisho ya Kikristo ambayo yalikubalika na kuwekwa kuwa msingi ambayo yaliwapasa waumini wote kuyashika na kuyafuata. Aliongeza maneno „mara moja tu" kwa kuonyesha upekee wa mafundisho hayo. Ilihesabiwa kosa kufuata mafundisho mengine yaliyozuka mara kwa mara katika shirika za Kikristo.

„watakatifu" ni watu wa Mungu, yaani, waumini wote. Imani ya Kikristo ina mizizi katika historia ya Yesu kufanyika mwili na kwa njia ya Kristo Mungu alisema na wanadamu. Kwa hiyo ushuhuda wa wale waliomwona na kumsikia Yesu ulikuwa muhimu kabisa katika kumjua Kristo (2 Yoh.9). Maendeleo si katika kuongeza mafundisho yenyewe bali ni katika kuwa mwaminifu kwake (1 Tim.6:20; 2 Tim.1:13-14). Ni juu ya kila kizazi kuyatafsiri kwa wakati na mazingara yake.

Neno „mwaishindanie" lilitumika kwa mashindano ya michezo. Kwa kulitumia neno hilo Yuda alitaka kuwajulisha wasomaji wake kwamba walihitaji kuwa na bidii katika kuishindania hiyo Imani. Budi wakaze nia zao. Wawe tayari kudhihakiwa na kufikiriwa kuwa „watu wa zamani" watu wasiotaka maendeleo. Pia waieleze Imani kwa lugha iliyofahamika na watu, na kuitafsiri ili iwe na maana kwa mazingara na wakati wao na kwa maisha yao. Imani ni kweli zilizokabidhiwa, hizo hazibadiliki, hata hivyo ni kweli zilizo hai zisemazo na kugusa maisha yao na uhusiano wao na Yesu Hai.

k.4. Yuda alitumia lugha kali alipoeleza tabia za hao watu. Kwanza alisema walijiingiza kwa siri, wakiificha shabaha yao na kwa werevu walijifanya kuwa Wakristo wazuri lakini sio. Yuda aliwaita „makafiri" watu wasiomcha Mungu,

waliomkana Mungu kwa jinsi walivyoishi. Halafu alisema „wabadilio neema ya Mungu wetu kuwa ufisadi" maana yake hawakumjali Mungu wala amri zake. Walifundisha kwamba kuokolewa kwa neema kumewaweka uhuru, na kwa sababu hiyo wataishi kwa jinsi walivyopenda wenyewe. Walifurahia msamaha bila kukubali wajibu wa kuishi maisha safi. Mafundisho ya aina hiyo yalienea sana katika makanisa, na Paulo alisema sana juu yake (Rum.6 na 7). Walijiinua na kujiamuria mambo yao ndiyo sababu Yuda alisema kwamba walimkana Bwana wao Yesu Kristo na Mungu Baba. Hawakukubali mamlaka ya Kristo katika maisha yao. Tena walijitoa kabisa kufanya ufisadi (Tito.1:16; 2 Pet.2:1, 1 Yoh.2:22; 2 Pet.2:18-19; 1 Kor.6:9ku; 1 Yoh.3:7ku. Ufu.2:24).

k.5-7 Ukumbusho wa hukumu za Mungu za hapo nyuma

Yuda, kama Petro alivyofanya katika Waraka wake, aliwakumbusha yaliyotokea zamani za kali, akionyesha kwamba, potelea mbali wadai kuwa Wakristo, neno la maana si madai yao bali ni maisha yao. Mfano wa kwanza uliwahusu Watu wa Mungu waliotolewa Misri kwa mkono hodari wa Mungu, walionja nguvu zake na kuyaona maajabu yake, hasa katika kuvuka Bahari ya Shamu, hata hivyo wengi wao waliangamizwa jangwani kwa kutokuamini na kuasi kwao, wakakosa kuingia nchi ya ahadi (1 Kor.10:1ku. Ebr.3:12ku). Hata na hao watu waliojiingiza kwao hawataiepa hukumu ya Mungu. Kwa kutumia habari ya Waisraeli inaonekana hao watu walikuwa Wakristo wa kweli waliorudi nyuma.

Ukumbusho wa pili ulihusu malaika walioasi na kuanguka. Hawakuridhika na mahali pao pa juu. Huenda Yuda alikuwa akiwaza habari iliyoandikwa katika Mwanzo 6:1-4 (2 Pet.2:4). Malaika, mahali pao ni mbinguni, isipokuwa wanapotumwa na ujumbe fulani hapo duniani, lakini inaonekana walijaribu kuweka makao yao hapa duniani hali wakitamani wanawake. Hawakuwa waaminifu katika wajibu waliopewa wa kulinda mambo ya thamani sana, hivyo Mungu aliwatoa mbinguni na kuwafunga gizani mpaka siku ya mwisho ya hukumu (2 Pet.2:4). Hali yao ya sasa ya giza ni mbaya mno kulingana na hali yao ya kwanza walipoishi katika nuru kuu ya Mungu. Kiburi kimetajwa kuwa shida yao (Isa.14:12; 24:21-22) na tamaa (Mwa.6:4).

Halafu mfano wa tatu alioutumia Yuda katika kuwatahadharisha wasomaji wake juu ya wale watu walioingia kwao ni habari ya Sodoma na Gomora (Mwa.19:1-25; 2 Pet.2:6). Maangamizo ya miji hiyo yalikaa sana katika mawazo ya watu kizazi baada ya kizazi yakiwa ishara ya hukumu ya Mungu. Kwa nini miji hiyo iliangamizwa? Sababu ilikuwa uasherati wa wenyeji. Walijitoa kwa maisha machafu katika kufanya mambo ya mwili kinyume cha kawaida, wanaume waliacha wanawake na kukaribiana wao kwa wao (Rum.1:26-27). Huenda Yuda alikuwa akisema juu ya wenyeji waliotaka kuchukua wale wageni wawili waliomjia Lutu, ambao walikuwa malaika, iwapo hawakujua ni malaika (Mwa.19:1,5). Katika Mwanzo 6 malaika waliwajia

wanawake wa dunia, na katika Mwanzo 19 wanaume wa dunia waliwajia malaika!!

Iwapo mambo hayo yalitokea zamani ni onyo lidumulo kwa wakati wote na kwa vizazi vyote. Wakati wa Yuda yalikuwa onyo kali kwa wale waliojiingiza kwa siri katika shirika zao.

k.8-13 Dhambi za ndugu wa uongo

Yuda aliacha habari za zamani za kale na kusema juu ya tabia na maisha mabovu ya wale walioingia kwa siri. Iwapo hukumu kali ziliwapata waasi wa zamani, hao watu walithubutu kufuata vielelezo vyao vibaya. Hawakujifunza lolote kwa hukumu za Mungu katika historia iliyotangulia.

Aliwashtaki mambo matatu:"walitia mwili uchafu (uasherati) walikataa mamlaka (uasi) na waliyatukana matukufu (ufidhuli). „katika kuota kwao" pengine walidai wamepata mafundisho yao kwa njia ya maono. Walifanya uasherati mbaya kabisa na kuwafundisha wengine kufanya vivyohivyo (2 Pet.2:2,10,18; 1 Kor.5:1; 6:9; 2 Kor.12:21). Walikataa mamlaka ya Mungu (k.4) na walisema vibaya juu ya malaika. Yuda aliwatofautisha na Mikaeli, malaika mkuu, na jinsi alivyofanya alipotumwa kumzika Musa (Dan.12:1; 1 The.4:16; Ufu.12:7; Kum.34:5-6) Ibilisi alimpinga akimdai Musa kuwa wake kwa sababu ya Musa kufanya dhambi ya uaji (Kut.2:12) pia, mwili wake ulikuwa wa dunia hii, kwa hiyo Musa ni mali yake. Iwapo Mikaeli hakukubaliana naye, hakuthubutu kumkemea uso kwa uso, ila alimwachia Mungu amkemee. Habari hiyo imeandikwa katika Kitabu kiitwacho “Kupaa kwa Musa” (“The Assumption of Moses”). Yuda alitumia Kitabu kingine kisicho katika Biblia kiitwacho “Kitabu cha Henoko” (“Enoch”). (Kwa sababu Yuda alitumia madondoo kutoka vitabu hivi baadhi ya wataalamu walisita kuukubali Waraka huo uwekwe katika orodha ya Vitabu vya Kanuni vya Agano Jipya).

k.10. Yuda aliona shida ya hao watu ni upungufu wa kiroho (k.19; 1 Kor.2:7- 11). Hali wamejibana katika mambo ya dunia hii wametawaliwa na tamaa za mwili sawa na wanyama wasio na hali ya kiroho mwishowe watajiharibu. Kujumlisha: waliharibika kimwili (uasherati) waliharibika kiakili (kiburi) waliharibika kiroho (uasi wa Bwana).

k.11-13. Katika vifungu hivi viwili Yuda aliangalia habari za watu watatu wabaya waliotajwa katika Agano la Kale. Ndipo akatupa macho yake juu ya maumbile ili apate mifano ya kufuliza hoja yake juu ya ubaya wa watu hao.

Katika watu wa Agano la Kale aliwachagua Kaini, Balaamu, na Kora. Alianza na neno zito „ole" neno la hukumu/sikitiko/au mchanganyiko wa hukumu na sikitiko. Ole hiyo iliwahusu wale watu waliokuwa wameingia kwa hila katika shirika za Kikristo. Hasa alitaka kuwathibitishia kwamba mwisho wao utakuwa mbaya sana sawa na miisho ya Kaini na wenzake.

„walifuata njia ya Kaini" Kaini alikuwa mwuaji wa kwanza katika historia ya wanadamu. Walifuataje njia ya Kaini? Kama Kaini alivyomwua ndugu yake ndivyo na hao wafanyavyo wakizi"ua" roho za waumini wenzao. Kaini hakumpenda ndugu yake Habili wala Mungu. Alimwonea wivu kwa sababu matendo ya Habili yalikuwa mazuri na yake yalikuwa mabaya (Mwa.4:4,5,9; 1 Yoh.3:12). Mwandishi wa Waraka kwa Waebrania alimwona Kaini kuwa kielelezo cha kutokuamini, mtu wa dunia, aliyemdharau Mungu na ndugu yake (Ebr.11:4). Na hao watu ndivyo walivyo.

„kosa la Balaamu" (Hes.22-24) Balaamu alikuwa mchoyo aliyetafuta faida iwapo mwanzoni alikataa kulipwa au kupokea rushwa (Hes.22:7-18). Pia ni yeye aliyewashawishi Waisraeli kuzini na wanawake wa Moabu, ndipo hao wanawake waliwavuta Waisraeli kuabudu miungu yao (mabaali) na kwa njia hiyo walimwasi Mungu kwa kuivunja amri ya kwanza „usiwe na miungu mingine ila Mimi" (Kut.20:3; Hes.25:1-9; Kum.23:4). Mara tatu Baalamu alishindwa kuwalaani Waisraeli, bila shaka aliwaambia kwamba hata wakifanya nini, hata kuzini, Mungu hatawahukumu. Hivyo aliwashawishi kuzini. Katika mapokeo ya Kiyahudi Balaamu alihesabiwa kuwa mbaya sana (Ufu.2:14). Kumbe! hao waliowajia ni sawa na Balaamu, wakipenda mapato (k.16) wakifundisha watu kuzini, eti Mungu husamehe dhambi bure, nao wameokolewa kwa neema si sheria, kwa hiyo, Mungu hatajali jinsi waishivyo!!!
Katika Nyaraka za Kiuchungaji Paulo alisema sana juu ya watumishi wa Kanisa waliojitafutia faida (1 Tim.6:5; Tit.1:11).

Halafu Yuda alimtaja Kora (Hes.16). Huyo aliwaasi Musa na Haruni, viongozi waliowekwa na Mungu kuwaongoza Waisraeli watoke Misri na kuingia nchi ya Kanaani. Kora alijikusanyia kwake kundi la watu na kuwafundisha kuwaasi viongozi wao. Alijiinua na kufanya ibada tofauti na zile zilizowekwa, na kufanya mambo ambayo hayakuwa halali ayafanye. Hakutaka kumtii Mungu wala viongozi waliowekwa na Mungu. Mwishowe aliangamia vibaya (Hes.16:31-32). Yuda aliona kwamba hao walioingia kwa siri katika shirika za Kikristo walifanana na Kora na wenzake. Hawakutaka kuwa chini ya wengine, walipenda kujiamuria mambo yao. Katika Agano Jipya twaona Kanisa lilisumbuliwa na watu wa namna hiyo (Tito.1:10,11; 3:10,11; 1 Tim.1:20; 2 Tim.3:1-9; 3 Yoh.9,10).

Kwa kujumlisha, dhambi za hao watu watatu zilikuwa wivu na ukosefu wa upendo kwa Mungu na wanadamu; choyo na utayari wa kufundisha watu ya kuwa dhambi si kitu, na kutafuta mapato; kiburi cha kujiinua na kujichukulia madaraka na kuukataa uongozi wa uhalali uliopo.

Ndipo Yuda aliendelea na malaumu yake makali kwa kutumia mifano kutoka maumbile.

k.12. „miamba yenye hatari" hao watu wamefanana na miamba isiyoonekana, iliyofichwa chini majini, lakini hatari ni kwamba miamba inaweza kuvunja merikebu. Hao watu walikuwa na uwezo wa kuharibu imani ya Wakristo wa kweli. Hasa Yuda aliona kwamba walipata nafasi wakati wa karamu za upendo. Hizo karamu zilifanyika katika shirika za Kikristo. Watu walizoea kukutana kabla ya Ushirika Mtakatifu na kushirikiana kwa kula pamoja. Kila mmoja alileta chakula kiasi alichoweza, wengine kama watumwa hawakuweza kuleta chochote, na maskini walileta kidogo tu, ila ilitazamiwa kwamba wote wataonyesha upendo wao kwa wao kwa kushirikishana vyakula pamoja. Tena ilitazamiwa watashirikiana bila kubagua na bila kujifanya vikundi. Ndipo baada ya kula pamoja wakafanya ibada ya Chakula cha Bwana. Lakini shida ilitokea. Wengine hawakushirikisha vyakula vyao, wengine walijifanya vikundi na kula pamoja na kuacha wengine peke yao. Baadhi yao wachache walitumia kwa nafasi ya kuuvuta usikivu wa wanawake (1 Kor.11:20ku. 2 Pet.2:13-14). Kwa hiyo hao watu waliosemwa na Yuda walichukua nafasi ya karamu hizo kuendeleza shabaha yao ya kuwapoteza Wakristo „wakijilisha pasipo hofu". Walijipenda na kuangalia mahitaji yao na kwa anasa kufanya karamu kuwa sherehe, walijilisha tu (Eze.34:8).

„mawingu yasiyo na maji yachukuliwayo na upepo" hao watu walionekana kana kwamba wanaleta baraka, kumbe siyo. Hawakuwa imara, walichukuliwa huko na huko na kila upepo uliovuma. Badala ya kuleta mvua kwenye nchi kavu hawakuleta hata tone la maji. Waliwadanganya watu na madai ya kuwa na ufunuo wa elimu mpya ya kiroho, lakini mafundisho yao hayakuleta maburudiko yoyote katika maisha ya wasikilizaji.

„miti iliyopututika, isiyo na matunda, iliyokufa mara mbili, na kung"olewa kabisa". Hawakuzaa matunda katika maisha yao wala katika maisha ya wasikilizaji (Mt.7:15-20; Mk.11:12-14; Luk.13:6-9; 2 Pet.1:8, 3:18). Huenda maana ya kufa mara mbili ni kwamba walikuwa „wafu" katika dhambi (sawa na sisi sote Efe.2:1). Walihuishwa katika Kristo, ndipo wakafa tena kwa sababu walijitenga na Kristo, mzabibu hai wa kweli (Kol.2:7; Ebr.6:4ku. 10:26ku; 2 Pet.2:20ku). Katika Agano la Kale „kung"olewa" ni ishara ya hukumu ya Mungu (Zab.52:5; Mit.2:22). Kwa mfano huo mwandishi Yuda amekaza tena upungufu wao na ukosefu wa kuzaa matunda.

k.13. „mawimbi ya bahari yasiyozuilika, yakitoa aibu yao wenyewe kama povu". Ni picha ya kutokulia kwao, hawakuwa na utaratibu, walifanana na misukosuko ya bahari ambayo hufanya povu na kutupa takataka kwenye pwani - „povu" ni dalili ya aibu yao, matokeo ya dhambi zao.

„ni nyota zipoteazo, ambao weusi wa giza ndio akiba yao waliowekewa milele". Inaonekana Yuda amepata mawazo hayo kutoka Kitabu cha Henoko. Walifanana na viongozi vipofu waliosemwa na Yesu (Lk.6:39). Huenda Yuda

aliwaza nyota, kimwondo, zitokeazo kwa ghafula na kuvuka mbinguni halafu huanguka chini. Hao watu walidai kwamba mafundisho yao huwatia watu nuru lakini kweli yenyewe ni kwamba wao wenyewe wamo gizani, wamepotea na kuondoka katika njia na hukumu yao ni „weusi wa giza" (2 Pet.4:17). Katika Kitabu cha Henoko malaika waliomwasi Mungu walipoteza nafasi ya kukaa mbinguni, wakawekwa kifungoni kwenye giza kuu. Henoko, mtu wa kweli, alitofautiana nao, yeye alifika mbinguni kwa sababu alimtii Mungu. Wasafiri, hasa mabaharia, wategemea nyota kuwaongoza katika safari, wakipata kujua walipo kutokana na mahali pa nyota. Lakini hao watu hawana msimamo, hawawezi kutegemewa kuwaonyesha watu njia itakayowafikisha kwa Mungu.

Kwa hiyo, katika vifungu hivi viwili Yuda amechora picha ya ajabu kuhusu hao watu. Ni wa hatari sana mfano wa miamba iliyofichwa chini majini, ni wa kujipenda kama wachungaji wasiostahili kuitwa wachungaji, hali wakijilisha badala ya kuwalisha kondoo zao. Wanadanganya watu, wakiahidi baraka, bila kuleta hata tone la maji, sawa na mawingu yasiyo na maji. Wamekufa kama miti isiyozaa, kisha ikang'olewa. Ni wachafu kama bahari inayofanya povu na kuacha takataka kwenye pwani. Hakika wamewekewa hukumu ya milele sawa na malaika walioanguka.

k.14-16 Faida ya Unabii wa Henoko

Yuda alitilia mkazo maneno yake makali kwa kuutimia unabii wa Henoko. Yuda alisema Henoko alikuwa mtu wa 7 kutoka Adamu (Mwa.5:3-24; 1 Nya.1:1-3; Lk.3:27). Kwa Wayahudi numbari 7 ilikuwa muhimu yenye maana „ukamilifu/utimilifu". Watu walivutwa kusikia Yuda atasema nini kuhusu Henoko, kwa sababu alikuwa „wa saba kutoka Adamu".

Hayo maneno ya Henoko hayapatikani katika Biblia, ni madondoo kutoka Kitabu cha Henoko (1 Henoko 1:9). Henoko alisema nini? Alisema “Bwana alikuja pamoja na watakatifu wake maelfuelfu ili afanye hukumu na kuwaadhibisha waasi wote”. Yuda aliona maneno hayo ya Henoko yalihusu Kurudi kwa Bwana Yesu na hukumu atakayoifanya atakapokuja tena. Hao watu walikuwa tofauti na Henoko ambaye Biblia yasema “alitembea na Mungu,...akatoweka, kwa kuwa Mungu alimtwaa”. Alimtii Mungu kwa ukamilifu, akatembea na Mungu kwa ukaribu, kisha Mungu akamtwaa. Kifo chake hakutajwa. Kwa hiyo, wapokezi wa barua hiyo ya Yuda walitiwa moyo wa kumtii Mungu na kutembea na Mungu kwa ukaribu. Wasipofanya hivyo walionywa juu ya mwisho wao kuwa mbaya (Mwa.5:22-24). Twaona maneno „wasiomcha Mungu" yametumiwa mara kwa mara. Katika Biblia jambo la hukumu latajwa kuwa jambo la uhakika kabisa.

Yuda aliendelea kueleza hao waasi na tabia zao. Moja ni kunung'unika, ilikuwa vigumu kuwapendeza, hawakuridhika na hali zao. Walikuwa watu wa malalamiko. Pia waliendeshwa na tamaa zisizotulizwa. Pia walikosa katika

matumizi ya maneno, wakinena makubwa kwa kiburi. Tena tabia nyingine ilikuwa kujipendekeza kwa wakuu, kwa kuwapaka mafuta, n.k. ili wapate faida. Wakristo wameitwa wasiwe watu wa kunung'unika wala kulalamika, wala wasiwe na upendeleo wa watu, na waseme kwa hekima ya kuyapima maneno yao. Kiburi kilihesabiwa ni kinyume kabisa (Flp.2:14; Yak.2:1ku; 3:11,16; 4:6,11).

k.17-23 Maneno ya Mitume na Maisha yawapasayo

Baada ya kuutumia unabii wa Henoko, Yuda aliendelea kwa kutaja Mitume wa Bwana Yesu na maneno yao. Wakristo walioandikiwa walipaswa wayakumbuke maneno yao iwapo waalimu wa uongo walikuwa wameamua kutokuyajali. Yuda alivuta usikivu wao kwa kutumia tena neno „wapenzi". Sehemu kubwa ya Waraka imesema juu ya walioishi vibaya na kuleta mafundisho mabovu. Ilimbidi Yuda atoe maonyo mengi kwa Wakristo ili wasaidiwe kupambana na hao. Yuda aliwaonyesha kwamba hata Mitume walisema sana juu ya mambo hayo kuwa ni mambo ya kutazamiwa yatakayotokea katika maisha ya Kanisa mara kwa mara. (Mdo.20:29-30; 1 Tim.4:1-3; 2 Tim.3:1ku. 2 Pet.3:3). Katika Waraka wa Petro tuliona dhihaka za watu zilihusu neno la Kurudi tena kwa Bwana. Yuda hakutoboa wazi dhihaka za hao watu walioingia katika shirika zilihusu mambo gani. Pengine waliwacheka wale waliokataa kujiunga nao na kufuata njia zao mbaya.

k.19: Kwa dharau Yuda aliwataja “watu hao” kama alivyofanya katika k.12 na k.16. Ndipo aliwageukia walioandikiwa na kusema “bali ninyi wapenzi” (k.17,19).

Je! Yuda alisema nini zaidi kuhusu „watu hao"?. Neno lingine lilifunua hali yao nyingine. Ni watu „waletao matengano" watu wa dunia hii tu, wasio na Roho". Walijiinua na kujiona kuwa bora kuliko Wakristo wengine, kana kwamba wamefunuliwa neno la ajabu, ila neno lenyewe lilikuwa la upotevu. Lilihusu „uhuru" - uhuru wa kufanya wapendayo tu. Uhuru wa kweli ni „uhuru wa kufanya wapasayo". Yesu ametuweka uhuru, amezivunja pingu za dhambi zetu, ili tuweze kufanya yale mema yaliyotushinda wakati tulipokuwa tungali „wafungwa" wa dhambi. Wamefanana na Mafarisayo, wakati wa Bwana Yesu, waliojisifu hali yao ya kidini ya kufunga na kutoa zaka n.k. lakini Bwana Yesu alisema mioyo yao ilikuwa mbali na Mungu.

Hali yao ya kujiona ilionekana kwa jinsi walivyohudhuria karamu za upendo na kujifanya kundi, wakizungumza wao kwa wao, bila kuwajali wengine, wakiwahesabu hao wengine kuwa Wakristo dhaifu (k.12). Inaonekana waliwadharau viongozi wa shirika hasa ikiwa hao viongozi hawakuwa na elimu iliyolingana na yao (k.8). Pia walijiunga na matajiri kama ni wakuu wenzao (k.16). Walijaa kiburi, waliona kwamba „wamehitimu" mambo ya kiroho na kiakili. Bwana Yesu aliona kwamba Mafarisayo walikuwa watu waliojitenga na

wenzao, lakini kwa hali hiyo walishuhudia kwamba walikuwa wameachana na Mungu. Pengine walidai kujazwa na Roho, na kwa sababu hiyo waliona hawakuhitaji kujitia chini ya uongozi wa wengine, wala kufuata barabara kanuni za Wakristo wenzao. Yuda alisema wazi „hawana Roho".

k.20: Yuda alitumia tena neno „wapenzi", akiendelea kusema na Wakristo wa kweli na kuwashauri wajijenge katika imani yao, washirikiane na wasaidiane. Wafanye nini ili wajijenge? hasa wayazingatie Maandiko na kudumu katika maombi. (Ebr.5:12; 2 Tim.2:15). Halafu Yuda alisema „imani yenu iliyo takatifu sana". Imani yao ni ya tofauti sana na dini nyingine, kwa kuwa ni ufunuo kutoka Mungu Mtakatifu, hivyo itikio la kufaa kwa wito wa Mungu ni kuwa watakatifu, Si imani ya kuchezewa, bali ni imani ya kushikwa sana na kufuatwa kwa uaminifu katika kuishi maisha safi kila siku. Pia aliwashauri waombe katika Roho Mtakatifu, maana yake, wamtegemee uongozi wa Roho Mtakatifu katika maombi, ili waombe kulingana na mapenzi ya Mungu si matakwa yao ya binafsi (1 The. 5:11; 1 Pet.2:5).

k.21: „jilindeni katika upendo wa Mungu" ni juu yao kuona ya kuwa wanaendelea kuuitikia upendo wa Mungu, kwa kuwa, Mungu daima huendelea kuwapenda. Yawezekana Yuda aliongozwa kusema hayo kwa kuwaza hao wengine ambao walipendwa na Mungu na kuujua upendo wake kisha wakamwasi. Ni hekima kufanya juu chini kujilinda katika upendo wa Mungu kwa sababu mwisho wa hayo yote ni uzima wa milele. Huo uzima ni matimizo ya kudumu katika imani. Yuda alipenda sana kutaja rehema za Mungu, wokovu ulianzia katika rehema za Mungu, na tunahitaji rehema yake kila siku, na mwishowe kabisa katika Siku ya Hukumu sote tutaihitaji (2 Tim.1:18).

k.22-23: Kisha Yuda aliwashauri jinsi ya kuwafanyia wale ambao wameguswa hata kunaswa na wale walioleta mafundisho mabovu. Baadhi waliguswa kiasi bila kunaswa kabisa, „walio na shaka". Iliwapasa kuwahurumia hao, kuzungumza na kuhojiana nao ili wapate kuutambua ubovu wa mafundisho yaliyoletwa na hao watu na hatari ya kujiunga nao katika maisha yaliyopotoka. Ndipo wengine walikuwa wamepokea hao watu na mafundisho yao. Hao wamo „motoni" maana yake wamo katika hatari ya kupotea. Hivyo mazungumzo hayatawasaidia, iliyohitajika ni kuwakabili kwa nguvu na kuwashika na kuwanyakua mikononi mwa hao watu. Huenda walikuwako wengine waliokuwa tayari kushawishiwa na hao watu, kwa hiyo ni vema kuwahurumia ila wajihadharini wasije wakaguswa wenyewe na kunaswa katika dhambi zao. Wawahurumie wenye dhambi ila kamwe wasiibembeleze dhambi. Huenda Yuda alikumbuka maneno ya manabii (Zek.3:2-3; Amo.4:11; Isa.61:10). Ni vema kukumbuka ya kwamba tunapojaribu kuwasaidia watu walioteleza katika maisha yao ya kiroho twapaswa kuichukia dhambi zao huku tunawapenda watu wenyewe.

k.24-25 Kuwakabidhi kwa Mungu na Sifa Kuu kwa Mungu

Yuda alifunga Waraka kwa kuwakabidhi kwa Yule mwenye uwezo wa kuwalinda. Ni baraka iliyolingana na hali na mazingara yao na haja yao kubwa, maana walihitaji sana ulinzi wa Mungu ili wasimame imara na kuitetea imani ya kweli, ile waliyoletewa, ambayo ni ileile iliyoanzia kwa Mitume, mashahidi wa kweli wa Bwana Yesu.

Katika k.21 aliwaambia „jilindeni katika upendo wa Mungu" neno lililotumika na Yuda lilikuwa na maana ya „kuwa macho". Maneno ya Bwana Yesu alipokaribia kuwaacha wanafunzi wake lilikuwa „kaeni katika pendo langu, mkizishika amri zangu mtakaa katika pendo langu" (Yn.15:9,10). Hapo neno kuhusu ulinzi wa Mungu ni neno tofauti, ni neno lenye maana ya kulinda. Kwa hiyo tukiweka pamoja maneno hayo mawili Yuda alisema wawe macho, wakae karibu na Bwana kwa sababu ni Yeye peke yake aliye na uwezo wa kuwalinda wasije wakajikwae. Hawana haja ya kusikitika au ya kukata tamaa, kwa kuwa Mungu wao ni mwenye uwezo wa kuwalinda, tena zaidi ya kuwalinda aweza kuwasimamisha mbele zake katika utukufu wake wa ajabu. Hivyo, wapaswa kumtegemea huku wao wenyewe wanakesha juu ya imani yao. Kwa hiyo Yuda aliwatazamisha tena wayawaze yale mazuri yaliyo mbele yao mwisho wa maisha ya hapa duniani. Mungu atafurahi, nao watafurahi sana, katika Siku ile kuu ya mwisho. Kwa wakati huo wamo hatarini, wamo shidani, wamekutana na magumu, wapaswa waishindanie imani ya kweli na kupambana na wapinzani wake, ila wasisahau kwamba baadaye watafika mbele za Mungu Mtukufu kwa furaha kuu. Ajabu ni kwamba watafika mbele zake „bila mawaa". Lugha hiyo inakumbusha dhabihu za wanyama zilizotolewa hapo nyuma. Waabudu walitakiwa kuleta wanyama wasiokuwa na mawaa (1 Pet.1:19). Shabaha ya Mungu ni kujipatia Kanisa lisilo na mawaa (Efe.1:4; 5:27; Kol.1:22; 1 The.3:13;). Kwa nini hawatakuwa na mawaa? ni kwa sababu wamo katika Kristo asiyekuwa na mawaa, pia Mungu hana neno juu yao (Rum. 8:1,31) na damu ya Kristo yatusafisha dhambi yote (1 Yoh.1:7-8).

Agano Jipya lasema sana juu ya uwezo wa Mungu kutulinda (Yn. 10:28-29; Rum.14:4; Efe.3:20; 2 Tim.1:12; Ebr.7:25; 1 Pet.1:5)

k.25 Katika kifungu hicho cha mwisho Yuda alifika upeo katika kumsifu sana Mungu. Mungu wao ni Mungu pekee, hamna mwingine mfano wake. Ni Mungu Mwokozi, tabia na mapenzi yake ni kuokoa (Isa.45:15; 1 Tim:1:1; 2:3-5; 4:10; Tito.1:3; 2:10; 3:4; Lk. 1:47). Ameutengeneza wokovu wa wanadamu kwa njia ya Yesu Kristo, nao wameujua uwezo wake wa kuokoa. Ndipo Yuda alitangaza sifa za huyo Mungu pekee: utukufu, ukuu, uwezo, na nguvu. Ndivyo alivyo, tangu milele, hata sasa, hata milele. Ni Mungu asiyebadilika, ni Mungu asiyeweza kupatikana au kuguswa na jambo lolote au hali yoyote, yu nje na juu ya mambo yote, Mtawala. Ajabu ni kwamba kwa upendo na rehema zake amejihusisha na hao watu katika yote yaliyowapata naye ataendelea kuwa nao

na kuwalinda na kuwafikisha Kwake. Kisha Yuda alitumia neno la Kiyahudi „Amina" maana yake „iwe hivyo" yaani „ndiyo". Bila shaka walioandikiwa walitiwa moyo sana na maneno hayo. Hata sisi wa leo twatiwa moyo wa kudumu kuwa waaminifu katika imani yetu ya thamani sana (1 Pet.1:7).

MASWALI: WARAKA WA YUDA

Yuda alikuwa na shahaba gani katika kuwaandikia waumini Waraka huo?

1:3Aliwaita waumini wafanye nini kuhusu irnani? Alisemaie juu ya imani hiyo? ni nini inayobadilika; imani yenyewe? au jinsi inavyotafsiriwa katika maisha na mazingira ya wakati huo?

1:4ku Ilikuwa imetokea nini katika shirika zao? Yuda alisema sana juu ya hukumu ya Mungu - kwa nini? Toa maelezo ya hali mbovu za hao watu waliojiingiza katika shirika zao?

1:20-23 Yuda aliwashauri waumini kufanya nini kwa upande wao wenyewe na kwa wale walioguswa na hao waalirnu wa uongo?

Je! Kanisa la leo lasumbuliwa na Wakristo wa uongo na mafundisho ya uongo?
Ukijibu „ndiyo" eleza hali yao na mafundisho yao.
Kanisa lifanye nini kusaidia waumini ili wasinaswe nao?
Kanisa lifanye nini kwa hao watu?